# Nipashe

Alhamisi Oktoba 26, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581475

MWANGA WA JAMII

0745 700710 LIKE & FOLLOW US

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com





UK. 22

**BELLINGHAM FITI KUIVAA BARCA**

# Tishio jipya la vidonda tumbo

• **Mabingwa** Mloganzila wafichua vyakula hatarishi...*Endelea ukurasa 3*




## Ripoti Kamati ya PM yabaini watu 10 mtandao wa watoroshaji fedha

UKURASA 2

UKURASA WA 7

**Dk.** Mwinyi atoa miezi mitatu kwa wafanyabiashara wasilipe kodi



UKURASA WA 7

**Mke** wa Bilionea Msuya adai hakuwa na ugomvi na wifi yake aliyeuawa



UKURASA WA 19

**UN:** Mashambulizi ya Israel Gaza yanakiuka sheria





## Zambia yaikaribisha Tanzania ubia kilimo

UKURASA 2

**MICHEZO** **ROBERTINHO: AL AHLY WAMETUPA 'DARASA'** UK.24 **KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Zambia yaikaribisha Tanzania ubia kilimo

**Na Jenifer Gilla**

RAIS wa Zambia, Hakainde Hichilema, ametangaza kuipatia Tanzania ofa ya kushirikiana katika kilimo, inayonuia kwenye mapinduzi ya kilimo, kujitosheleza kwa chakula na ziada kuingizwa soko la dunia.

Hatua hiyo inachukua nafasi kwenye ugeni wa Rais Samia Suluhu Hassan akiwa jijini Lusaka, Zambia, huku serikali yake ikiwa imeshaanza kutekeleza mkakati wa kilimo biashara ambao ni sehemu ya nguzo ya uchumi wa nchi katika sura mpya.

Pia marais hao jana walishiriki tukio la utiaji saini hati nane za Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) katika sekta za maendeleo ikiwamo sayansi, teknolojia na uvumbuzi, ulinzi, huduma za kitabibu na mradi wa kusafirisha gesi asilia kupitia bomba la mafuta la TAZAMA.

Katika warsha ya utiaji saini makubaliano hayo, Rais Hichilema alisema wanaikaribisha Tanzania kushirikiana katika sekta ya kilimo ili wananchi wao wawe na chakula cha kutosha, wasifikie hatua ya kulala njaa ilhali wanazo rasilimali za kilimo za kutosha.

"Hakuna sababu ya wananchi wetu kulala bila chakula, hizi nchi mbili zimejaliwa maliasili. Lakini zaidi ya hayo tunataka kulisha Afrika na kuchangia kapu la chakula duniani ambalo ni tupu," alisema.

Rais huyo alisema ni matarajio yao kuwa ushirikiano kupitia makubaliano hayo utakuwa chachu ya mafanikio na maboresho katika sekta mbalimbali ikiwamo elimu, kuboresha miundombinu ikiwamo reli ya TAZARA, gesi, ulinzi, madini na fursa kwa vijana kujiinua kiuchumi.

"Tunataka kujifunza kutokana na hii mipaka yetu, orodha inaendelea tungependa mikataba hii, maelewano haya yasirudi nyuma. Tunaweza kuzalisha mapato kusaidia elimu na sekta nyingine za kijamii," alisema.

Rais huyo aliishukuru Tanzania kwa kuwapatia hekta 20 za ardhi katika Bandari ya Kwala. Wataitumia fursa hiyo kukuza uchumi wa nchi yao.

"Lakini ujumbe wangu kwako wa kuwapeleka Watanzania ni kwamba tunawapenda. Zambia kama nyumba ya pili kwao na kwako. Sisi siyo wachoyo.

Naye Rais Samia alisema makubaliano hayo yatakuwa suluhisho kwa changamoto za kibiashara zinazozikabili nchi hizo ikiwamo vifaa vya biashara.

"Mimi na kaka yangu tulipata fursa ya kujadili na kubadilishana mawazo juu ya masuala mbalimbali yenye maslahi kikanda na kimataifa.

"Wakati wa majadiliano yetu tuliridhishwa na juhudi za makusudi zilizofanywa na serikali zetu za kuimarisha uhusiano bora wa muda mrefu kati ya nchi zetu," alisema.

Rais Samia alisema serikali za nchi hizo zina dhamira ya dhati kuuenzi uhusiano, urafiki, ushirikiano na misingi imara iliowekwa na waasisi; Hayati Mwalimu Julius Nyerere na Kenneth Kaunda.

"Tumeona baadhi ya MoU zimetiwa saini leo (jana) na tunatarajia nyingine zitatia saini mapema zaidi kwa sababu tumewapa kazi hizo viongozi wetu wa serikali na tunaamini wataenda kuifanya. Hivyo, makubaliano zaidi yanatarajiwa kutiwa saini na hiyo ni ishara ya mafanikio," alisema.

Akihutubia Bunge la nchi hiyo, Rais Samia alisema kasi ya ushirikiano wa biashara kati ya nchi hizo mbili inaongezeka kwa kiasi kikubwa ikiwamo kutenga hekta 20 za eneo katika Bandari ya Kwala kwa ajili ya kuhifadhi mizigo inayopelekwa nchini humo.



Rais Samia Suluhu Hassan akiongoza ujumbe wa Tanzania katika mazungumzo rasmi na ujumbe wa Zambia ulioongozwa na Rais Hakainde Hichilema, Ikulu ya Lusaka jana. **PICHA: IKULU**

# Ripoti kamati ya PM yabaini watu 10 mtandao wa uhamishaji fedha

**Na Mwandishi Wetu**

RIPOTI ya uchunguzi wa tuhuma za ubadhirifu wa fedha katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji iliyoundwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, imebaini watu 10 wanahusika na mtandao wa uhamishaji fedha kinyume cha taratibu.

Taarifa ya ripoti hiyo ilikabidhiwa jana kwa Waziri Mkuu ikiwataja wahusika wa uchepushaji wa fedha hizo ambao wanatarajiwa kufikishwa mahakamani wakati wowote.

Pia wamo maofisa kutoka TAMISEMI, Hazina na baadhi ya wafanyabiashara ambao wanatumiwa ili kupitisha miamala ya fedha hizo.

Majaliwa aliunda timu hiyo akiwa katika ziara ya siku tatu iliyofanyika kuanzia Septemba 20, mwaka huu, baada ya kupata taarifa ya uwapo wa fedha zilizoingizwa kwenye akaunti ya Amana ya Halmashauri hiyo kutoka TAMISEMI na kisha fedha hizo kuondolewa baada ya muda bila maelekezo maalum wala kujua zilitumikaje.

Akizungumza jana jijini Dodoma baada ya kupokea taarifa hiyo, Majaliwa alisema: "Taarifa nimeipokea na mapendekezo ya kamati wote tumeyasikia.

"Hatua za haraka zichukuliwe kwa sababu Mheshimiwa Rais (Samia Suluhu Hassan) anatafuta fedha za kuleta maendeleo, lakini kuna watu wachache wanafanya ubadhirifu," aliagiza.

Majaliwa alisema kila mtumishi wa umma ni lazima atunze na kuratibu vizuri matumizi ya fedha zinazopatikana.

Pia, amewataka mawaziri na makatibu wakuu wasiridhishwe na taarifa za miradi wanazopokea wakiwa ziarani, kutokana na licha ya kuwa kuna wataalamu wanatoa taarifa nzuri mbele ya viongozi hao, bado kuna mbinu wanachezacheza.

Awali, akitoa taarifa ya timu kwa niaba ya wenzake, Mwenyekiti wa timu ya uchunguzi (jina linahifadhiwa) alisema timu hiyo ilibaini kuwa uchepushaji wa fedha hizo unafanyika kwa kutumia njia kadhaa ikiwamo kuomba kibali kutoka Hazina cha kuvuka na bakaa ya fedha za miradi mwaka wa fedha unapokaribia kwisha.

"Timu ya uchunguzi imebaini kuwa jumla ya Sh. milioni 463.59 zilitumwa Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma na hazikuwa kwenye mpango wala bajeti ya manispaa na hazijawahi kuombewa matumizi kama bajeti ya ziada," alibainisha.

Aliwataja watumishi wahusika na uchepushaji wa fedha hizo ni Ferdinand Filimbi, Salum Said, Kombe Kabichi, Athumani Msabila, Moses Zahuye, Jema Mbilinyi, Mhandisi Joel Shirima, Aidan Mponzi, Tumsifu Kachira na Mzee Mohamed Ubwa.

Wakati huohuo, alisema: "Timu imebaini kuwa Kitengo cha Usimamizi wa Fedha katika Akaunti Jumuifu ya Amana kilichopo TAMISEMI kinahusika kutuma fedha kwenye halmashauri mbalimbali na kisha kuzitoa kwa kushirikiana na watumishi wa halmashauri hizo."

Alisema baadhi ya halmashauri zinakuwa hazijaomba kibali cha kuvuka na fedha za bakaa kutoka HAZINA, lakini zinatumiwa fedha hizo na zipo zinazoomba kibali, lakini zinapewa pungufu ya fedha zilizoomba na zinazobakia hazijulikani zinafanya nini.

# Mshtuko ugumba

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MATUMIZI holela ya dawa za kuzuia mimba, utaratibu wa wanawake kutoa mimba mara kwa mara na maradhi ya uzazi vimetajwa kuwa chanzo kwa wanawake wengi nchini kukabiliwa na tatizo la ugumba.

Hali hiyo inaelezwa kuwa tishio kwa wanawake wengi mkoani Shinyanga wanaokabiliwa na tatizo la ugumba kwa asilimia kubwa ikiwa asilimia 30 mpaka 40 ya wanaopatiwa huduma hukutwa na tatizo hilo.

Daktari Bingwa wa magonjwa ya kinamama na uzazi kutoka Hospitali ya Rufani Mkoa wa Shinyanga, Dk. Augustino Maufi, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe kuhusu hali ya tatizo hilo.

Alisema tatizo la ugumba kwa wanawake katika Mkoa wa Shinyanga ni kubwa na asilimia 40 wanakabiliwa na tatizo la mirija ya uzazi kuziba na kusababisha kutopata watoto.

"Mkoani hapa tatizo hili ni kubwa, ukiangalia kwenye kliniki ya magonjwa ya kinamama ambayo hufanyika mara mbili kwa wiki, Jumatatu na Alhamisi asilimia 30 hadi 40 shida yao kubwa ni matatizo ya ugumba," alisema Dk. Maufi.

Alitaja baadhi ya sababu kubwa za tatizo hilo, kuwa ni utoaji mimba ovyo, matumizi holela ya dawa za kuzuia mimba ikiwamo P2, maradhi katika mfumo wa uzazi, magonjwa ya zinaa kikiwamo kisonono na kusababisha mirija ya uzazi kuziba.

Hata hivyo, alisema ugumba si kwa kinamama pekee hata wanaume wanakabiliwa na tatizo hilo kwa mbegu zao kushindwa kutunga ujauzito na kutoa wito kwa wanandoa ambao wanakabiliwa na tatizo la kukosa watoto, wahudhurie wote kwenye huduma za afya ili wapate vipimo na kutibiwa.

Dk. Maufi alisema tatizo la ugumba linatibika endapo wahusika watawahi kupata tiba na kuzingatia ushauri wa daktari na kuwataka kinamama wanaopatiwa huduma hiyo na kusikiliza ushauri wa watu wasio wataalamu kuwataka kusitisha dozi husika.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima, hivi karibuni alisema wanawake wenye matizo ya ugumba hawapaswi kunyanyapaliwa.

## HABARI KITAIFA

# Biteko awapa mbinu wawekezaji madini

**Na Gwamaka Alipipi**

NAIBU Waziri Mkuu, Dotto Biteko, amewataka wawekezaji kuwekeza katika mnyororo wa madini, ikiwamo kujenga viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazotumia madini kama malighafi.

Alitoa wito huo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua Kongamano la Kimataifa la Uwekezaji na Madini la mwaka 2023, lililozikutanisha kampuni za kimataifa za utafiti na uchimbaji, wafanyabiashara wa madini, wachimbaji wadogo, watunga sera na taasisi za kifedha.

Biteko alisema sekta ya madini ni nguzo muhimu na chachu ya maendeleo ya uchumi wa nchi, ili madini yaweze kubadilisha uchumi wa nchi na kuleta maendeleo kwa wananchi ni lazima sekta hiyo inafungamanishwa na sekta nyingine za kiuchumi kama viwanda na kilimo.

Alisema, hatua hiyo itawezesha kuzalisha bidhaa mbalimbali zinazotumia madini kama malighafi mfano mbolea, betri za magari, simu, kompyuta na bidhaa nyingine.

Biteko alisema endapo ikitekelezwa Tanzania itapata manufaa zaidi kutokana na hazina ya madini yaliyopo.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha kuwa sekta ya madini inaendelea kuongeza mchango wake katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

"Mpango wa serikali ni kuhakikisha kuwa sekta hii inachangia asilimia 10 au zaidi katika pato la taifa ifikapo mwaka 2025. Mchango wa sekta ya madini umekuwa ukiongezeka kutoka asilimia 7.3 mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 9.1 mwaka 2022," alisema Biteko.

Alisema ukuaji wa sekta ya madini kwa mwaka 2022 umekuwa kwa asilimia 10.9 ukilinganishwa na ukuaji wa asilimia 9.4 mwaka 2021, lengo la serikali ni ifikapo mwaka 2025 mchango wa sekta ya madini ufikie asilimia 10 kwenye pato la taifa.

Biteko alisema mchango wa sekta ya madini katika fedha za kigeni kwa mauzo yote ya bidhaa nje ya nchi umeendelea kuimarika kutoka Dola za Marekani bilioni 1.6 mwaka 2018 hadi Dola za Marekani bilioni 3.4 mwaka 2022.

Naibu Waziri Mkuu pia alipongeza Kampuni ya AngloGold Ashanti – GGML kwa kufadhili kongamano hilo la siku mbili.

Dk. Biteko alisema serikali imeamua kuboresha kongamano hilo ili liwe na hadhi ya kimataifa kwa lengo la kukuza sekta ya madini nchini jambo ambalo pia limeungwa na wadau wa sekta hiyo ikiwamo GGML.

"Upatikanaji wa taarifa za kijiolojia katika maeneo mengi ya nchi yetu utahamasisha kasi ya uwekezaji katika utafutaji wa kina wa madini nchini ambao ndio msingi mkubwa wa uanzishwaji wa migodi," alisema.

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, alisema katika kupata taarifa za kijiolojia, wizara imepanga kufanya utafiti kwa teknolojia ya kisasa katika eneo kubwa zaidi nchini ifikapo mwaka 2030.

Alisema upatikanaji wa taarifa za kijiolojia nchini utahamasisha kasi ya uwekezaji katika utafutaji wa kina wa madini nchini ambao ndiyo msingi mkubwa wa uanzishwaji wa migodi.

Mavunde alisema wizara itatekeleza mpango huo kupitia Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST), kwamba wizara inaendelea kutafuta fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo kuunga mkono juhudi za serikali katika kufanikisha programu hiyo.

Alisema utekelezaji wa Dira ya mwaka 2030 itakuwa ni chachu ya kuongezeka kwa shughuli za utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji, uongezaji thamani na biashara ya madini pamoja na uanzishwaji wa viwanda vinavyotumia madini kama malighafi hususani viwanda vya kuzalisha mbolea, saruji, chuma, nyaya za umeme, chokaa na vinginevyo.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha anayeshughulikia Huduma za Hazina, Jenifa Christian Omolo (kulia), akizungumza wakati akifungua Kongamano la Wakuu wa Vitengo vya Mawasiliano wa Taasisi za Wizara ya Fedha na Wahariri wa Vyombo vya Habari, mjini Morogoro jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

MAKALA MAALUM

# Tishio vidonda vya tumbo

**Na Christina Mwakangale**

HADI sasa katika jamii, vidonda vya tumbo ni sehemu ya magonjwa yanayokua kwa kasi katika jamii, huku ikirejesha maswali wanayohoji umma, nini mzizi wa kuenea kwake kwa kasi hata kuwafikia watoto hivi sasa.

Mbali ya kutajwa kitaalamu sababu zilizozoeleka; msongo wa mawazo na kukaa njaa muda mrefu, bingwa wa upasuaji na Mkuu wa Idara ya Upasuaji katika Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila, Dk. Eric Muhumba ana ufafanuzi wa ziada.

Hapo anaiambia Nipashe kwamba, matumizi ya vyakula vyenye viungo vingi, vilevile maziwa, ni sehemu ya vyanzo visababishi vya maradhi ya vidonda vya tumbo. Fuatilia mazungumzo...

**Swali:** Katika lugha ya kawaida, mfumo wa chakula ni nini?

**Dk. Muhumba:** Mfumo wa chakula ni sehemu zote za mwili, chakula kinakopita, kuanzia mdomoni hadi sehemu ya kutoa haja.

Swali: Mfumo wa chakula unatafsiri vipi maisha ya binadamu?

**Dk. Muhumba:** Mfumo wa chakula ndio uhai wa binadamu, kwa maana ya kila kiungo mwilini kinategemea chakula kutoka kwenye huo.

**Swali:** Imekuwa jambo la kawaida mfumo wa chakula kuambatana na maradhi ya vidonda vya tumbo, shida (chanzo) kuu ni nini?

**Dk. Muhumba:** Chanzo kikuu cha vidonda vya tumbo ni maambukizi ya bakteria wanaoitwa 'Helicobacter pylori' na kuzidi kwa acid (tindikali) tumboni.

**Swali:** Hospitali ya Muhimbili - Mloganzila, inaweza kubaini wenye maradhi hayo kwa idadi gani kwa kipindi cha siku?

**Dk. Muhumba:** Kwa siku tunawabaini wenye maradhi hayo kati ya wawili hadi watano.

**Swali:** Makundi gani katika jamii, umri, jinsi hukumbwa zaidi na maradhi hayo?

**Dk. Muhumba:** Ni umri wowote, ingawa kwa watoto ni mara chache sana kuona wenye vidonda vya tumbo.

**Swali:** Kuna aina ngapi za vidonda vya tumbo?

**Dk. Muhumba:** Kuna aina mbili, ya kwanza tumbo (gastric) na utumbo mdogo (duodenal).

**Swali:** Je, kuna uhusiano wowote kati ya maradhi na hali ya hewa, mtindo wa maisha na mazingira ya mlo?

**Dk. Muhumba:** Vidonda vya tumbo vinahusishwa na 'stress' (msongo wa mawazo) za maisha, kukaa na njaa kwa muda mrefu, kula vyakula vya jamii ya maharage, vyakula vyenye viungo vingi, maziwa na kadhalika.

Swali: Kwanini maradhi haya yanahusianishwa na maisha ya binadamu hasa msongo?

**Dk. Muhumba:** Wenye msongo wa mawazo huzalisha kiwango kikubwa cha 'acid' wanapokuwa kwenye hali hiyo na kuathiri tumbo.

**Swali:** Walio katika hatari ya kupata maradhi hayo ni wasiopata mlo au chakula ndani ya saa nyingi, kama jamii inavyotafsiri?

**Dk. Muhumba:** Ni kweli wanaokaa bila kula kwa muda mrefu wanapata vidonda vya tumbo kirahisi zaidi ya wale wanaokula kila mara, ingawa kuna baadhi ya watu wakiwa na vidonda wanaongeza kula mara kwa mara, sababu wanapata nafuu wanapokula.

**Swali:** Kama mtaalamu, mnatafsiri vipi maradhi hayo na mabadiliko pamoja namna ya kukabiliana nayo?

**Dk. Muhumba:** Mabadiliko ya nini? Jinsi ya kukabiliana nayo ni kwenda hospitali, ambako watapima na kugundua vidonda na kama una maambukizi ya 'Helicobacter pylori'(wadudu visababishi) ili upate matibabu.

Swali: Kama mtaalamu, kuna aina gani ya maradhi yanaendana na vidonda vya tumbo?

**Dk. Muhumba:** Kuwa na uzalishaji mkubwa wa 'acid' tumboni na maambukizi ya 'Helicobacter pylori'.

**Swali:** Vidonda vya tumbo, vinasababishwa na aina gani ya bakteria? Je, vinatibika, vina hatua mbaya hadi kuhitaji upasuaji? Baadhi nimeshuhudia wakipunguzwa utumbo au wanaotumia dawa za kudumu yaani maisha yao yote.

**Dk. Muhumba:** Vinasababishwa na 'Helicobacter pylori'. Matibabu ni magumu kidogo, kwa sababu 'acid' inazalishwa na mwili wako na tiba yetu kazi yake kubwa ni kupunguza uzalishaji wa 'acids', ingawa ukiacha dawa ni rahisi uzalishaji kurudia kiwango chake cha awali.

Athari kubwa ya vidonda vya tumbo ni kuta za tumbo kuvimba na kuziba njia ya chakula kuingia kwenye utumbo mdogo (pyloric stenosis).

Pili, ni kidonda kumwaga damu tumboni hadi kusababisha mtu kutapika damu.

Ya tatu, ni tumbo kutoboka, hivyo 'acids' kusambaa tumboni na kuleta maumivu makali sana yanayohitaji upasuaji wa haraka, kwenda kuziba pale palikotoboka au kupunguza tumbo.

**Swali:** Aina gani ya kasoro zilizopo kwenye jamii ili kufanikisha mapambano dhidi ya 'ulcers?

**Dk. Muhumba:** Kushindwa kuzuia maambukizi ya 'Helicobacter pylori', ambayo yanaenezwa kwa kula chakula kilicho na uchafu, hasa kinyesi.

**Swali:** Tiba yake ni nini na mtu anawezaje kujikinga? Wanaougua hushauriwa mlo wa aina gani mara ngapi kwa siku?

**Dk. Muhumba:** Tiba ya kwanza ya vidonda vya tumbo, ni kumaliza maambukizi ya 'Helicobacter pylori.'

Pili, kupunguza kiasi cha 'acids' tumboni na tatu ni kutokula vyakula vinavyoleta maumivu ya tumbo.

**TANGAZO**

Access Microfinance Bank Tanzania

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZISIZOKAGULIWA KWA UMMA

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2023

| | | (Kiasi kwa shilingi milioni) Robo Mwaka ya sasa 30 SEPTEMBA 2023 | Robo Mwaka iliopita 30 JUNI 2023 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 5,396 | 4,775 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 8,991 | 8,070 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 375 | 226 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 28 | 22 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 200 | 200 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 53,945 | 52,875 |
| 12 | Mali Nyingine | 7,592 | 8,499 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 729 | 788 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **77,256** | **75,455** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | 700 |
| 18 | Amana za Wateja | 59,647 | 57,130 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 951 | 1,020 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 1,578 | 2,107 |
| 27 | Dhima Nyingine | 6,344 | 6,057 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **68,520** | **67,014** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **8,736** | **8,441** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 40,000 | 40,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (32,537) | (32,537) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,273 | 978 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **8,736** | **8,441** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 170 | 495 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 4,414 | 4,782 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 4,495 | 4,783 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 64 | 64 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 11.31% | 11.19% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 7.55% | 8.29% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 97.98% | 99.70% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 69.83% | 70.07% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 70.09% | 70.34% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 3.14% | 4.93% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 2.39% | 4.18% |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBNA 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kipindi cha sasa hadi 30 Septemba 2023** | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 2023 | 40,000 | - | (32,537) | - | - | 7,463 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,273 | - | - | 1,273 |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa 30 Septemba 2023** | **40,000** | **-** | **(31,264)** | **-** | **-** | **8,736** |
| **Kipindi cha Mwaka uliopita hadi 31 Disemba 2022** | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 2022 | 40,000 | - | (33,813) | 229 | - | 6,416 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,047 | - | - | 1,047 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 229 | (229) | - | - |
| **Salio la mwisho wa 31 Disemba 2022** | **40,000** | **-** | **(32,537)** | **-** | **-** | **7,463** |






## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka sasa 30 SEPTEMBA 2023 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30 SEPTEMBA 2022 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30 SEPTEMBA 2023 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30 SEPTEMBA 2022 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 6,253 | 5,341 | 18,259 | 14,762 |
| 2 Gharama za Riba | (1,212) | (1,014) | (3,596) | (2,467) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | 5,041 | 4,327 | 14,662 | 12,295 |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | 0 |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (349) | (747) | (1,124) | (2,017) |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,257** | **1,395** | **3,649** | **3,386** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | (65) | 39 | (8) | 63 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 423 | 344 | 1,142 | 978 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 899 | 1,012 | 2,515 | 2,344 |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **(5,497)** | **(4,642)** | **(15,647)** | **(13,008)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (3,088) | (2,931) | (9,320) | (8,305) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | (120) | (141) | (394) | (408) |
| 7.3 Gharama Nyingine | (2,290) | (1,570) | (5,933) | (4,295) |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **452** | **333** | **1,536** | **656** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | (157) | (73) | (263) | (97) |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **295** | **260** | **1,273** | **559** |
| 11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **295** | **260** | **1,273** | **559** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 380 | 401 | 380 | 401 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 30 | 26 | 42 | 19 |
| 15 Idadi ya Matawi | 8 | 8 | 8 | 8 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.53% | 1.56% | 2.27% | 1.18% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 13.65% | 15.09% | 20.70% | 11.41% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 73.20% | 68.92% | 71.42% | 71.68% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 37.54% | 38.13% | 37.77% | 38.75% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho.**

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo Mwaka ya sasa 30 SEPTEMBA 2023 | Robo Mwaka iliyopita 30 JUNI 2023 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30 SEPTEMBA 2023 | Limbikizo la robo Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30 SEPTEMBA 2022 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 452 | 513 | 1,536 | 655 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 764 | 737 | 2,394 | 2,832 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1,070) | (2,751) | (7,174) | (8,624) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 1,817 | 2,716 | 6,219 | 7,755 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (291) | (266) | (420) | (1,382) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 964 | 610 | 1,208 | (248) |
| - Kodi Iliyolipwa | (75) | (390) | (540) | (218) |
| - Mengineyo (bainisha) | (219) | (86) | (364) | (442) |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **2,342** | **1,082** | **2,860** | **328** |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (57) | (157) | (257) | (134) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | 6 | 6 | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato ahirishwa | (603) | (2) | (622) | (60) |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(660)** | **(153)** | **(873)** | **(194)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | (204) | (302) | (730) | - |
| Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | **(204)** | **(302)** | **(730)** | **-** |
| | | | - | - |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **1,478** | **627** | **1,257** | **134** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Kipindi | **10,056** | **9,429** | **10,277** | **10,411** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Kipindi | **11,534** | **10,056** | **11,534** | **10,545** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2023

Imesainiwa na: Julius J Ruwaichi — Imesahiniwa — Mtendaji Mkuu — Tarehe: 23 Oktoba 2023

Imesainiwa na: Tajinder Singh — Imesahiniwa — Mkuu wa Idara ya Fedha — Tarehe: 23 Oktoba 2023

Imesainiwa na: Catherine Temu — Imesahiniwa — Mkaguzi Mkuu wa Ndani — Tarehe: 23 Oktoba 2023

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2016, na zinaonyesha hali halisi.

Imesainiwa na: Thomas Engelhardt — Imesahiniwa — Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi — Tarehe: 23 Oktoba 2023

Imesainiwa na: Johannes Mainhard — Imesahiniwa — Mkurugenzi — Tarehe: 23 Oktoba 2023

# ACCESS MICROFINANCE BANK TANZANIA LIMITED
# MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| DESCRIPTION | CHARGE/FEE | |
|---|---|---|
| **ACCESS RAHISI,NORMAL SAVINGS, RAHISI CAA, ELIMU, AND KIKUNDI ACCOUNT(RAHISI ACCOUNT)** | **TZS** | **USD** |
| Required minimum opening balance | 10,000.00 | - |
| Monthly service fees | 2,000.00 | - |
| Cash withdrawal over counter up to 10M | 3,000.00 | - |
| Cash withdrawal over counter >10M | 10,000 | - |
| Bank statement 1free per month | FREE | - |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | - |
| New ATM card issuance | 10,000.00 | - |
| ATM card renewal or replacement | 15,000.00 | - |
| Replacement of the PIN | 10,000.00 | - |
| Standing order Internal | 2,000.00 | - |
| Standing order External | 12,980.00 | - |
| Dormant account fee | FREE | - |
| Interbank transfer | 10,000.00 | - |
| International transfer | $ 55 | 55.00 |
| Closure of account | 20,000.00 | - |
| **NUFAIKA TRANSACTIONAL ACCOUNT** | | |
| Required minimum opening balance | 50,000.00 | 25.00 |
| Monthly service fees | 6,000.00 | 3.00 |
| Bank statement 1free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| New ATM card issuance | 15,000.00 | N/A |
| Fees per ATM withdrawal | 2,000.00 | N/A |
| Interbank transfer | 10,000.00 | 4.20 |
| International transfer | $ 55 | 55.00 |
| ATM mini statement | 1,000.00 | N/A |
| Standing order Internal | 2,000.00 | 1.00 |
| Standing order External | 12,980.00 | 12.98 |
| Dormant account fee | FREE | FREE |
| Reactivation of Dormant account | FREE | FREE |
| Letter of recommendation and certificate of balance | 50,000.00 | 23.00 |
| **NORMAL CURRENT ACCOUNT (NUFAIKA ACCOUNTS)** | **TZS** | **USD/EURO** |
| Required minimum opening balance | 100,000.00 | 50.00 |
| Monthly service fees | 6,000.00 | 3.00 |
| Cash withdrawal over counter up to 10M | 3,000.00 | 0.18% |
| Cash withdrawal over counter >10M | 10,000 | 10 |
| Fees per ATM withdrawal | 2,000.00 | N/A |
| ATM mini statement | 1,000.00 | N/A |
| Bank statement 1free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 25 leaves | 20,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 50 leaves | 35,000.00 | 15.00 |
| Dishonored cheque | 30,000.00 | 30.00 |
| Bankers Cheque | 50,000.00 | FREE |
| Stop payment | 30,000.00 | 30.00 |
| Standing order Internal | 2,000.00 | 1.00 |
| Standing order External | 12,980.00 | 12.98 |
| Balance enquiry | 1,000.00 | 1.00 |
| New ATM card issuance | 15,000.00 | N/A |
| ATM card renewal or replacement | 15,000.00 | N/A |
| Interbank transfer | 10,000.00 | 4.20 |
| International transfer | $ 55 | 55.00 |
| Dormant account fee | FREE | FREE |
| Reactivation of Dormant account | FREE | FREE |
| Letter of recommendation and certificate of balance | 50,000.00 | 23.00 |
| **SPECIAL ACCESS NUFAIKA ACCOUNT** | **TZS** | **USD/EURO** |
| Required minimum opening balance | 100,000.00 | 50.00 |
| Monthly service fees | 60,000.00 | 50.00 |
| Minimum monthly turover | 20,000,000.00 | 10,000.00 |
| Cash withdrawal over counter | FREE | 0.18% |
| Fees per ATM withdrawal | 2,000.00 | N/A |
| ATM mini statement | 1,000.00 | N/A |
| Bank statement 1free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 25 leaves | 20,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 50 leaves | 35,000.00 | 15.00 |
| Dishonored cheque | 30,000.00 | 30.00 |
| Bankers Cheque | 50,000.00 | FREE |
| Stop payment | 30,000.00 | 30.00 |
| Standing order Internal | 2,000.00 | 1.00 |
| Standing order External | 12,980.00 | 12.98 |
| Balance enquiry | 1,000.00 | 1.00 |
| New ATM card issuance | 15,000.00 | N/A |
| ATM card renewal or replacement | 15,000.00 | N/A |
| Interbank transfer | FREE | FREE |
| International transfer | $ 55 | 55.00 |
| Dormant account fee | 5,000.00 | 5.00 |
| Reactivation of Dormant account | FREE | FREE |
| Letter of recommendation and certificate of balance | 50,000.00 | 23.00 |
| **MIKAKATI SAVING ACCOUNTS** | **TZS** | **USD/EURO** |
| Required minimum opening balance | 20,000.00 | 20.00 |
| monthly service fees | FREE | FREE |
| Bank statement 1free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| Cash withdrawal over counter | 1 FREE PER MONTH | 1 FREE PER MONTH |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | 20,000.00 | 20.00 |
| Dormant account fee | FREE | FREE |
| International transfer | $ 55 | 55.00 |
| Account closure | 12,000.00 | 5.00 |
| **MIKAKATI PLUS SAVING ACCOUNTS** | **TZS** | **USD/EURO** |
| Required minimum opening balance | 10,000.00 | |
| monthly service fees | FREE | |
| Bank statement 1free per month | FREE | |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | |
| Cash withdrawal over counter | 1 FREE PER MONTH | |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | 5,000.00 | |
| Dormant account fee | FREE | |
| International transfer | $ 55 | 55.00 |
| Account closure | 12,000.00 | |
| **KIKUNDI SAVING ACCOUNT** | **TZS** | |
| Required minimum opening balance | 10,000.00 | |
| monthly service fees | FREE | |
| Bank statement 1free per month | FREE | |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | |
| Cash withdrawal over counter | 3,000.00 | |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | 3,000 | |
| Dormant account fee | FREE | |
| International transfer | $ 55 | |
| Account closure | FREE | |
| **BARAKA JUNIOR ACCOUNT** | **TZS** | **USD/EURO** |
| Required minimum opening balance | - | - |
| monthly service fees | FREE | FREE |
| Bank statement 1free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| Cash withdrawal over counter | FREE | FREE |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | FREE | FREE |
| Dormant account fee | FREE | FREE |
| International transfer | $ 55 | 55.00 |
| Account closure | FREE | FREE |

**TERM DEPOSIT RATES 2022**

| Amount | Interest Rates |
|---|---|
| 5,000,000 - 500,000,000 | 3% - 12% p.a |
| >500,000,000 | Negotiation |

| AGENCY BANKING | To Govt | Old Customer Fee | To AMBT | To Agent | New Customer Fee |
|---|---|---|---|---|---|
| **Withdrawal (TZS) (agents) Range** | | | TZS | | |
| 1 - 2,999 | 10 | 710 | 450 | 350 | 810 |
| 3,000 - 3,999 | 14 | 711 | 450 | 350 | 814 |
| 4,000 - 4,999 | 27 | 719 | 450 | 350 | 827 |
| 5,000 - 6,999 | 54 | 739 | 450 | 350 | 854 |
| 7,000 - 9,999 | 56 | 770 | 450 | 350 | 856 |
| 10,000 - 14,999 | 102 | 788 | 450 | 350 | 902 |
| 15,000 - 19,999 | 195 | 924 | 450 | 350 | 995 |
| 20,000 - 20,000 | 306 | 1,127 | 450 | 350 | 1,106 |
| 20,001 - 29,999 | 306 | 1,372 | 1,400 | 700 | 2,406 |
| 30,000 - 39,999 | 351 | 2,672 | 1,400 | 700 | 2,451 |
| 40,000 - 49,999 | 419 | 2,770 | 1,400 | 700 | 2,519 |
| 50,000 - 99,999 | 573 | 3,050 | 1,400 | 700 | 2,673 |
| 100,000 - 100,000 | 707 | 3,435 | 1,400 | 700 | 2,807 |
| 100,001 - 199,999 | 707 | 3,771 | 2,620 | 980 | 4,307 |
| 200,000 - 200,000 | 821 | 5,271 | 2,620 | 980 | 4,421 |
| 200,001 - 299,999 | 821 | 5,558 | 3,325 | 1,275 | 5,421 |
| 300,000 - 300,000 | 838 | 6,558 | 3,325 | 1,275 | 5,438 |
| 300,001 - 399,999 | 838 | 6,950 | 3,950 | 1,650 | 6,438 |
| 400,000 - 499,999 | 982 | 7,950 | 3,950 | 1,650 | 6,582 |
| 500,000 - 599,999 | 1,245 | 8,370 | 3,950 | 1,650 | 6,845 |
| 600,000 - 699,999 | 1,532 | 9,140 | 3,950 | 1,650 | 7,132 |
| 700,000 - 750,000 | 1,700 | 9,980 | 3,950 | 1,650 | 7,300 |
| 750,001 - 799,999 | 1,700 | 10,470 | 4,850 | 2,250 | 8,800 |
| 800,000 - 899,999 | 1,500 | 11,970 | 4,850 | 2,250 | 8,600 |
| 900,000 - 1,000,000 | 1,776 | 12,264 | 4,850 | 2,250 | 8,876 |
| 1,000,0001 - 3,000,000 | 1,875 | 13,230 | 4,850 | 2,250 | 8,975 |
| 3,000,0001 - 5,000,000 | 2,000 | 13,580 | 4,850 | 2,250 | 9,100 |
| **Deposit (TZS) (agents) Range** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | **To AMBT** | **To Agent** | **New Customer Fee** |
| 0 - 10,000 | - | - | - | 100 | - |
| 10,001 - 20,000 | - | - | - | 150 | - |
| 20,001 - 50,000 | - | - | - | 200 | - |
| 50,001 - 100,000 | - | - | - | 350 | - |
| 100,001 - 150,000 | - | - | - | 550 | - |
| 150,001 - 200,000 | - | - | - | 700 | - |
| 200,001 - 250,000 | - | - | - | 850 | - |
| 250,001 - 300,000 | - | - | - | 900 | - |
| 300,001 - 500,000 | - | - | - | 1,100 | - |
| 500,001 - 750,000 | - | - | - | 1,200 | - |
| 750,001 - 3,000,000 | - | - | - | 1,600 | - |
| 3,000,001 - 5,000,000 | - | - | - | 1,600 | - |
| **MOBILE BANKING** | | | | | |
| **Withdrawal - Bank to Wallet (TZS)** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | **To AMBT** | | **New Customer Fee** |
| 100-2,999 | 10 | 500 | 500 | | 510 |
| 3,000-3,999 | 14 | 500 | 500 | | 514 |
| 4,000-4,999 | 27 | 500 | 500 | | 527 |
| 5,000-6,999 | 54 | 500 | 500 | | 554 |
| 7,000-9,999 | 56 | 500 | 500 | | 556 |
| 10,000-14,999 | 102 | 500 | 500 | | 602 |
| 15,000-19,999 | 195 | 500 | 500 | | 695 |
| 20,000-29,999 | 306 | 500 | 500 | | 806 |
| 30,000-39,999 | 351 | 500 | 500 | | 851 |
| 40,000-49,999 | 419 | 500 | 500 | | 919 |
| 50,000-50,000 | 573 | 500 | 500 | | 1,073 |
| 50,001-99,999 | 573 | 1,000 | 1,000 | | 1,573 |
| 100,000-100,000 | 707 | 1,000 | 1,000 | | 1,707 |
| 100,000-199,999 | 707 | 2,000 | 2,000 | | 2,707 |
| 200,000-250,000 | 821 | 2,000 | 2,000 | | 2,821 |
| 250,001-299,999 | 821 | 3,000 | 3,000 | | 3,821 |
| 300,000-399,999 | 838 | 3,000 | 3,000 | | 3,838 |
| 400,000-499,999 | 982 | 3,000 | 3,000 | | 3,982 |
| 500,000-599,999 | 1,245 | 3,000 | 3,000 | | 4,245 |
| 600,000-699,999 | 1,532 | 3,000 | 3,000 | | 4,532 |
| 700,000-750,000 | 1,700 | 3,000 | 3,000 | | 4,700 |
| 750,001-799,999 | 1,700 | 4,000 | 4,000 | | 5,700 |
| 800,000-899,999 | 1,500 | 4,000 | 4,000 | | 5,500 |
| 900,000-1,000,000 | 1,776 | 4,000 | 4,000 | | 5,776 |
| 1,000,001-3,000,000 | 1,875 | 4,000 | 4,000 | | 5,875 |
| 3,000,001-5,000,000 | 2,000 | 4,000 | 4,500 | | 6,500 |
| **Deposit (TZS) (Wallet to Bank)** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | **To AMBT** | | **New Customer Fee** |
| 0 - 50,000 | - | FREE | - | | - |
| 50,001 - 100,000 | - | FREE | - | | - |
| 100,001 - 250,000 | - | FREE | - | | - |
| 250,001 - 750,000 | - | FREE | - | | - |
| 750,001 - 3,000,000 | - | FREE | - | | - |
| **Air-time top-up** | - | FREE | - | | - |
| **Utility payments** | - | FREE | - | | - |
| **Balance inquiry** | - | 100 | 300 | | 300 |
| **Mini-statement** | - | 200 | 300 | | 300 |
| **Full account statement request** | - | 500 | 500 | | 500 |
| **Cheque book request** | - | 600 | 600 | | 600 |
| **AMBT internal transfers (same account holder)** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | **To AMBT** | | **New Customer Fee** |
| 1 - 999 | - | - | FREE | | - |
| 1,000 - 1,999 | - | 10 | FREE | | - |
| 2,000 - 2,999 | - | 11 | FREE | | - |
| 3,000 - 3,999 | - | 19 | FREE | | - |
| 4,000 - 4,999 | - | 39 | FREE | | - |
| 5,000 - 6,999 | - | 70 | FREE | | - |
| 7,000 - 9,999 | - | 88 | FREE | | - |
| 10,000 - 14,999 | - | 224 | FREE | | - |
| 15,000 - 19,999 | - | 427 | FREE | | - |
| 20,000 - 29,999 | - | 672 | FREE | | - |
| 30,000 - 39,999 | - | 770 | FREE | | - |
| 40,000 - 49,999 | - | 1,050 | FREE | | - |
| 50,000 - 99,999 | - | 1,435 | FREE | | - |
| 100,000 - 199,999 | - | 1,771 | FREE | | - |
| 200,000, 299,999 | - | 2,058 | FREE | | - |
| 300,000 - 399,999 | - | 2,450 | FREE | | - |
| 400,000 - 499,999 | - | 2,870 | FREE | | - |
| 500,000 - 599,999 | - | 3,640 | FREE | | - |
| 600,000 - 699,999 | - | 4,480 | FREE | | - |
| 700,000 - 799,999 | - | 4,970 | FREE | | - |
| 800,000 - 899,999 | - | 5,264 | FREE | | - |
| 900,000 - 1,000,000 | - | 6,230 | FREE | | - |
| 1,000,001 - 3,000,000 | - | 6,580 | FREE | | - |
| **AMBT internal outgoing transfers (other account holder)** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | **To AMBT** | | **New Customer Fee** |
| 1 - 2,999 | 10 | 510 | 500 | | 510 |
| 3,000 - 3,999 | 14 | 511 | 500 | | 514 |
| 4,000 - 4,999 | 27 | 519 | 500 | | 527 |
| 5,000 - 6,999 | 54 | 539 | 500 | | 554 |
| 7,000 - 9,999 | 56 | 570 | 500 | | 556 |
| 10,000 - 14,999 | 102 | 588 | 500 | | 602 |
| 15,000 - 19,999 | 195 | 724 | 500 | | 695 |
| 20,000 - 29,999 | 306 | 927 | 500 | | 806 |
| 30,000 - 39,999 | 351 | 1,172 | 500 | | 851 |
| 40,000 - 49,999 | 419 | 1,270 | 500 | | 919 |
| 50,000 - 99,999 | 573 | 1,550 | 500 | | 1,073 |
| 100,000 - 199,999 | 707 | 1,935 | 500 | | 1,207 |
| 200,000 - 299,999 | 821 | 2,271 | 500 | | 1,321 |
| 300,000 - 399,999 | 838 | 2,558 | 500 | | 1,338 |
| 400,000 - 499,999 | 982 | 2,950 | 500 | | 1,482 |
| 500,000 - 599,999 | 1,245 | 3,370 | 500 | | 1,745 |
| 600,000 - 699,999 | 1,532 | 4,140 | 500 | | 2,032 |
| 700,000 - 799,999 | 1,700 | 4,980 | 500 | | 2,200 |
| 800,000 - 899,999 | 1,500 | 5,470 | 500 | | 2,000 |
| 900,000 - 1,000,000 | 1,776 | 5,764 | 500 | | 2,276 |
| 1,000,001 - 3,000,000 | 1,875 | 6,730 | 500 | | 2,375 |
| 3,000,001 - 5,000,000 | 2,000 | 7,080 | 500 | | 2,500 |
| **FOREIGN EXCHANGE TRANSACTION** | | | **TZS** | **USD** | |
| Telegraphic Transfer - Normal Customer (SWIFT) | | | 55.00 | 55.00 | |
| TISS- Normal Customer | | | 10,000.00 | 4.20 | |
| TISS-Staff | | | 6,000.00 | 2.10 | |
| **LOAN PRODUCT LENDING RATES** | | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | from 36% to 72% Based on risk profile/risk group of client | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 35,000,000 | | | from 36% to 60% Based on risk profile/risk group of client | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 35,000,000 | | | from 30% to 74.4% Based on risk Profile/Risk Group of client | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | | | from 26.4% to 33.6% Based on risk profile/Risk Group of client. | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | | 20.40% | N/A | |
| **Loan Processing Fee** | | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | 3.40%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | | | 3.40%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | | | 3.70%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | | | 2.90%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | | 1.5% Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| **Application Fee** | | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | | 20,000.00 | N/A | |
| **Insurance Fee** | | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | 1.5% | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | | | 1.5% | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | | | 2.9% | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 150,000,000 | | | 1.5% | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | | 1.5% | N/A | |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# 'Nitumie kwa namba hii' mtakipata mnachokitafuta

**WIZI** kwa njia ya mitandao ya simu umeendelea kushamiri kila siku na watu wanatapeliwa pesa zao kwa kutozingatia tahadhari zinazotolewa na Jeshi la Polisi na Mamlaka ya Mawasiliano Nchini (TCRA).

Watu wanaotumia wizi wa mitandao huja na mbinu tofauti kwa kumpigia mteja wa mtandao wa kampuni yoyote ya simu na kumtaka afuate maelekezo wakidai kuwa kuna maboresho yanafanyika.

Mteja atakapofuata maelekezo hayo hujikuta akipoteza pesa zake alizozihifadhi kwenye simu yake.

Njia nyingine wanayotumia matapeli hao ni kutuma ujumbe wa muamala kuonyesha pesa imeingia kwenye simu na tapeli humpigia mhusika mwenye simu kumtaarifu kuwa kuna pesa imeingia kimakosa na kumtaka arudishe kwa namba atakayotumiwa.

Mteja atakapotuma pesa hujikuta alichotumia ni akiba yake aliyonayo kwenye simu na anapojaribu kupiga namba aliyotuma muamala, inakuwa haipatikani tena.

Watu wengi wamelizwa kwa njia hiyo kwa kujikuta wakipoteza pesa nyingi kwa kuwatumia matapeli hao.

Hata hivyo, kuna maswali mengi ya kujiuliza, inakuaje mtu ajue namba yako na kama simu yako ina pesa.

Kuna uwezekano mkubwa kuwa wanaofanya utapeli huo ni watu waliowahi kufanya kwenye kampuni za simu na kufahamu mbinu za kufanya wizi huo.

Pia kumekuwa na madai ya vijana wanaotumika kusajili laini za simu kwa kupita mitaani kuwa pia wanahusika kufanya utapeli huo.

Katika kudhibiti utapeli huo, TCRA imesema imezifungia namba za simu 34,848 zilizoripotiwa kupotea, kuibiwa na kuhusika katika matukio ya uhalifu katika kipindi cha Julai hadi Septemba, mwaka huu.

Aidha, imezifungia simu zilizobainika kuhusika na viashiria vya ulaghai kuanzia kipindi hicho kuwa ni 23,328 ikilinganishwa na 23,234 kati ya Aprili hadi Juni, mwaka huu.

Ujumbe wa ulaghai unaotumwa kwenye siku ni 'nitumie kwa namba hii', 'ile kodi tuma kwenye namba hii' au tapeli hupiga na kuongea kwa sauti ya unyonge kuwa ametuma kimakosa pesa ya matibabu ya mgonjwa wake.

Mamlaka hiyo ikitoa taarifa ya mwenendo wa sekta ya mawasiliano katika kipindi cha Julai hadi Septemba, mwaka huu, imeeleza kuwa kufungiwa kwa simu hizo, kumetokana na elimu kwa wananchi iliyotolewa ya matumizi ya namba 15040 ya kuripoti namba za simu za uhalifu na ulaghai.

Kufungiwa kwa simu hizo pia kumewezesha kupunguza matukio ya wizi na kusaidia upatikanaji wa vifaa vya mawasiliano vyenye ubora.

Mamlaka hiyo imeendelea kutoa elimu kwa umma na kuhamasisha usalama mtandaoni na kampeni ya "Futa Delete Kabisa" na kuwakumbusha wananchi kuepuka kusambaza taarifa zozote zisizo za uhakika na uchochezi.

Imesisitiza mtu akipokea jumbe ya kitapeli au simu ya kitapeli atume kwenda namba 15040 na kutoamini simu ya mtoa huduma wa mawasiliano ambayo siyo namba 100.

Wateja wa mitandao ya simu ni lazima wawe makini kwa sababu matapeli wa mtandaoni wana mbinu nyingi za kuibia watu.

Jeshi la Polisi kila mara limekuwa likituma ujumbe kwenye simu kuwataarifu wananchi wasikubali kurubuniwa na matapeli na wanapotumiwa ujumbe wa kitapeli waripoti namba hizo ili ziweze kufutwa.

Watu walioripoti namba hizo wamepata ushirikiano na nyingi zimefutwa kwa kushirikiana na TCRA na kampuni za simu.

Umakini na tahadhari zikizingatiwa utapeli wa kimtandao hautakuwa na nafasi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wahitimu changamkieni fursa za maisha, msibweteke mitaani

Na Mary Seme

**HIVI** karibuni baadhi ya vyuo vimetunukisha shahada mbalimbali kwa wahitimu kutoka vyuo hivyo ikiwa ni utaratibu wa kawaida kufanya hivyo kila mwaka.

Yaani kila mwaka maelfu ya wanafunzi wanamaliza elimu ya juu katika fani mbalimbali na kuingia mtaani pasipo kujua nini watafanya.

Kutokana na wingi wa wahitimu kutoka vyuo mbalimbali nchini kumekuwa na changamoto ya ajira kwa vijana wengi hasa kwa miaka ya hivi karibuni. Hali hii ni kutokana na kuwa na wasomi wengi huku taasisi nyingi zikiwa na wafanyakazi wengi waliojitosheleza katika fani mbalimbali na kuwafanya vijana wengi wanaotoka vyuoni kukosa ajira. Ni muhimu sasa kwa serikali kutoa vipaumbele kwa wimbi kubwa la vijana walohitimu waliopo mtaani kwa kuwawezesha fedha ili waweze kushirikiana katika vikundi vidogo vidogo na kuanzisha biashara zitakazo wasaidia kukidhi maisha yao pindi wawapo mtaani. Hata hivyo, ni vyema pia kwa wahitimu kushirikiana na ndugu jamaa na marafiki wakabuni mbinu mbalimbali za ujasiriamali kwa kuzingatia changamoto zilizopo katika jamii vinginevyo wataendelea kulia na uhaba wa ajira.

Kuhitimu shahada ya chuo kikuu kisiwe kikwazo katika kujitafutia kipato kupitia shughuli mbalimbali kama vile kilimo, ufugaji, sanaa, uvuvi nakadhalika kwa kuzingatia eneo au jamii anapotokea mhitimu husika kwa kuwa fursa hazifanani kwa kila eneo.

Kwa mfano, kwa mhitimu anayetokea Kanda ya Ziwa anaweza kufanya shughuli za uvuvi kwa kuwa ni maeneo zinapofanyika sana shughuli za aina hiyo tofauti na kanda ya kati katika mikoa ya Singida na Dodoma ambapo hakuna maeneo ya kufanya uvuvi labda tu iwe ni samaki wa kufuga katika bwawa la kuchimbwa na binadamu.

Si vibaya kufanya kitu nje ya kile ulichosomea ilimradi tu kupata kipato cha kukidhi mahitaji muhimu na iwe ni kazi halali inayokubalika kwa mujibu wa sheria. Mimi ninawafahamu wahitimu walioamua kujiajiri katika fani tofauti na ile waliyoisomea na sasa wanamaisha mazuri kwa msemo wa mtaani 'wameyapatia maisha'. Hivyo vijana acheni kubweteka na kuilalamikia serikali kuwa hakuna ajira ilihali 'vijana ni nguvukazi ya Taifa' na mnaweza kufanya kazi yeyote itakayoweza kuwapitia ridhiki.

Wapo vijana wengi ambao wameamua kuungana pamoja na kujiingiza katika ujasiriamali huku wakikopa fedha katika vikundi vya kijamii kama vile 'SACCOS' ambapo wameweza kujishughulisha katika ufugaji wa samaki, kilimo cha bustani n.k na wameweza kuendesha maisha yao kupitia biashara hizo walizozibaini.

Ukiingia mtaani na kiburi cha usomi na kukataa kuendana na mazingira mtaa nao utakuonyesha kiburi kwa kukataa kufungua fursa kwa ajili yako, matokeo yake utaendela kulalamika na mwisho wa malalamiko utagundua hakuna kilichobadilika katika maisha. Maisha hayakusubiri ujifunze kwanza, yanaendelea na utaratibu wake wa siku zote.

Hivyo, ipo haja kwa wahitimu kutokukuchagua kazi ya kufanya pindi wanapomaliza masomo yao vyuoni, na kuondokana na ile dhana ya kuwa wao ni wasomi na wanasubiri kuajiriwa serikarini.

Vijana kuweni na 'Jicho la tatu' katika kutafuta kazi na sio kusubiri ajira kwani kazi ni kazi tu mathalani ni kazi ya halali na inakuingizia kipato na maisha yanaendelea.

Kwa kufanya hivyo, kila kijana itamsaidia kuachana na tabia ya kulalamika pasipo sababu na wengine kushinda vijiweni huku wakilalamika kuwa kuna uhaba wa ajira.

Vijana wengi sana wamejikuta wakijiingiza katika makundi yasiyofaa kama vile uvutaji bangi, ulevi, uporaji na baadhi ya wadada wamekuwa wakifanya kazi ya kuuza miili yao.

Huku vijana wengine wakiamua kufanya kazi zenye faida kwao na kuendesha maisha yao na kuachana na biashara zisizo na manufaa kwao.

Ni vyema kwa wahitimu sasa kuachana na dhana ya kuwa Tanzania hakuna ajira badala yake wasibweteke mitaani kusubiri kuajiliwa na serikali, badala yake wafanye kazi na wajiingize katika kila fursa inayokuja mbele yao na kwa kufanya hivyo itawafanya waishi maisha ya kujitegemea kiuchumi na kifedha. ALLAMSIKI

## HABARI KITAIFA

# Dk. Mwinyi atoa miezi mitatu wafanyabiashara wasilipe kodi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ametoa miezi mitatu kwa wafanyabiashara na wajasiriamali wa Mkoa wa Kusini Unguja kufanya biashara zao bila kulipa kodi.

Alitoa msamaha huo akiwa kwenye ziara mkoani humo baada ya kuzindua kituo maalum cha wafanyabiashara na wajasiriamali eneo la Kitogani, Kijiji cha Mtule katika mwendelezo wa ziara zake za kutembelea na kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo nchi nzima ikiwa ni shamrashamra za mafanikio ya miaka mitatu ya uongozi wa awamu ya nane ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Pia Dk. Mwinyi, aliiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Kusini kutowatoza kodi kubwa wajasiriamali wa eneo hilo ili kuwapunguzia mzigo wa gharama za maisha na kuwapa wepesi wa kufanyabiashara zao kwa utulivu ili kukidhi haja ya biashara zao.

Pia aliitaka halmashauri hiyo kuyatunza na kuyadumisha kwa kuyakarabati majengo hayo yatakapoanza kuchakaa.

Katika hatua nyingine Rais Mwinyi aliwataka wafanyabiashara wa eneo hilo kudumisha usafi na kutenganisha biashara zao na maeneo ya barabara ili kuheshimu mipango ya miji iliyowekwa kwa kudumisha haiba ya mwonekano mzuri wa Zanzibar.

Aliitaka Halmashauri ya Wilaya ya Kusini kutengeneza vyanzo zaidi vya mapato ili kuwapa uwezo wa kuendeleza miradi ya maendeleo.

Kituo hicho cha wafanyabiashara na wajasiriamali Mtule, kiligharimu Sh. bilioni 4. 16 hadi kukamilika, kinajumuisha biashara za mbao, karakana, wachoma vyuma, gereji za magari, maduka ya bidhaa mbalimbali na wajasiriamali wa kuchora hina na piko, kina uwezo wa kuchukua wafanyabiashara 300.

Akiwa Kijiji cha Jozani wakati akiweka jiwe la msingi mradi wa ujenzi wa barabara inayounganisha vijiji vinne vya Jozani – Ukongoroni – Charawe hadi Bwejuu, Rais Mwinyi aliiagiza Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi kuwalipa fidia wananchi wote waliopisha ujenzi wa barabara hiyo.


Aliwaahidi wananchi na wakulima wa Mkoa Kusini Unguja kuwafikishia huduma za umeme mashambani ili wazalishe zaidi mboga na matunda.

Alisema, Zanzibar ina zaidi ya hoteli za utalii 600 zenye mahitaji mengi kutoka kwa wakulima wa ndani.

Alisema, hakuna haja kwa Zanzibar kuagiza matunda na mboga kutoka nje na kuliagiza Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kuwafikishia huduma ya umeme wakulima wote wa mkoa huo ili kuwapa fursa ya kutumia vyema rasilimali zilizomo kwenye vijiji vyao.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Muhammed, alipongeza uongozi wa Rais DK. Mwinyi wa kuendelea kutatua matatizo ya wananchi wa Unguja na Pemba na kueleza mafanikio yaliyopatikana ndani ya kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake yameweka alama zisizofutika kwenye historia za Wazanzibari.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Nadir Abdullatif Yussuf, alisifu hatua kubwa za maendeleo zilizotekelezwa ndani ya kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk. Mwinyi hasa kwenye miundombinu ya barabara ambapo zaidi ya kilomita 800 tayari zimetengenezwa Unguja Pemba, ujenzi wa viwanja vya ndege vya kisasa, ujenzi wa bandari jumuishi ya Mangapwani na kueleza maendeleo hayo yamepita ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020/ 2025.




Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk. Batilda Burhan (wa tatu kushoto), akipokea mfano wa hundi ya zaidi ya sh. milioni 374, kutoka kwa Mkuu wa Idara ya Kilimo Biashara wa NMB, Nsolo Mlozi (watatu kulia), kwa ajili ya fidia ya wakulima wa tumbaku walioharibiwa mazao yao na mvua kwa msimu wa 2022/2023, kwenye hafla iliyofanyika mjini Tabora jana. Wanaoshuhudia ni Meneja wa Mamlaka ya Bima kanda ya Magharibi, Dk. Lupilya Emmanuel (wa pili kushoto), Ofisa Mkuu wa Fedha wa kampuni ya Bima ya UAP, Nelson Rwihula (kulia) na (kushoto) ni Mwenyekiti wa Chama cha Msingi cha Ushirika cha Tumbaku Mtapenda, Deogratius Richard. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

### KESI MAUAJI ANETH MSUYA

# Mke wa Bilionea Msuya: Sikuwa na ugomvi wa mali na wifi yangu

**Na Grace Gurisha**

MIRIAM Mrita, aliyekuwa mke wa mfanyabiashara wa madini mkoani Arusha, Erasto Msuya 'Bilionea Msuya', amedai mahakamani kuwa hakuwahi kuwa na ugomvi wa mali na marehemu wifi yake, Aneth Msuya.

Pia amedai kuwa yeye ndiye alipeleka taarifa kwa wakwe zake kuwa Aneth amepata mchumba na kwamba yeye na mumewe ndiyo waliomlea wifi yake huyo tangu akiwa shule ya msingi hadi anaolewa na alikabidhiwa kwa ajili ya kumlea.

Mrita alidai hayo jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wakati anatoa utetezi wake dhidi ya kesi hiyo ya mauaji inayomkabili yeye na mfanyabiashara Revocatus Muyela.

Alidai kuwa Aneth alikuwa mtoto wa mwisho wa familia ya Elisaria Msuya. Muda mfupi baada ya kuolewa na Erasto, walikabidhiwa Aneth kama mtoto wao wa kumlea akiwa anasoma shule ya msingi.

Mrita alidai kuwa walimlea hadi alipofikia umri wa kuolewa, alikuwa mtoto wao aliyeishi kwenye familia yao. Aneth na Erasto ni mtu na dada yake wa damu.

Alikuwa anaongozwa na Wakili wake, Peter Kibatala, aliyemtaka aieleze mahakama kuhusiana na ushahidi wa Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Arusha, SSP David Mhanaya kwamba moja ya sababu ya mauaji ni ugomvi wa mali.

"Sijawahi kuwa na ugomvi wowote na Aneth kuhusiana na mali. Aneth baada ya kumaliza masomo yake alikuja Dar es Salaam kujiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wakati huo wote alikuwa chini ya uangalizi wetu, yaani mimi na mume wangu," alidai.

Aliendelea kudai kuwa, akiwa Dar es Salaam, Anethy alipata mchumba, wakati huo alikuwa anaishi mwenyewe, alikuja kuwafahamisha na mtu wa kwanza kumweleza ni yeye kama mama yake mlezi.

Shahidi huyo alidai alichukua jukumu la kwenda kuwaeleza wazazi Mirerani mkoani Arusha. Wazazi wakamweleza kwamba Aneth ni mtoto aliyekabidhiwa, hivyo alipaswa kuamua wapi anataka kufanyia shughuli yake.

Alidai kuwa Agosti 7, 2013 aliteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi katika Mahakama Kuu Arusha na hakuwahi kugombania mirathi na Aneth.

Pia alidai kuwa Aneth hakuwahi kufungua kesi au kudai chochote kwamba amedhulumiwa na hakuna shahidi wa upande wa mashtaka aliyewasilisha nyaraka kuthibitisha kulikuwa na ugomvi wa kugombania mirathi au mali.

"Wasimamizi kwa sasa ni Kelvin Erasto Msuya na Glory Erasto Msuya, ni watoto wetu. Kelvin ni wa kumzaa na Glory ni mtoto wa Erasto ambaye alimpata kabla ya kufunga naye ndoa, ambapo waliteuliwa Oktoba 27, 2021," alidai.

Shahidi huyo alidai kuwa alifahamu hayo baada ya Jaji Devotha Kamuzora aliyesikiliza hiyo kesi hiyo, kuagiza apelekwe kusikiliza shauri kwa njia ya video na pia zipo nyaraka zinazothibitisha uamuzi huo na waliteuliwa baada ya shauri lililofunguliwa na Ndeshukulwa Elisaria Msuya, akitaka yeye (Miriam) aondolewe kuwa msimamizi wa mirathi.

Shahidi huyo alidai kuwa usimamizi wa mali ulihamishwa kwenda kwa watoto kwa sababu yeye yuko gerezani.

Aliendelea kudai kuwa baada ya kuteuliwa kuwa msimamizi wa mali, Februari 2014 alifanya mgawanyo wa mali, ambapo aligawa fedha zilizokuwa kwenye akaunti mbalimbali za Erasto.

"Niligawa kwa baba wa marehemu na mama wa marehemu na kwa ma wifi zangu; Esther, Bahati, Joyce na Aneth Elisaria Msuya, Happy, Namtuja. Kwahiyo, hakuna siku Aneth alidai chochote baada ya mgawanyo huo," alidai.

Miriam alidai kuwa baba wa Erasto alipata Sh. milioni 225, mama alipata Sh. milioni 225, wifi zake kila mmoja walipokea Sh. milioni 73, Walipewa kwa mfumo wa benki na walitia saini mbele ya mwanasheria.

Alidai kuwa baada ya kugawa mali hizo, hakuna mahali palitokea migongano wala malalamiko yoyote kuhusu mgawanyo huo.

Kuhusiana na ushahidi wa SSP Mhanaya kuwa aliambiwa na dada wa kazi wa Aneth, Getruda kuwa mali atafute yeye wengine wafaidi, alidai kuwa kama kweli alikuwa na hisia hizo, basi asingefanya hayo aliyoyafanya. Asingegawa hizo mali.

Pia alidai kuwa katika Kampuni ya SG Northen Adventure inayohusika na SG Hotel, wanahisa ni yeye na Erasto, Erasto ana hisa 600 na yeye ana hisa 200.

Alidai kuwa katika kampuni ya Unique Mining inayojihusisha na masuala ya madini, wanahisa ni Erasto na Miriam, anakumbuka mgawanyo wa hisa, Erasto hisa 400 na yeye 100.

Alidai kuwa yeye na marehemu Erasto wana watoto watatu; Kelvin, Mourin na Calvin na kuhusu kubadili umiliki mali, hakuna nyaraka zozote zilizoletwa mahakamani kuthibitisha yeye alihamisha umiliki wa mali kutoka kwa Erasto kwenda kwake.

Miriam ambaye ni mshtakiwa wa kwanza katika kesi hiyo ya mauaji hayo ya wifi yake, Aneth, aliyeuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake Kibada, Kigamboni, Dar es Salaam, anadaiwa kukiri kuhusika na mauaji hayo katika maelezo yake ya onyo.

# Laini 34,800 zafungiwa, zimo za utapeli 'tuma kwenye namba hii'

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imezifungia laini za simu 34,848 zilizoripotiwa kupotea, kuibiwa na kuhusika katika matukio ya uhalifu katika kipindi cha Julai hadi Septemba mwaka huu.

Pia imezifungia simu 23,328 zilizobainika kuhusika na viashiria vya ulaghai katika kipindi hicho. Simu 23,234 zilifungwa na mamlaka hiyo kwa kipindi cha kuanzia Aprili hadi Juni mwaka huu.

Jana jijini Arusha, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabir Bakari, alibainisha hayo alipotoa taarifa ya mwenendo wa sekta ya mawasiliano katika kipindi cha Julai hadi Septemba mwaka huu.

Alisema kufungiwa kwa simu hizo kumetokana na elimu kwa wananchi iliyotolewa ya matumizi ya namba 15040 ya kuripoti namba za simu za uhalifu na ulaghai.

Alisema kufungiwa kwa simu hizo pia kumewezesha kupunguza matukio ya wizi na kusaidia upatikanaji vifaa vya mawasiliano vyenye ubora.

Dk. Bakari pia alisema TCRA inatoa rasilimali za mawasiliano bila malipo kwa wabunifu (Start-ups) mbalimbali wanaohitaji kufanya majaribio kwenye huduma zao kwa kipindi maalum.

Mkurugenzi huyo alitoa wito kwa vijana wajasiriamali, wabunifu na watafiti kuwasilisha wazo katika Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na wakishapitishwa, watapatiwa rasirimali hizo bila malipo.

"Tunaendelea kutoa elimu kwa umma na kuhamasisha juu ya usalama mtandaoni tukizingatia huu ni mwezi wa usalama mtandaoni. Tunaendelea na kampeni ya 'Futa Kabisa', hivyo tunawakumbusha wananchi kuepuka kusambaza taarifa zozote zisizo za uhakika na uchochezi.

"Mtu akipokea ujumbe wa kitapeli au simu ya kitapeli, atume kwenda namba 15040 na kutoamini simu ya mtoa huduma wa mawasiliano ambayo siyo 100," alisema.

Aliwataka watumiaji wa huduma za mawasiliano kuhakikisha wanapata huduma kwa mtu aliyesajiliwa na TCRA ili kuendelea kuwa salama na kupata huduma bora.

Alisema sekta ya mawasiliano ya simu nchini imeendelea kukua. Hadi mwezi uliopita, kulikuwa na laini za simu milioni 67.12 kutoka laini milioni 64.01 za mwezi Juni mwaka huu sawa na ongezeko la asilimia 4.86 zilizotimiwa na watu kwenye mitandao ya simu ya Airtel, Vodacom, Halotel, TTCL, Tigo na Smile.

Pia alisema, watumiaji wa intaneti wameendelea kuongezeka, kuliwa na ongezeko la asilimia 1.24 kutoka watumiaji 34,047,407 Juni mwaka huu hadi kufikia 34,469,022 Septemba mwaka huu.

Alibainisha sababu za ongezeko hilo la matumizi ya intaneti ni kuwapo maudhui ya Kiswahili mtandaoni na ongezeko la programu-tumizi (applications) kwa lugha ya Kiswahili.

Kwa mujibu wa Dk. Jabir, takwimu za utangazaji zinaonesha kuwa visimbuzi 3,631,649 vilikuwa hewani hadi Septemba kulinganishwa na visimbuzi 3,342,626 Juni mwaka huu. Kati yake, visimbuzi 1,789,090 ni vya dijitali kwa mfumo wa televisheni wa utangazaji wa mitambo ya ardhini na 1,842,559 ni vya mfumo wa televisheni wa satelaiti.

"Hapa Dar es Salaam inaongoza kwa kuwa na visimbuzi milioni 1.39, ikifuatwa na Arusha 287,908, Mwanza 282,779 na Mbeya 229,570, huku mkoa wenye visimbuzi vichache kuliko yote ni Manyara 1,816," alibainisha.

**UBORA WA HUDUMA**

Mkurugenzi huyo alisema TCRA imekuwa inafuatilia maudhui ya redio na televisheni kuhakikisha watoa huduma wanarusha maudhui yenye ubora yanayoendana na sheria, kanuni na miongozo ya utangazaji.

"Watoa huduma 80 walikutwa na makosa ya urushwaji wa maudhui yasiyofaa na hatua zimechukuliwa dhidi yao ikiwa ni pamoja na kupewa onyo, adhabu na maelekezo kwa mujibu wa sheria," alisema.

Aliongeza kuwa TCRA kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum imekamilisha uratibu wa programu maalum ya kuandaa vipindi vya maadili vitakavyorushwa na vituo vya utangazaji 150 vyenye leseni ya kiwilaya.



Mkuu wa Teknolojia na Operesheni wa Benki ya Standard Chartered, Christohpher Vuhahula, akipanda mti na mwanafunzi wa Shule ya Msingi Kimele ya Bagamoyo mkoani Pwani, Shabani Ramadhan, wakati wa kampeni ya kupanda miti inayoendeshwa na benki hiyo wilayani humo, juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Zao mbaazi linavyowakwamua kiuchumi wakulima

**Na Mwandishi Wetu, KARATU**

BAADHI ya wakulima wilayani karatu Mkoani Arusha wameeleza jinsi zao la mbaazi lilivyowakwamua na umaskini huku wakilishukuru Shirika la RIKOLTO kuwaondoa kwenye dhana ya kuwa ni zao la biashara pekee.

Wakiongea kwa nyakati tofauti wilayani hapa wakulima hao, Joachim Gitagno na Martha Margwe, walisema awali walifanya zao hilo kuwa la biashara, lakini baada ya shirika lisilokuwa la kiserikali la RIKOLTO kuwapa mafunzo ya matumizi mbadala kwa ajili ya chakula zao hilo limeongezeka thamani kwa kiwango kikubwa.

Walisema wamepata pia utaalamu wa mapishi na familia zinafurahia mlo wa mbaazi tofauti na awali.

"Tulikuwa hatuli sana mbaazi lakini baada ya mafunzo tumefanya mbaazi kuwa sehemu ya mlo, bei yake ni nafuu ukilinganisha na maharage, zao la mbaazi pia linastahimili ukame," alisema Gitagno.

Gitagno alisema, soko pa mbaazi limekua ikilinganishwa na miaka miwili iliyopita, mwaka 2020 kilo moja waliuza Sh. 800, lakini mwaka huu wanauza Sh. 2,200 hadi 2,400.

Matumizi ya mbaazi yameanza kutumika pia shuleni na mwalimu wa Shule ya Msingi Mbulumbulu, Benjamin Shekibuha, alisema RIKOLTO walikwenda kuwapa mafunzo ya mapishi na walipoanza kuwapikia watoto walifurahia mlo na imekuwa mbadala ya maharage.

Bwana shamba shirika la RIKOLTO alisema mbali na kutoa mafunzo matumizi mbadala ya mbaazi, wanahakikisha chakula kinazalishwa kwa gharama nafuu ili walaji waweze kumudu na hoteli zaidi ya 50, shule 100 za msingi na sekondari, mama lishe 70 na watoa huduma za chakula kwenye shughuli 200 wamepewa mafunzo na wameanza kuwa na mlo wa mbaazi kwenye menyu zao.

Lema alisema, awali waligundua kuwa maeneo mengi wanayolima mbaazi walikuwa wanalima kwa ajili ya biashara pekee, walikuwa hawatumii majumbani, lakini tangu RIKOLTO ilipoanza kutoa mafunzo ya mapishi ya zao hilo kwa wananchi, shuleni, kwa mama na baba lishe, Magereza na watoa huduma kwenye sherehe mbalimbali thamani yake imepanda kwa kiwango kikubwa.

# Mpango kuweka jiwe la msingi ujenzi kiwanda mipira ya mikono

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amedhamiria kuleta mapinduzi sekta ya viwanda hususan viwanda vya dawa na vifaa tiba.

Amesema katika hatua hiyo, Rais Dk. Samia anaendelea kutoa fedha kwa ajili ya uwekezaji sekta ya viwanda na miradi yote ya maendeleo iliyoanzishwa awamu ya tano inatekelezwa.

Waziri Ummy alisema hayo mkoani Njombe wakati wa ukaguzi wa uzalishaji wa kiwanda cha mipira ya mikono (gloves) kilichopo Idofi kinachosimamiwa na Bohari ya Dawa (MSD) ambacho kesho kinatarajia kuwekwa jiwe la misingi na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Alisema ujenzi na uzalishaji wa kiwanda cha mipira ya mikono Idofi unaridhisha na kukidhi mahitaji. Aliongeza kuwa uwekezaji wa viwanda vya dawa na vifaa tiba unaofanywa na serikali unaenda kupunguza uagizaji wa bidhaa nje ya nchi na matumizi ya fedha za kigeni.

Alisema, katika hatua ya uwekezaji wa kiwanda hicho, Rais Dk. Samia alikuta kikiwa asilimia 30 na sasa ni asilimia 90.

"Lengo la serikali ya Rais Dk. Samia ni kufikia asilimia 50 kutoka asilimia 15 iliyopo sasa katika ununuzi wa bidhaa za afya ndani ya nchi kufikia mwaka 2030," alisema.

Alisema kwa sasa vifaa vya afya kwa asilimia 85 tunanunua kutoka nje na unaponunua kuna changamoto ikiwamo kusubiri kwa miezi tisa bidhaa kufika hali inayosababisha uhaba wa dawa na kuongezeka matumizi ya fedha za kigeni. Waziri Ummy alisisitiza kwa sasa kuna viwanda 30 vya dawa na vifaa tiba vya ndani na kati ya hivyo 11 vinafanya kazi.

Alithibitisha kuwa tayari serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 11 ya uendelezaji wa kiwanda hicho na kudhamiria kuongeza uzalishaji wa viwanda vya dawa na vifaa tiba.

"Nipongeze sana bodi ya MSD hapa tunazungumzia bidhaa za afya za watu lazima kujiridhidhisha wamefanya hivyo na kiwanda kiko vizuri ambapo tutakifungua kabla ya uchaguzi wa serikali za mitaa," alisisitiza.

Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Mavere Tukai, alisema kiwanda hicho kimeanza uzalishaji wa awali na kinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu.

Alisema kiwanda hadi kitakapokamilika kitagharimu Sh. bilioni 22.5, kitakuwa na uwezo wa kuzalisha mipira ya mikono 20,000 kwa saa sawa na jozi (pairs) 10,000 na hivyo kufanya uzalishaji wa takribani jozi 86,400,000 kwa mwaka.

"Hii ni sawa na asilimia 83.4 ya makadirio ya mahitaji ya mipira ya mikono nchini ya jozi milioni 104 kwa mujibu maoteo ya uhitaji ya bidhaa za gloves nchini kwa mwaka 2023/2024," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka alisema, Rais Dk. Samia amefanya mabadiliko makubwa katika kiwanda hicho na amedhamiria kuona uzalishaji wake unakuwa na tija kwa Watanzania na hasa wananchi wa Njombe ambao wameanza kunufaika na fursa zilizopo hususani kupata kipaumbele katika ajira.

**TANGAZO**

KCBL
*Together, Transforming Lives*

# KILIMANJARO CO-OPERATIVE BANK LIMITED

## UONYESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30/09/2023
(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| A. | MALI | Robo mwaka kwa sasa 30.09.2023 | Robo mwaka iliyopita 31.06.2023 |
|---|---|---|---|
| 1 | Fedha Taslimu | 139,517 | 63,706 |
| 2 | Salio katika benki kuu ya Tanzania | 404,320 | 545,106 |
| 3 | Uwekezaji katika amana za serikali | 2,200,000 | 1,200,000 |
| 4 | Salio katika benki nyingine na Taasisi za fedha | 4,844,192 | 3,616,573 |
| 5 | Hundi na miamala ya kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala baina ya matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizofikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za wateja zilizokubalilka | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa benki nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji katika amana nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo halisi iliyopo | 7,487,018 | 7,079,175 |
| 12 | Mali nyingine | 966,055 | 680,514 |
| 13 | Uwekezaji wa hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali zisizohamishika,mitambo na vifaa | 1,934,978 | 1,919,894 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **17,976,080** | **15,104,968** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za benki nyingine na Taasisi za fedha | - | - |
| 18 | Amana za wateja | 8,905,451 | 6,405,507 |
| 19 | Dhamana ya malipo kwa fedha taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalum | - | - |
| 21 | Maagizo ya malipo /Fedha kuhamisha | 24,954 | - |
| 22 | Hundi na Hawala za kibenki zilizotolewa | - | - |
| 23 | limbiko la kodi na ghalama zitakazolipwa | 41,184 | 40,931 |
| 24 | Dhima la tozo kwaajili ya usuluhishi baina ya benki na mteja | - | - |
| 25 | Fedha za washirika(MIVARF Grant) | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya kipindi kijacho na tozo nyingine zitakazo lipwa baadaye | - | - |
| 27 | Dhima nyingine | 93,505 | 116,491 |
| 28 | Madeni | 1,000,000 | 1,000,000 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **10,065,094** | **7,562,929** |
| 30 | **MALMI /(DHIMA) HALISI(16 kutoa 29)** | **7,910,986** | **7,542,040** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa hisa uliolipwa | 16,828,410 | 16,545,451 |
| 32 | Akiba ya mtaji | 24,846 | 37,855 |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | (10,915,657) | (10,928,666) |
| 34 | Faida(hasara)ya kipindi husika | 238,596 | 152,608 |
| 35 | Akaunti nyingine za mtaji | 1,734,792 | 1,734,792 |
| 36 | Stahiki za wenye hisa chache | - | - |
| 37 | **JUIMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **7,910,986** | **7,542,040** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | 2,035,591 | 1,087,885 |
| 39 | Mikopo chechefu | 238,174 | 242,319 |
| 40 | Tengo kwa ajili ya mikopo chechefu | 73,402 | 63,957 |
| 41 | Jumla ya mikopo ghafi na amana | 7,615,919 | 7,189,266 |
| 42 | Mali nyingine chechefu | | |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa fedha za wanahisa na jumla ya mali | 44.01% | 49.93% |
| (ii) | Uwiano wa mikopo chechefu na jumla ya mikopo ghafi | 3.13% | 3.37% |
| (iii) | Uwiano wa mikopo ghafi na jumla ya amana | 85.52% | 112.24% |
| (iv) | Uwiano wa mikopo halisi na jumla ya mali halisi | 41.65% | 46.87% |
| (v) | Uwiano wa mali zinazozalisha na jumla ya mali | 42.19% | 47.39% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 39.03% | 2.37% |
| (vii) | Ongezeko la mali | 19.01% | 4.21% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO INAYOISHIA 30/09/2023
(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Robo mwaka ya sasa 30/09/2023 | Robo Mwaka iliyopita 30.09.2022 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30.09.2023 | Limbikizo la mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30.09.2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato yariba | 357,620 | 241,616 | 949,984 | 665,297 |
| 2 | Gharama za riba | 40,073 | 23,733 | 133,964 | 59,424 |
| 3 | Mapato halisi ya riba(1 kutoa 2) | **317,547** | **217,883** | **816,020.00** | **605,873** |
| 4 | Madeni viza yaliyopitwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/ongezeko la tengo katika mikopo | 9,444 | 78 | 457 | 9,160 |
| 6 | **Mapato yasiyo ya riba** | **123,966** | **110,852** | **284,963** | **253,910** |
| | 6.1 Faida/(hasara) zitokanazo na miamala ya fedha za kigeni | 10,588 | | 37,566 | |
| | 6.2 Ada na kamisheni | 26,413 | 27,369 | 75,890 | 81,475 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato mengine | 86,965 | 83,483 | 171,507 | 172,435 |
| 7 | **Gharama zisizo na riba** | **346,080** | **273,204** | **861,930** | **741,064** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 139,377 | 130,409 | 403,915 | 380,580 |
| | 7.2 Ada na kamishani | - | 1,553 | - | 2,189 |
| | 7.3 Gharama nyingine | 206,703 | 141,242 | 458,015 | 358,295 |
| 8 | **Faida/(Hasara) ya uendeshaji** | **85,989** | **55,609** | **238,596** | **127,879** |
| 9 | **Tengo la kodi ya mapato** | | | | |
| 10 | **Faida /(Hasara)Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **85,989** | **55,609** | **238,596** | **127,879** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa(bainisiha)** | | | | |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **85,989** | **55,609** | **238,596** | **127,879** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 24 | 22 | 24 | 22 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 3.10 | 1.99 | 8.59 | 4.61 |
| 15 | **Idadi ya Matawi** | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (I ) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.48% | 0.60% | 1.33% | 1.38% |
| | (ii) Uwiano wa Faida Baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 3.26% | 4.49% | 9.05% | 10.32% |
| | (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo na Riba na Mapato Ghafi | 71.86% | 77.51% | 69.79% | 80.62% |
| | (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 3.45% | 2.52% | 9.56% | 5.79% |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHA 30/09/2023

| Robo Mwaka wa sasa | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | ziada ya kisheria | Upunguzaji wa jumla wa matengo | Ziada ya mali zisizohamishika | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa Robo mwaka wa sasa** | 16,545,450 | 0 | -10,776,058 | 37,855 | 0 | 1,734,792 | 0 | 7,542,040 |
| Faida/(hasara) halisi baaada ya kodi ya mapato | | | 85,987 | | | | | 85,987 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | | | | | | | 0 |
| Miamala na wanahisa | 282,959 | | | | | | | 282,959 |
| Gawio lililolipwa | | | | | | | | 0 |
| Ziada ya kisheria | | | 13,009 | (13,009) | | | | 0 |
| Ziada ya kisheria | | | | | | | | 0 |
| Ziada ya mali zisizohamishika | | | | | | - | | |
| Mengineyo | | | | | | | | 0 |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka** | **16,828,409** | **-** | **(10,677,062)** | **24,846** | **-** | **1,734,792** | | **7,910,986** |
| **Robo ya Mwaka iliyopita** | | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka** | **16,067,148** | **-** | **(10,826,924)** | **41,504** | **-** | **1,718,417** | **-** | **7,000,146** |
| Faida/(hasara) halisi baaada ya kodi ya mapato | | | 86,776 | | | | | **86,776** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | | | | | | | **0** |
| Miamala na wanahisa | 478,302 | | | | | | | **478,302** |
| Gawio lililolipwa | | | | | | | | **0** |
| Tengo la ziada ya jumla | | | (35,910) | (3,649) | | | | **-39,559** |
| Ziada ya kisheria | | | | | | | | **0** |
| Ziada ya mali zisizohamishika | | | | | | 16,375 | | 16,375 |
| Mengineyo | | | | | | | | **0** |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka** | **16,545,450** | **-** | **(10,776,058)** | **37,855** | **-** | **1,734,792** | **-** | **7,542,040** |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30/09/2023
(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Robo mwaka kwa sasa 30.09.2023 | Robo mwaka iliyopita 31.06.2023 |
|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 85,989 | 86,776 |
| | **Marekebisho Kwa Ajili ya:** | - | - |
| | - Badiliko katika mali isiyoshikika | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | (15,084) | 8,665 |
| | - Badiliko halisi katika Mikopo | (407,843) | 282,161 |
| | - Faida/Hasara kwenye mauzo ya mali | - | - |
| | - Mabadiliko halisi katika amana | 2,499,944 | 148,439 |
| | - Mabadiliko halisi katika amana za muda mfupi zilizo afikiwa | - | - |
| | - Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | (22,986) | (36,519) |
| | - Mabadiliko halisi katika mali nyingine | (285,541) | 78,454 |
| | - Kodi iliyolipwa | 253 | (22,714) |
| | - Mengineyo(bainisha) | 24,954 | (20,407) |
| | - Maslahi ya wachache | (1) | (39,559) |
| | - Madeni na benki nyingine | | |
| | ***Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika)kwa shughuli za uendeshaji*** | **1,879,685** | **485,296** |
| II: | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | |
| | gawio lililopokelewa | - | - |
| | Ununuzi wa mali za kudumu | - | - |
| | Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - |
| | Mapato kutokana na mauzo ya amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - |
| | Mengineyo (Bainisha) | - | - |
| | ***Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji*** | - | - |
| III: | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha** | | |
| | Ulipaji wa madeni ya muda mrefu | - | - |
| | Mapato kutokana na utoaji wa madeni ya muda mrefu | - | - |
| | Mapato kutokana na utoaji wa mtaji wa hisa | 282,959 | 478,302 |
| | Gawio lilolipwa kwa fedha taslilmu | - | - |
| | Mabadiliko halisi katika madeni mengine | - | - |
| | Mengnineyo | - | - |
| | ***Fedha halisi zilizotolewa(Zilizotumika) kwa shughuli za kifedha*** | **282,959** | **478,302** |
| IV: | **Fedha taslimu na mali zinazo fanana na fedha taslimu:** | | |
| | **Ongezeko/Punguzo halisi kaitka fedha taslimu na mali** | **2,162,644** | **963,598** |
| | **Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa robo ya mwaka.** | **5,425,385** | **4,461,787** |
| | **Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa robo ya mwaka.** | **7,588,029** | **5,425,385** |

| *JINA NA CHEO* | *SAINI* | *TAREHE* |
|---|---|---|
| CPA. KINYAKI O. KINYAKI<br>**MKUU WA FEDHA NA UTAWALA** | | 25/10/2023 |
| GODFREY J. NG'URAH<br>**MENEJA MKUU** | | 25/10/2023 |
| CPA. APOLINARY S. KITYAMWI<br>**MKUU WA UKAGUZI WA NDANI** | | 25/10/2023 |

Sisi,tuliotajwa hapo chini ,wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu ,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006,na zinaonesha hali halisi.

| *JINA NA CHEO* | *SAINI* | *TAREHE* |
|---|---|---|
| 1. **Dr GERVAS M. MACHIMU, MWENYEKITI WA BODI** | | 25/10/2023 |
| 2. **CPA. MWAMINI J. MUSSA, MKURUGENZI** | | 25/10/2023 |

## MINIMUM DISLOSURES OF CHARGES AND FEES

| TRANSACTION | DESCRIPTION | 2023 VAT exclusive | 2023 VAT inclusive |
|---|---|---|---|
| **MAINTENANCE FEE: CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Normal Business Current account | Per month | 15,000 | 17,700 |
| Personal Customers | Per month | 15,000 | 17,700 |
| Umoja Account | Per month | 13,000 | 15,340 |
| Jasiri Account | Per month | 5000 | 5,900 |
| **SAVINGS ACCOUNT** | | | |
| Normal Saving Account | Per Month | 2,000 | 2,360 |
| Salary Account | Per Month | 2,000 | 2,360 |
| Msomi Account | Per Month | 1,000 | 1,180 |
| Mtoto Account | Per Month | Free | n/a |
| Mama Afrika Account | Per Month | Free | n/a |
| Mafao Account | Per Month | Free | n/a |
| Wekeza Account | Per Month | Free | n/a |
| Kilimo Tija Account | Per Month | 1,500 | 1,170 |
| **CASH WITHDRAW OVER THE COUNTER** | Per transaction | VAT exclusive | VAT inclusive |
| **UMOJA ACCOUNT** | Per transaction | 5,000 | 5,900 |
| **All savings account (Except those exempted from charges)** | 1,000 -499,999 | 5,000 | 5,900 |
| | 500,000 - 999,999 | 6,000 | 7,080 |
| | 1,000,000 -2,999,999 | 7,000 | 8,260 |
| | 3,000,000 -4,999,999 | 8,000 | 9,940 |
| | 5,000,000 & above | 0.25% | 0.295% |
| **Current Account** | Below 3,000,000 | 5000 | 5,900 |
| | 3,000,000 - 4,999,999 | 7000 | 8,260 |
| | 5,000,000 – above | 0.2% | 0.236% |
| **ATM** | **BAND** | VAT exclusive | VAT inclusive |
| KCBL and CRDB ATMs | 5,000-150,000 | 1,300 | 1,534 |
| | 155,000-400,000 | 2000 | 2,360 |
| | 405,000-600,000 | 2500 | 2,950 |
| Other Local Banks ATM's | Per Transaction | 4,000 | 4,720 |
| Other Banks ATM outside the Country | Per Transaction | 6,780 | 8,000.40 |
| Transaction Decline at ATM Outside the country due to PIN Error | Per decline | 1,000 | 1,180 |
| ATM withdrawal (Customer of other Banks) | Per transaction | 4,000 | 4,720 |

**WAKALA**

| Per Transaction | VAT exclusive | VAT inclusive | Per Transaction | VAT exclusive | VAT inclusive |
|---|---|---|---|---|---|
| <1,999 | 254.00 | 299.72 | 300,000-399,999 | 5,900 | 6,962 |
| 2,000-2,999 | 350.00 | 413 | 400,000-599,000 | 6500 | 7,670 |
| 3,000-4,999 | 400 | 472 | 600,000-999,999 | 7000 | 8,260 |
| 5,000-6,999 | 750 | 885 | 1,000,000-1,999,999 | 7500 | 8,850 |
| 7,000-19,999 | 800 | 944 | 2,000,000-2,999,999 | 8000 | 9,440 |
| 20,000-29,999 | 2650 | 1947 | 3,000,000-3,999,999 | 9000 | 10,620 |
| 30,000-49,999 | 1800 | 2,124 | 4,000,000-6,000,000 | 9900 | 11,682 |
| 50,000 -99,000 | 2550 | 3,009 | 6,000,001-7,999,999 | 11000 | 12,980 |
| 100,000-199,999 | 3,500 | 4,130 | 8,000,000-9,999,999 | 13,000 | 15,340 |
| 200,000-299,999 | 4,900 | 5,782 | 10,000,000-19,999,999 | 15,000 | 17,700 |

| TRANSACTION | DESCRIPTION | 2023 VAT exclusive | 2023 VAT inclusive |
|---|---|---|---|
| **CHEQUE BOOK** | | | |
| Cheque Book order | Per Leaf (Tzs.100 Stamp duty inclusive | 700 | 826 |
| Stop Payment Order | Per cheque | 1.0% of the amount Min. 50,000 Max 300,000 | 1.18% |
| Stop/unblock cheque leaf | Per leaf | 20,000 Max 40,000 | |
| Stop/unblock cheque book | Per cheque book | 50,000 | 59,000 |
| Encashment of third-party cheque without checklist | Per cheque | 5,000 | 5,900 |
| Unpaid cheque for reason "refer to drawer or effects not cleared | Per page | 1% min. 150,000 max 300,000 | |
| "Uncollected cheque Book (After collection notification has been sent to a customer to collect the cheque Book)" | Per cheque book per month | 6,000 | 7,080 |
| **INTERBANK** | | | |
| Inward cheques for clearance | Per cheque | 1,000 | 1,180 |
| **BANKERS CHEQUE** | | | |
| Sale of Bankers Cheque | Per leaf | 30,000 | 35,400 |
| Cancellation/Repurchase | Per leaf | 25,000 | 29,500 |
| **TRANSACTION** | **DESCRIPTION** | | |
| **BALANCE ENQUIRY** | | | |
| Over the Counter (OTC) | Per Enquiry | 1000 | 1,180 |
| At our ATM- KCBL Customer | Per Enquiry | 350 | 413 |
| Other Local Bank Customers | Per Enquiry | 1,000 | 1,180 |
| At the other banks ATMs within the country | Per Enquiry | 500 | 590 |
| At other Banks ATMs Outside the Country | Per Enquiry | 1,000 | 1,180 |
| Kili Mobile | Per Enquiry | 500 | 590 |
| At CRDB Wakala | Per Enquiry | 500 | 590 |
| **BREAKING OF ACCOUNT CONTRACTS** | | | |
| Uplifting of Fixed Deposit(FDR) | Per transaction | 50% of interest paid" | 50% of interest paid"+18% |
| Uplifting of Mama Afrika Account | Per transaction | 50% of interest paid min 10,000 | 50% of interest paid"+18% |
| Uplifting of Wekeza Account | Per transaction | 50% of interest paid" | 50% of interest paid"+18% |
| Mtoto Account Cash withdrawal exceeding 4th transaction per annum | Per transaction | 12,000 | 14,160 |
| **ACTIVATION OF DORMANT ACCOUNT** | | | |
| CURRENT ACCOUNT | Per activation | 20,000 | 23,600 |
| Savings Account except Mtoto A/c | Per activation | Free | n/a |
| Accrued Monthly/Maintenance Fee on dormant accounts with zero balance | Per activation | Free | n/a |
| **CLOSING ACCOUNT** | | | |
| Current Account | Per account | 23,000 | 27,140 |
| Savings Account | Per account | 10,000 | 11,800 |
| **FUND TRANSFER** | | | |
| Between KCBL Customers | | | |
| Over the counter | Own account | Free | n/a |
| Mobile banking | 3rd party account | 2,000 | 2,360 |
| Mobile banking | Transfer to MNOs (Mpesa, TigoPesa, Airtel Money and Halopesa) | | |
| | 5,000-10,000 | 1,500 | 1,770 |
| | 10,001-30,000 | 2,600 | 3,068 |
| | 30,001-100,000 | 3,500 | 4,130 |
| | 100,001-200,000 | 4,500 | 5,310 |
| | 200,001-500,000 | 4,600 | 5,428 |
| | 500,001-1,000,000 | 6,000 | 7,080 |
| | Per Transaction | 1% | 1.18% |
| GePG payments | Per Transaction | 1% | 1.18% |
| **INTER BANK (OUTWARD FUND TRANSFER** | | | |
| TISS | Per Transaction | 10,000 | 11,800 |
| EFT | Per Transaction | 10,000 | 11,800 |
| **INTER BANK (INWARD TRANSFER)** | | | |
| TISS | Per transaction | Free | |
| EFT | Per transaction | 4,000 | 4,720 |
| **INTERNATIONAL/FOREIGN FUNDS TRANSFER** | | | |
| Within East Africa Community Countries (TISS) | Per Transaction | 10,000 | 11,800 |
| Outward transfers to other countries | Per Transaction | Equiv. USD 50 | Equiv. USD 59 |
| Inward Foreign Funds transfer | Per Transaction | 5,000 | 5,900 |
| **KCBL VISA CARD** | | | |
| VISA card | Per card | free | |
| Annual Card fee | Per card | 15,000 | 17,700 |
| **RENEWAL OF CARD ON EXPIRY** | | | |
| VISA card | Per card | 10,000 | 11,800 |
| **REPLACEMENT OF CARD** | | | |
| VISA card | Per card | 15,000 | 17,700 |
| PIN creation | Per creation | 3,500 | 4,130 |
| **ACCOUNT STATEMENTS** | **DESCRIPTION** | | |
| Mini statement over the counter (10 transactions) | Per Statement | 3,000 | 3,540 |
| Monthly statement for current Account | Per Page | 1,500 | 1,770 |
| All statement-All Accounts | | 1,500 | 1,770 |
| **SALARY PAYMENTS** | | | |
| Manual Salary Processing | Per Entry | 3,000 | 3,540 |
| Bulk Salary Processing Automated | Per transaction | 1,500 | 1,770 |
| **CASH COUNTING/DEPOSIT OF SMALL DENOMINATIONS** | | | |
| 1,000 Notes | Above 1,000,000 | 0.2% min 2,000 | 0.236% |
| Coins | Above 100,000 | 0.2% min 2,000 | 0.236% |
| **INFORMATION SEARCH** | | | |
| For Information Up to 12 Past Months | Per Document | 50,000 | 59,000 |
| For Information of 1 to 5 Past Year | Per Document | 80,000 | 94,400 |
| For Information of Above 5 Past years | Per Document | 100,000 | 118,000 |
| CCTV image retrieve for ATM per transaction | Per Document | 100,000 | 118,000 |
| Loan Processing Fee | Personal loans | 2.1% | 2.48% |
| | Cooperatives | 2.5% | 2.95% |
| | MSME up to 100 Mn | 2.0 % min 200,000 No Max | 2.36% |
| | SME 101mn-1Bn | 2.0% Min 1,000,000 no maxi | 2.36% |
| Lending interest rates | Co-operative Union loans | 17% P.a | |
| | MSME Loans with Traditional Security | 18% P.a | |
| | MSME Loans with Non-Traditional Security | 23% P.a | |
| | Mama Afrika Loans | 14% P.a | |
| | Personal Loan | 15% P.a | |
| | Jasiri Group Loan | 48% P.a | |
| Restructuring fees | MSME | 1% | 1.18% |
| Documents and Legal Charges | Per Document | 100k@, Max 600,000 | 118K@, max 708,000 |
| Loan Take Over by Other Banks | Personal Loan, SME& Co-operatives | 3% of take Over balance | |
| Commitment fees | Unutilized Overdraft amount | 1% | 1.18% |
| **STANDING ORDER** | | | |
| Within KCBL Accounts | Per Transaction | Free | n/a |
| **INTRODUCTION LETTER AND CERTIFICATE OF BALANCE** | | | |
| Certificate of Balance | Per Item | 50,000 | 59,000 |
| Status Report | Per Report | 50,000 | 59,000 |
| Visa Recommendation | Per Item | 50,000 | 59,000 |
| Any other introduction | Per Item | 50,000 | 59,000 |
| Confirmation of customer's Bank statement requested by other banks (born by Customer) | Per Item | 50,000 | 59,000 |
| **POSTAGE AND COURIER CHARGES** | | | |
| Local Postage | Per Item | | |
| International Postage | Per Item | Equivalent USD | |
| IMPORT L/Cs | Opening- Issuance commission | 1% per quarter | 1.18% per quarter |
| | Acceptance | 0.5% PQ | 0.59% |
| | Discrepancy fee | USD 100 | USD 118 |
| | Document Processing Fee | USD 100 | USD 118 |
| Amendments | General Amendments | USD 100 | USD 118 |
| | Extension Validity | 0.25% per Month | 0.295% per month |
| **TIME DEPOSITS** | | | |
| Interest on FDR | | 3-5% | 3.54%-5.9% |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information. NB:All charges are VAT exclusive.

| | Name | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1 | CPA. Kinyaki O. Kinyaki | HEAD OF FINANCE AND ADMINISTRATION | | 25th October 2023 |
| 2 | Godfrey Ng'urah | GENERAL MANAGER | | 25th October 2023 |
| 3 | CPA. Apolinary S. Kityamwi | HEAD OF INTERNAL AUDIT AND RISK | | 25th October 2023 |
| | ***Name*** | | ***Signature*** | |
| 1. | **Dr GERVAS M. MACHIMU,** | CHAIRMAN, BOARD OF DIRECTORS | | 25th October 2023 |
| 2. | **CPA. MWAMINI J. MUSSA,** | DIRECTOR | | |





# WB yatoa bil. 20/-uboreshaji miundombinu barabara

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

BENKI ya Dunia (WB) imetoa Sh. bilioni 20.8 kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Uimarishaji Miji katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga.

Fedha hizo zitatumika katika ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 24 kwa kiwango cha lami pamoja na mitaro.

Mratibu wa mradi huo, Enne Mosses, aliyasema hayo juzi wakati akisoma taarifa juu ya utambulisho

**Maandalizi ya mradi yamekamilika, hivyo kuwaomba wadau wa maendeleo kutoa ushirikiano katika utekelezaji wa mradi huo ili utekelezwe kwa wakati.**

wa mradi huo kwa wadau wa maendeleo na kusema ujenzi huo utakuwa katika vifurushi vitatu.

"Itajengwa mitaro ya upitishaji maji pamoja na barabara ambazo zitajengwa kupitia mfuko wa Benki ya Dunia kwa kipindi cha miezi 15 ambapo kampuni yenye zabuni ya ujenzi wa miradi hiyo ni kutoka China, tayari wamesaini mkataba," alisema Moses.

Mshauri wa Mradi huo kutoka Kampuni ya Nimelta Consult, Mhandisi Emanuel Taseni, alisema wananchi wanatakiwa kuwa tayari kuupokea mradi huo ambapo barabara hizo zinatarajia kupita katika kata zaidi ya tano katika manispaa hiyo.

Meneja wa Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) Mkoa wa Shinyanga, Oscar Gilbert alisema maandalizi ya mradi yamekamilika, hivyo kuwaomba wadau wa maendeleo kutoa ushirikiano katika utekelezaji wa mradi huo ili utekelezwe kwa wakati.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Anderson Msumba, alitoa wiki moja kwa wafanyabiashara walipo pembezoni mwa barabara kupisha maeneo hayo ili kuruhusu utekelezaji wa mradi huo kuanza.

"Ninachowaomba wananchi tupishe maeneo ya kandokando ya barabara ambayo tayari yamewekwa alama ni wapi mitaro itapita na wapi barabara itapita lengo kukuza mji kwa maendeleo yetu," alisema Msumba.



Baadhi ya wanafunzi waliokuwa wakitumia bweni la wasichana katika Shule ya Sekondari ya Queen Mary of Peace inayomilikiwa na Kanisa Katoliki, mkoani Geita, wakiwa wameweka vifaa vyao nje, baada ya moto kuteketeza bweni hilo, juzi. **PICHA: SAID SINDO**

## Kamati ya fedha Msalala yaridhishwa utekelezaji miradi

**Na Mohab Dominick,** MSALALA

KAMATI ya Fedha, Uongozi na Mipango ya Halmashauri ya Msalala, Kahama imeridhishwa na usimamizi katika utekelezaji wa miradi, pamoja na kasi ya maendeleo ndani ya halmashauri hiyo.

Wajumbe wa kamati hiyo walieleza hayo jana katika kikao cha Baraza la Madiwani kilichoketi kupitia taarifa ya utekelezaji wa robo ya kwanza kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Pamoja na mambo mengine walimpongeza Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Khamis Katimba kwa kusimamia na kutekeleza miradi husika ndani ya muda.

Diwani wa Kata ya Segese, Joseph Manyara, alisema kuwa kama madiwani waliweka malengo katika kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa wakati lakini katika usimamizi wa mkurugenzi huyo imekamilika kabla ya muda.

Naye Diwani wa Kata ya Ikinda, Matrida Msoma, alisema kuwa licha ya miradi kufanikiwa kwa wakati vilevile waliweka kiwango cha makusanyo ya fedha katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/24.

Akisoma taarifa ya fedha kwenye kikao hicho, Mweka Hazina wa Halmashauri hiyo, Gordon Dinda alisema, katika robo hii, shughuli nyingi za maendeleo zimefanyika ikiwamo ujenzi wa Shule ya Msingi Kabale yenye madarasa 12, maktaba na matundu ya vyoo 10.

Dinda alisema serikali ilitoa fedha kupitia mradi wa boost ambapo Sh. milioni 561 zilitumika, huku wananchi wakitumia nguvu zao katika ukusanyaji wa mawe na mchanga.

## Bweni shule ya wasichana lateketea kwa moto

**Na Said Sindo,** GEITA

BWENI la wasichana katika Shule ya Sekondari Queen Mary of Peace mkoani Geita limeungua moto huku wanafunzi watano wakikimbizwa hospitalini kutokana na mshtuko wa tukio hilo.

Bweni hilo linalomilikiwa na Kanisa Katoliki Geita limeungua na kusababisha uharibifu wa jengo hilo, pamoja na hasara ya vifaa vya wanafunzi ikiwa ni pamoja na vitanda na magodoro.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya tukio hilo, Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Geita, Mrakibu wa Zimamoto (SF), Shaban Dawa, alisema chanzo cha moto huo bado hakijabainika na jeshi hilo linaendelea na uchunguzi dhidi yake.

Aidha, alieleza kuwa jeshi hilo lilifanikiwa kuuzima moto huo huku wanafunzi watano wakikimbizwa hospitali kutokana na mshtuko walioupata kutokana na taharuki.

Alitaja madhara yaliyotokea kufuatia moto huo kuwa ni pamoja na kusababisha hasara ya kuteketea kwa vitanda, magororo, vifaa binafsi vya wanafunzi pamoja na uharibifu wa jengo lakini hakuna kifo wala majeruhi mahututi.

## Walipwa fidia uharibifu mvua mawe

**Na Mwandishi Wetu,** TABORA

WAKULIMA wa tumbaku zaidi ya 400 mkoani Tabora wamelipwa fidia kutokana na hasara waliyopata baada ya mashamba yao kuharibiwa na mvua kubwa ya mawe iliyonyesha Januari na Mei mwaka huu.

Hundi ya malipo ya madai hayo ya Sh. milioni 374 kutoka kampuni ya bima ya UAP Insurance ilikabidhiwa jana kwa Mkuu wa Mkoa huo, Balozi Dk. Batilda Buriani aliyesema kuwa fidia hizo ni kubwa kuwahi kulipwa wakulima wengi nchini kwa wakati mmoja.

Kiongozi huyo alisema wakulima waliokata bima kwa ajili ya mashamba yao dhidi ya majanga walifanya uamuzi sahihi kwa kuwa bima hizo zimekuwa mkombozi wao na sasa wataweza kuendelea na shughuli zao wakiwa na uhakika wa maisha.

Dk. Buriani aliwashukuru UAP na Benki ya NMB kwa kuchukua hatua za haraka kuhakikisha wakulima hao wanalipwa madai yao kwa wakati huku akisema hilo linaendana na azma ya serikali kuwaunga mkono wakulima na kuchangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini.

Mkuu wa Idara ya Kilimo Biashara wa benki hiyo, Nsolo Mlozi, alisema wanaunga mkono juhudi za serikali kuhakikisha kilimo nchini kinakuwa na tija na kuwanufaisha wakulima.

Alisema benki yao na serikali ni wadau wakubwa wa maendeleo na kutatua changamoto zinazowakabili wakulima na wananchi wote kwa ujumla.

Mlozi alisema benki yao inathamini umuhimu wa kilimo cha kisasa na mchango wa zao la tumbaku katika ujenzi wa taifa ndiyo maana ina ushirika na wadau mbalimbali ili kuwasaidia wakulima na sekta ya kilimo.

Alisema baada ya wakulima hao kufikwa na madhila hayo, benki hiyo na kampuni ya UAP walifanya upembuzi stahiki na tathmini ya kina kuona ni fidia kiasi gani inastahili kwa uharibifu wa mashamba husika.

Mwakilishi wa UAP, Mariam Hussein, aliwaambia walioshiriki katika makabidhiano hayo kuwa lengo la kushirikiana na NMB ni kuhakikisha kuwa huduma za bima zinachangia kikamilifu kuendeleza kilimo na kuleta maendeleo ya uchumi nchini.

ama
ALHAMISI OKTOBA 26, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

## BAADA YA MADHARA...
## Kahama na operesheni ya marufuku tiba kichaa cha mbwa kwa waganga



## Darasa kwa wachimbaji wadogo sumu zebaki, wazinduka balaa!

Ukurasa 12

SEKTA MAJI NA 'KAZI IENDELEE'. . .

# Vita vya Awamu Sita kulipa deni la umma majisafi na salama kwa wote

**Na Mwandishi Wetu**

INAPOTAJWA maji ni neno la kisekta, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika miaka miwili na nusu ya uongozi wake, amewekeza kwa umakini, anafuatilia kwa hatua, hadi akianika 'upolisi' wake katika utendaji wa waziri mwenye dhamana.

Alhamisi iliyopita, gazeti hili lilikuwa na makala Dk. Samia, akizindua mradi wa maji mkoani Singida, kutoka Ziwa Victoria. Vilevile, sehemu ya mradi huo maji yaliyopelekwa mkoani Shinyanga, Januari mwaka huu, uzinduzi ulifanywa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Tarehe 17 mwezi uliopita, akiwa mkoani Mtwara, Rais Dk. Samia akawahakishia wananchi, serikali inaendelea na jitihada kuhakikisha wote mkoani wanafikiwa na huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza.

Rais amekuwa akishiriki kuzindua na kukagua mradi ya maji kitaifa na katika kauli yake Mtwara, katika wilaya Newala ilitoka alipopata maelezo ya Mradi wa Maji wa Makonde, kutoka kwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri.

Ni hatua ambayo Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, naye amekuwa akizichukua, zikiwamo za kinidhamu dhidi ya hujuma kwa sekta hiyo.

Hotuba yake ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2022/23, nako akagusa kuhusu maji, akizingatia mambo kadhaaa; Mpango na Bajeti ya Sekta Mwaka 2022/23; Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (2020 - 2025); Sheria, Kanuni, maoni na ushauri kuhusu utekelezaji huo.




Rais Samia Suluhu Hassan, akiondoa kitambaa kuzindua Mradi wa Maji wa Mlandizi- Chalinze – Mboga, mkoani Pwani, Machi 22 mwaka jana. **PICHA: MAKTABA.**

Katika hotuba yake ya makadirio ya mapato na matumizi, bungeni, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, anasema hadi sasa rasilimali maji ambazo Rais Dk. Samia anawekeza nguvu ziko mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka.

Aweso anasema, zimegawanyika katika; maji juu ya ardhi mita za ujazo bilioni 105 na zilizopo ardhini, mita za ujazo bilioni 21.

Anasema, hadi kufika Aprili mwaka jana, mahitaji ya maji nchini yanakadiriwa kuwa mita za ujazo bilioni 47 kwa mwaka, sawa na asilimia 37.37 ya maji yaliyopo.

Hata hivyo, anataja mwenendo hadi kufika mwaka 2035, mahitaji yanatarajiwa kuongezeka kufika mita za ujazo bilioni 80 kwa mwaka.

Pia, anataja wastani kila mtu nchini anatumia kiwango, kwa makadirio ya awali kabla ya Sensa ya Watu na Makazi 2023, ilikuwa wastani mita za ujazo 2,250, kwa mujibu wa makadirio ya watu milioni 55.9 wa mwaka 2019.

Waziri Aweso, anataja kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa ni mita za ujazo 1,700. Chini ya hapo, inahesabika kuwa uhaba wa maji. Hivyo, nchini hakuna uhaba wa maji.

Hivyo anasema, kiasi cha maji kilichopo nchini kinaonyesha hakuna uhaba wa maji, huku serikali ikiendelea kuwekeza katika utunzaji vyanzo vyake, ujenzi miundombinu ikijengwa kuongeza upatikanaji wa maji; kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuboresha ufanisi wa matumizi yake.

**UBORA WAKE**

Katika mikakati ya utendaji wake, Rais Dk. Samia, pia amekuwa akizama kwenye suala la usalama wa maji na vyanzo vyake.

Kwa mujibu wa Waziri Aweso, wizara kupitia maabara 17 za ubora wa maji nchini, inahakiki na kufuatilia ubora wa katika vyanzo na mitandao ya kusambaza maji mijini na vijijini, ili kutoa uamuzi sahihi wa matumizi yaliyokusudiwa.

Sura ya matokeo, Waziri Aweso anasema maji yanayosambazwa kupitia mifumo iliyopo mijini na vijijini, yanakidhi viwango kitaifa katika maeneo mengi nchini, inagawa anakiri changamoto za kuwapo madini ya chumvi katika mikoa kama; Pwani, Dodoma na Singida.

Pia, anataja kuwapo madini ya Fluoride katika ukanda unaopitiwa na Bonde la Ufa; ikiwamo mikoa ya Arusha, Manyara, Mara, Kilimanjaro, Shinyanga, Singida na Simiyu.

Inaendelea Uk. 14

AFYA

# Darasa kwa wachimbaji wadogo sumu zebaki, wazinduka balaa!

## • Inaharibu nguvu kiume na mimba, mtindio ubongo…

**Na Pilly Kigome, aliyekuwa Geita**

SEKTA ya madini inaonekana kukua kwa kasi kubwa nchini Tanzania. Ni shughuli zinazofanyika katika mikoa 14 Tanzania Bara na kutoa ajira za moja kwa moja kwa takribani watu milioni 1.5, huku ajira zisizo za moja kwa moja kwa zaidi ya watu milioni saba.

Tathimini ya hali ilivyo kwa sasa, inaonyesha kuwa wachimbaji wadogo wa dhahabu hutumia kiasi cha tani 13.2 hadi 24.4 ya madini ya mekyuri au zebaki kwa mwaka.

Hata hivyo, matumizi yatakuwa yasiyo salama katika kuchenjua dhahabu, ikisababisha athari kwa afya za binadamu na mazingira kwa ujumla.

Hivi karibuni mkoani Geita, katika Maonyesho ya Sita ya Kimataifa ya Teknolojia ya Madini, Baraza la Taifa Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limekemea vikali matumizi ya madini hayo zebaki kwa wachimbaji wadogo.

Ilikuwa katika semina elekezi ya kuachana na matumizi hayo, kwani yana madhara makubwa kwa afya za binadamu na uharibifu wa mazingira.

Ni mnamo Septemba 21 mwaka huu, Mratibu wa Mradi wa Kudhibiti Matumizi ya Mekyuri kwa Wachimbaji Wadogo (EHPMP), Mhandisi Dk. Befrina Igulu, akasema athari zinazotokana na kutumia zebaki wakati wa kukamatisha mchanga wenye dhahabu, wakati wakichoma magumu yenye mchanganyiko wa zebaki na dhahabu.

Inatajwa, matumizi yake katika shughuli za uchenjuaji dhahabu husababisha uchafuzi wa vyanzo vya maji, hewa na udongo na kusababisha madhara makubwa kwa binadamu, ikiwamo kuathirika kwa mfumo wa fahamu wa mtumiaji na figo kuharibika.



Shughuli za uchenjuaji madini ya dhahabu zikendelea kwa wachimbaji wadogo, matumizi ya zebaki yakikemewa hatari kiafya. **PICHA: MAKTABA.**

Mengine anayataja kuwa ni hali ya kuchanganyikiwa, kupoteza kumbukumbu, msongo wa mawazo, kupoteza uwezo wa macho kuona, mikono kutetema, kuhisi maruweruwe, kurithisha athari za zebaki kwa watoto.

Ni athari za zebaki anazozitaja kujumuisha pia kupungua nguvu za kiume, kuharibu mimba, watoto kuzaliwa na utindio wa ubongo, yote yanatokana na matumizi ya zebaki.

**UCHAFUZI MAZINGIRA**

Mtaalamu Dk. Igulu anaeleza, kuna madhara ya afya za kibinadamu ya mazingira kutoka kwenye uchenjuaji dhahabu, yanayosababisha uchafuzi wa mazingira, ikiwamo uchafuzi wa vyanzo vya maji hewa na udongo.

Anabainisha kwamba wapo katika mikakati ya kuondokana kabisa na matumizi hayo na kubainisha kuwa matumizi ya zebaki, ifikapo kikomo 2025.

Mkuu wa Wilaya ya Geita, Cornel Maghembe, akifungua mafunzo kwa wachimbaji wadogo, anayataja kwamba yatawasaidia wachimbaji kiafya na kimazingira, akifafanua:

"Mafunzo hayo yamekuja kwa wakati mwafaka, kwa kuzingatia, kwa kuwa na ongezeko la wachimbaji wadogo nchini, linakwenda sambamba na uharibifu wa mazingira."

Mkurugenzi wa Tathimini ya Athari ya Jamii kutoka NEMC, Lilian Mkambuzi, akimwakilisha Mkurugenzi Mkuu NEMC anasema kupitia mradi huo, wataweza kupitia sheria na kanuni zilizopo, kwa kuziboresha wakiingiza vipengele vitakavyowezesha usimamizi thabiti wa uingizaji, utunzaji, utumiaji zebaki, pamoja na utekelezaji wa kanuni husika.

Mwenyekiti wa Wachimbaji Madini Wanawake, Asia Masimba, anaiambia Nipashe kwamba wapo katika mikakati ya kuachana na matumizi ya zebaki, kwani wanakiri matumizi yana madhara makubwa kwa upande wao.

Ananena: "Ni mabaya kiafya, kwani tumeshaona madhara, kwani watu wanaathirika kwa kiwango kikubwa na tunatumia tu kwa ajili ya shida."

NEMC imeshaainisha mikakati na njia za kupunguza athari zitokanazo na matumizi ya zebaki katika shughuli za uchenjuaji dhahabu, ikiwamo ukamatishaji na uchomaji dhahabu, unaopaswa ufanyike kwenye maeneo maalum yaliyotengwa kufanyia kazi hizo, wakifuata miongozo na taratibu zilizowekwa.

Maono yaliyopo ni kwamba, shughuli za ukamatishaji na uchomaji dhahabu, inapaswa kufanyika mbali na vyanzo vya maji, pia makazi ya watu.

Vilevile inatajwa kwamba mabaki yake yasitupwe kwenye vyanzo vya maji au meneno ya mafuriko.

Hiyo inaendana na kuchoma mabaki ya zebaki na dhahabu yanayopaswa kufanyika ikiwa na mfumo mahsusi wa kutupa mabaki ya zebaki iliyotumika, kuacha watu na mazingira katika namna salama.

Mitazamo yote hiyo ikitekelezwa vilivyo, inatajwa kujenga dira kwamba madhara ya zabaki yanayotajwa na wataalamu, yatabaki historia kote.

# NGO yaingia ubia na serikali, kukabili janga maradhi ya akili

**Na Sabato Kasika**

MATUKIO ya kuua au kujiua, yakihusisha wivu wa kimapenzi yamekuwa yakiripotiwa nchini, huku kukiwapo maswali kwa kinachoendelea nyuma ya pazia.

Katika orodha ya vyanzo kunatajwa afya ya akili ina nafasi katika kuchochea ukatili huo, unaogeuka mjadala mitaani, pia mitandao ya jamii.

Shirika lisilo la kiserikali la Akili Platform Tanzania (APT), inayoshugulika na uelimishaji, kusaidia, kutetea na kuboresha afya ya akili, mazingira na haki za binadamu nchini, limebuni kampeni iitwayo 'Kuishi ni Mali'.

Mkurugenzi wa APT, Roghat Robert, anasema kampeni ilizinduliwa Julai mwaka huu katika ofisi zake mjini Tabora na wanajipanga kuzunguka kitaifa kuanzia Januari ijayo.

Ni hatua inayolenga kuhusisha kukomboa fikra kwa kila familia, waratibu wa magonjwa ya akili mkoa na wilaya, polisi, wataalamu wa kazi za mikono, hasa Shirika la Maendeleo la Viwanda Vidogo (SIDO), vyuo vya ufundi, walimu wa wenye mahitaji maalum, wazee wa mitaa, viongozi wa dini na viongozi wa serikali.

Robert anasema, wanalenga kuunganisha familia zenye watoto wenye ulemavu wa akili kila mkoa, wazazi na walezi wakipewa mafunzo ya malezi na makuzi.

Hapo inajumuisha kuandaa lishe, ulinzi na usalama, michezo muhimu, kazi za nyumbani na mikono kwa kaulimbiu "nisaidia nifanye mwenyewe."

Mkurugenzi huyo anawataja walengwa ni wenye umri chini ya 18, wenye ulemavu, wakikusudia kutoa elimu ya tiba na saikolojia kifamilia.

Mtaalamu huyo anasema, mauaji au watu kujiua kunachangiwa na afya ya akili, hivyo wanajitoa kuelimisha, jamii ibadilike.

"Mikoa ambayo itakuwa ya kwanza kupata elimu yetu ni Tabora, Dodoma, Njombe, Iringa na Dar es Salaam, kwani inatajwa kuwa na matukio mengi ya watu kuua au kujiua," anasema.

**HALI ILIVYO**

Waziri Ummy Mwalimu, anataja Tanzania inakadiriwa kuwa watu milioni saba wenye magonjwa ya akili, huku Shirika la Afya Duniani (WHO) likijulisha mwaka 2021 kulikuwapo waathirika wa magonjwa ya akili duniani milioni 970. Hapo anataja magonjwa ya sonona yenye watu milioni, 280 na magonjwa ya akili kwa watoto na vijana, watu milioni 301.

Kwa mujibu wa waziri, wanawake ndio waathirika zaidi kuliko wanaume, wako asilimia 52.4. Mtaalamu Saikolojia kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Isaac Lema, anataja wastani mtu mzima mmoja kati ya wanne, anapitia shida afya ya akili; pia, mmoja kati ya watano kazini ana shida hiyo.

Aidha, anasema asilimia 10 ya wafanyakazi wanahangaikia na sonona; wastani wa siku 36 za kazi zikipotea kutokana na sonona kwa mujibu wa Ripoti ya WHO ya mwaka 2017.

Vilevile, anataja sababu za tatizo la afya ya akili ni mtu kushindwa kukabiliana na changamoto za maisha, vinasaba alivyo navyo, magonjwa kama Ukimwi na malaria kali.

Pia, kunatajwa msongo wa mawazo kiwango cha juu, shinikizo la makundi rika na matukio yenye tishio kama vile majanga, ukatili, unyanyasaji na migogoro.

Taarifa ya WHO ya mwaka 2019, inasema kila baada ya sekunde 40 kuna mtu anajiua duniani, Afrika ikiongoza.

AFYA

## BAADA YA MADHARA KUKITHIRI…

# Kahama na operesheni ya marufuku tiba kichaa cha mbwa kwa waganga




Mtaalamu na Mkaguzi wa Mbwa kutoka Shirika lisilo la Kiserikali la Kutetea Haki na Ustawi wa Wanyama Tanzania (TAPO), Master George, akitoa elimu ya kichaa cha mbwa na dalili zake kwa vijana waliopeleka mbwa kupata chanjo ya kujikinga na maradhi hayo. **PICHA; SHABAN NJIA.**

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MARADHI kichaa cha mbwa kitaalamu yanatajwa hayana tiba, hivyo kinga ndio usalama pekee unaomlinda aliyeng'atwa na mbwa au paka.

Ni ugonjwa huo unaosababishwa na virusi viitwavyo kitaalamu kama "Rabies Virus" na vinapatikana katika mate au damu ya binadamu na wanyama wengine kama vile mbwa, Mbweha, paka pamoja na popo.

Maambukizi hayo hupita katika mfumo wa fahamu, yaani ubongo na hadi mgongo, vikimsababishia mgonjwa kupooza, kushindwa kula na kupoteza fahamu au hata kifo, isipochukuliwa hatua stahiki.

Uwapo wa hatari hiyo, ndio unaifanya serikali kuwa na utaratibu wa kutoa chanjo kwa Wanyama, ili usiendelee kuenea. Madhara yake yanatajwa husambaa kwa madhara kuchukua nafasi ndani ya siku 10 za maambukizi.

Ni hatari inayotajwa kwa watoto, huku uhalisia wao ndio wako karibu zaidi na wanyama wafugwao, hasa wanapoumwa au kugusa mate yao.

Tiba yake mpaka sasa inataja haijapatikana kama ilivyo kwa magonjwa mengine ya virusi, lakini kuna chanjo zinazotolewa ama kabla au baada ya maambukizi, ikizuia kusambaa.

**KINACHOENDELEA WILAYANI**

Katika kujihami, baadhi ya wananchi wilayani Kahama mkoa Shinyanga, wamekuwa na utaratibu wao kujihami kwenda kwa waganga wa jadi kupata matibabu ya kiasili, baada ya kung'atwa na mbwa anayesadikiwa kuwa na kichaa.

Imani yao ni kwamba wamelogwa, hata kuwafanya baadhi yao wanapoteza maisha kwa maradhi ya kichaa cha mbwa.

Kwa kuona ukubwa wa tatizo hilo, shirika lisilo la kiserikali la Kutetea Haki na Ustawi wa Wanyama Tanzania (TAPO), kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, wameamua kutoa chanjo bure kwa wanyama wafugwao; mbwa 6,000 na paka 200.

Damiani Kilyenyi, ni Ofisa Mifugo wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, anasema, elimu ya kujikinga na kichaa cha mbwa haiwajafikia vema wanajamii, hususan wanaoishi pembezoni mwa mji na vijijini.

Anataja tabia iliyotawala sasa kuna watu wanapong'atwa na mbwa wanakimbilia kwa waganga wa jadi kutibiwa kiasili, badala ya hospitalini kupata chanjo, hata kuchangia wengi kupoteza maisha.

Hapo anataja sababu ya kifo wanakuwa wamekaa muda mrefu bila ya chanjo ya kinga inayotolewa hospitalini, wakidumu katika imani mbwa aliyemg'ata sio wa kawaida.

Kilyenyi anatoa mfano wa kata za Isagehe, Zongomela na Nyandekwa, ambako waliong'atwa na mbwa wamekimbilia kwa waganga wa kienyeji na wanaposhtuka kuwahi hospitalini, inakuwa wamechelewa matibabu.

"Tuwaombe waganga wa jadi kuacha tabia ya kuingilia fani za watu na badala yake wanapopata mgonjwa wa namna hii wamshauri kufika hospitalini haraka na sio kukaa naye tu pasipo matibabu," anasema Dk. Kilyenyi.

Ofisa Mifugo wa Kata ya Bulige katika Halmashauri ya Msalala, Dk.David Sospiter, ana simulizi ya kuwapo watoto wawili waliong'atwa na mbwa, kisha wazazi wao wakawakimbiza kwa mganga wa jadi wakiamini mbwa alikuwa ametumwa na hakuwa wa kawaida, baada ya wiki moja walipoteza maisha.

Anasema, tukio hilo limemfanya kuanzisha mikutano vijijini kutoa elimu ya umuhimu wa kichaa cha mbwa na madhara yake na kutoa njia sahihi ya kupata chanjo, wakiachana na kukimbilia kwa waganga wa jadi kutibiwa.

**MRATIBU CHANJO**

Mkola Vedasto, Mratibu Chanjo wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, anakiri kupokea wagonjwa wa kichaa cha mbwa hospitalini kupata chanjo wakiwa katika hatua za mwisho, hali inayochangia baadhi kupoteza maisha na wanapowahojiwa ndugu, wanadai walianza kumpeleka kwa mganga wa kienyeji.

Anasimulia mkasa wa mtoto aliyeng'atwa na mbwa wa jirani na alipomueleza baba yake, alizuiliwa kutoa taarifa kwa mtu mwingine, kwa lengo la kulinda uhusiano na siku ya tatu alimueleza mama yake na wote hawakujali.

Vedasto anasema, baada ya siku saba mtoto alianza kuwa na hali ya tofauti na walilazimika kumfikia hospitalini kwa ajili ya kupata chanjo, lakini walikuwa wameshachelewa na mtoto alipoteza maisha.

Vedasto anasema, kwa siku wanapokea wagonjwa wastani watatu hadi watano, wakiwamo wanaokatisha dozi. Anataja dozi huwa tano na ya mtoto mwenye kilo 12 au chini ya hapo, ni Sh. 90,000 na mtu mzima Sh. 165,000.

**UTOAJI WA CHANJO**

Ofisa Mifugo Kilyenyi, anasema kwa kushirikiana na shirika la TAPO, wanatoa chanjo bure kwa wafugaji mbwa na paka, ili kujikinga na kichaa. Wanatarajia kutoa chanjo hiyo kwa mbwa 6,000 na paka 200 katika kata zote 20 za Kahama, huku faini kwa asiyechanja anatozwa faini ya Sh.20,000.

Anasema, chanjo wamekuwa wakifanya bure kila mwaka kabla ya kilele cha Maadhimisho ya Kichaa cha Mbwa Dunia, mwaka ikiwa na kaulmbiu" Afya kwa Wote."

Kilyenyi anataja dalili za mbwa mwenye kichaa, huwa mkali sana au mpole kuzidi, akiuma chochote anachokiona mbele yake, anauma watu ovyo hata asipochokozwa, kubweka na ana mate mengi, anaogopa maji na mwanga, anashindwa kula na kunywa, anadhohofika, kupooza na hatimaye kufa.

Mtalaamu wa TAPO, Master George, anasema huduma ya kwanza kwa aliyeg'atwa na mbwa, pasipo kujali ana kichaa au la, anatakiwa kuosha jeraha kwa maji na sabuni kupunguza wepesi wa maambukizi kushambaa mwilini.

Pia, anafafanua anayeng'atwa na mbwa mguuni atachelewa kupata madhara kutokana umbali wa mguu hadi kichwani, kulinganisha na anayeg'atwa mkononi, hivyo anawataka wanaog'atwa kutokupuuza chanjo, inayowanusuru maisha yao.

**SIMULIZI YA MASHUHUDA**

Saraha Shija, mkazi kata ya Malungu, Kahama anaeleza alivyog'atwa mguuni na paka wake aliyekuwa na chanjo, mguu ukavimba na kuanza kuuma, akapuuza kwenda hospitalini, ila akabahatika kupona, ila sasa amejiandaa kisakolojia, asipuuze hali kama hiyo tena.

Pia, mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Kishimba, Juma Simon anasema, alichojifunza ni umuhimu wa kuchanja mbwa wasiambukize kichaa cha mbwa na kuwataka vijana wenzake wanaofuga wanyama, kutokaa nao ndani, kwani ni hatari anapowang'ata na kukosa tiba.

Mratibu wa Shirikisho la Waganga wa Tiba za Asili Kanda ya Magharibi (SHIVYATIATI) Athumani Waziri, anakemea waganga wa jadi wanaotoa huduma kwa waliog'atwa na mbwa, akitaka atakayebainika, serikali imuwajibishe kisheria.

Anasema, kila anapoitisha vikao vyake huwa anawasisitiza suala la kutotoa huduma katika magonjwa ambayo yanahitaji mgonjwa kufika hospitalini.

AFYA

## SURA YA PILI NA 'KAZI IENDELEE'…

# Miaka 30 ya TGNP; kuanzia kutetea afya jinsia, ubia na Rais 'kumtua mama ndoo'

**Na Christina Haule, Morogoro**

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP) umefanikisha kupungua matukio hatarishi, ikiwamo shida za ndoa na mimba za utotoni, nyumba kuchomwa moto na adhabu shuleni katika kijiji cha Tomondo, Tarafa ya Mikese wilayani Morogoro.

Hiyo ni katika kuelekea miaka 30 ya huduma zake, ikiibua changamoto zinazowakuta wanawake nchini, huku kukitarajiwa Tamasha la 15 la Jinsia, litakalofanyika Dar es Salaam, tarehe 7 hadi 10 mwezi ujao.

Mwenyekiti wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Kijiji cha Tomondo, Morogoro, Mwanahawa Salehe, anasema kupitia TGNP, kuna matukio hatarishi yaliyokithiri mwaka 2019 hadi 2020, ikiwamo adhabu shuleni, kati ya mwaka 2021 na 2022 ndoa za utotoni zimepungua.

Anaeleza kujivunia TGNP, kutimiza miaka 30 elimu waliyoipata na mafunzo kama vile yaliyowafanya wanawake kujitambua katika kugombea nafasi za uongozi, kugundua kushiriki, ushirikishwaji na kushirikiana kwenye kampeni zilizowasaidia kutoyanyasika katika ndoa na kuwa wajasiri kupambania haki zao, wakifichua uhalifu.

Salehe anasema, changamoto zilizotatuliwa baada ya kupata elimu, sasa zimezaa matunda ya kuongezeka madarasa katika Shule ya Msingi Vuleni na kila kijiji kuingiziwa umeme na maji.



Mmoja wa wawezeshaji katika mafunzo kwa wanawake yaliyofanywa na TGNP katika Halmashauri ya Wilaya Morogoro. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

Anataja kuwapo changamoto zisizopatiwa ufumbuzi, ikiwamo kero ya mifugo kuvamia mazao ya wakulima zinazohitaji ufumbuzi wa haraka.

Kuhusu mafanikio ya TGNP kwa jamii, Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi wa Nguvu ya Pamoja na Harakati, Florah Ndaba, anasema wanajivunia mafanikio kwa baadhi ya waanzilishi wa vuguvugu za sheria mbalimbali zinazochangia zingine kurekebishwa nchini, pia kampeni kushika hatamu kuingia kwenye ajenda za kiserikali.

Anasema, mabadiliko ya sheria yalifanyiwa marekebisho na nyingine zimeundwa, zikibeba masuala ya kijinsia, zikiwa na uhai hata pasipo kuwapo TGNP.

Ndaba anasema, TGNP imefanikisha kusambaza bajeti yenye mrengo wa kijinsia, ambao mpaka sasa serikali imeona umuhimu wake katika sekta kama za maji, afya na elimu.

"Tunaona serikali imeanza kutenga bajeti zenye mrengo wa kijinsia na tunajivunia kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa serikali, tunaamini kuwapatia mafunzo juu ya bajeti ya mrengo wa kijinsia kutazidi kuzaa matunda zaidi kwa jamii," anasema Ndaba.

Anafafanua hatua ya serikali kuitikia wito wao, imesaidia huduma muhimu za matibabu kuwafikia wananchi, hasa waliopo vijijini, kwa kuboreshewa vituo vya afya na kujengewa zahanati, pia hospitali na vifaa vyake.

Ndaba anasema, TGNP ni mwanzilishi wa kampeni 'Mtue Mama Ndoo Kichwani' inayoendelea kutekelezwa ikiungwa mkono na Rais Samia Suluhu Hassan na Wizara ya Maji ikiongozwa na Waziri Jumaa Aweso, mikoa imenufaika na kampeni.

Anasema kampeni iliungwa mkono na taasisi, mashirika na kampuni za uchimbaji visima, kutengeneza matangi ya kuhifadhia maji na usambazaji mabomba, ili kuisaidia jamii kupata maji ya uhakika kwa urahisi.

"Kampeni hiyo imeweza kumsaidia mwanamke kupunguza muda na umbali wa kutafuta maji hivyo nguvu imeelekezwa kwa kuinua uchumi wa mwanamke, badala ya kuwa bize kutafuta maji…" anasema.

Pia Ndaba anataja mafanikio mengine, ni vuguvugu la kubadilisha Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 iliyokuwa na changamoto hasa kwenye umri sahihi wa mtoto wa kike kuolewa kuanzia miaka 14, akisema inapigiwa kelele na wadau, kupunguza ndoa za utotoni.

"Ingawa wapo baadhi ya watu wanaopigania na mabadiliko ya sheria ya likizo ya uzazi kwa wanaojifungua, ni kitu ambacho hakikuwapo lakini leo hii kinamama wanafaidika…" anaongeza.

Zingine, anazitaja ni mafanikio ya kampeni ya rasilimali kuwanufaishe wananchi, wakiwamo wanawake kukabidhiwa hati miliki za nyumba na ardhi.

Hata anakumbusha, TGNP hawakuendesha kampeni peke yake, bali na wadau wengine.

**CHANGAMOTO**

Ndaba anataja changamoto zilizopo ni ya kuwapo sheria zisizotekelezwa, kwani kazi kubwa imefanyika katika marekebisho ya sheria, lakini hawazioni kutekelezwa.

Pia analakamikia mila na desturi zinazoendelea kushikiliwa na baadhi ya makabila na kurudisha nyuma maendeleo ya jinsia.

Kingine analalamikia ajenda muhimu za mageuzi kijinsia, zinabebwa na wachache badala ya wengi, haya kuleta ugumu katika mageuzi ya haraka.

Ndaba, pia anataja changamoto ya ukuaji sayansi na teknolojia, upande wa pili inaacha nyayo za shida kijinsia, elimu hadi inawafikia watoto na kuangukia pabaya.

Kwenye ukatili wa kijinsia, Ndaba anasema changamoto hiyo anataja uelewa duni wa jamii ukisababisha kuongezeka matukio ya ukatili, ingawa kuna kasi ya vuguvugu la kuibua changamoto ikiwa na msaada wa kupunguza kasi hiyo.

Msaada uliopo anautaja serikali kujenga madarasa, mabweni na madawati kwa kutengeneza mikakati ya kupambana na ukatili kitaifa.

Hapo anaipongeza TGNP kupitia vuguvugu hilo, inaibua changamoto katika jamii na kuzifanyia kazi.

# VITA VYA AWAMU SITA KULIPA DENI LA UMMA MAJISAFI NA SALAMA KWA WOTE

**Inatoka Uk. 11**

Hatua zinazochukuliwa anazitaja ni kushirikiana na wadau kimataifai, serikali ikiwekeza katika teknolojia za kusafisha na kutibu maji, ikiweka mitambo ya kisasa kupunguza madini chumvi katika maji ya kunywa.

**MAJI VIJIJINI NA MIJINI**

Kwa mujibu wa Waziri wa Maji, upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi vijijini, inatarajiwa kufika zaidi ya asilimia 85 ifikapo mwaka 2025, serikali ikijenga, kukarabati na kupanua mitandao ya kusambaza maji, huku ikiimarisha usimamizi wake.

Itakumbukwa, alipokuwa akizundua Mradi wa Maji Chalinze mkoani Pwani, Rais Dk. Sama, akatoa karipio dhibi ya uchepushaji wa vyanzo vya maji, sambamba na wanaonywesha mifugo kwenye vyanzo.

Pia, inatajwa, hadi Aprili mwaka jana, upatikanaji huduma ya maji vijijini ulifika wastani asilimia 74.5 ikilinganishwa na asilimia 72.3 za Machi, 2021, msimu Rais Dk. Samia anaingia madarakani.

Waziri Aweso kwenye hotuba yake bungeni Agosti mwaka huu, akaahidi kukamilika ujenzi wa miradi mipya, ukarabati na upanuzi wa miradi 303, kukitarajiwa kunufaisha wananchi zaidi 1,467,107.

Anasema, hadi Aprili mwaka jana, upatikanaji maji mijini ilikuwa wastani asilimia 86.5 ya mahitaji halisi, kulinganishwa na asilimia 86 ya Machi 2021, ikiwa ni zao la kukamilika miradi 40 iliyohusisha ukarabati na upanuzi wake.

**KAZI INAVYOENDELEA**

Taarifa ya Bunge ya Wizara Maji, inaonyesha mikakati ya Rais Dk. Samia na miradi mipya ya maji iliyokuwa ikizinduliwa Januari mwaka huu ikigusa; kuboresha huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Arusha.

Pia, miradi ya maji; Mugango-Kiabakari- Butiama; kupeleka maji Miji ya Tinde – Shelui; Maji Kigamboni; Bunda; Chalinze; Kyaka-Bunazi; Namanga; Bagamoyo; na miradi 218 inayotekelezwa kwa fedha za Mpango wa Maendeleo wa UVIKO.

Hadi Aprili 2022, kunatajwa kuwapo vituo 178 vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji vilivyojengwa na baadhi kukarabatiwa, kutolewa vibali vipya 451 vya matumizi ya maji; vibali 649 vya kuchimba visima vya maji na kuweka mipaka vyanzo vya maji 48 kama hatua ya awali.

Pia, serikali imekamilisha mradi wa kuboresha huduma ya maji Mlandizi – Chalinze – Mboga kwa gharama ya Shilingi bilioni 18, nao ulizinduliwa na Rais.

Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, inaendelea kukarabati na kupanua mfumo wa usambazaji majisafi kutoka tanki la Chuo Kikuu Ardhi, Dar es Salaam, kwenda Bagamoyo

Vilevile, Aweso anasema, serikali inashirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA) na Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (Saudi Fund for Development – SFD), kutekeleza Mradi wa Maji wa Mugango, Kiabakari na Butiama, uliofika asilimia 54 kuifika katikati ya mwaka huu.

Mingine ni miradi ya maji katika maziwa makuu, Victoria, Tanganyika na Nyasa, kupeleka maji katika mikoa ya; Mwanza, Geita, Simiyu, Kagera, Mara, Katavi, Kigoma na Rukwa, Ruvuma na Njombe.

Mingine inayoendelea ni; kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira Arusha; Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Kigoma; Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Lindi; Kuboresha Huduma Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Morogoro; maji kutoka Mto Kiwira, Tukuyu hadi jijini Mbeya; Kuboresha Huduma ya Majisafi jijini Tanga; Dareda- Singu-Sigino-Bagara; majisafi Kyaka – Bunazi; Mradi wa Maji Same – Mwanga – Korogwe; na Mradi wa Kukabilianana Athari za Mabadiliko ya Tabianchi mkoani Simiyu.

Pia, kuna miradi inayotekelezwa kwa fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya Uviko

Kuhusu usafi na majitaka, Aweso anasema hadi mwezi Aprili mwaka jana, uwezo wa uondoshaji majitaka ulikuwa asilimia 13.5, lengo ni kufikia asilimia 30 mwaka 2025.

Waziri anahitimisha kwa kutaja changamotoz za sekta ya Maji, ikiwamo kwenye miundombinu; ufuatiliaji kodi, idadi ya watalaamu, mabadiliko ya tabianchi, pia fursa ya kutekeleza miradi ya maji kwa kutumia vyanzo vya maji vya uhakika kama vile mito mikubwa.





# Migogoro ya ardhi 774 yatatuliwa, hati 1,474 zatolewa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imefanikiwa kutatua migogoro 774 ya ardhi kwa wakazi wa Jiji hilo, huku ikitoa hati 1,474 kwa wananchi kupitia kliniki ya ardhi iliyofanyika hivi karibuni.

Kliniki hiyo ilifanyika Oktoba 16 hadi 20 mwaka huu ikilenga kutatua migogoro ya ardhi kwa haraka.

Mkurugenzi wa Jiji hilo, John Kayombo aliyasema hayo jana alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa kliniki ya ardhi kwa wananchi wenye mashamba na viwanja ndani ya Jiji la Dodoma.

Kayombo alisema kliniki hiyo imepangwa kuwa endelevu na moja ya hatua zilizofanyika ni pamoja na utoaji wa hatimiliki kwa haraka, kusikiliza kero za ardhi na kuzitafutia ufumbuzi.

Alisema zoezi hili ni sehemu ya hatua za utekelezaji wa mkakati wa Mkoa wa Dodoma wa kumaliza changamoto za ardhi zinazowakabili wananchi.

Alisema kliniki hiyo imetoa matokeo chanya ambapo wananchi 3,056 walisikilizwa, huku wakipokea maombi ya hati kutoka kwa jamii inayohitaji huduma huyo.

Hata hivyo, aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa serikali pale wanapohitajika kushiriki kwenye kliniki hizo ili waweze kutatuliwa kero ambazo zinawakabili kwenye masuala ya umiliki wa ardhi.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wengine, Josephine Sawia alisema kliniki hizo zinasaidia kutatua kero kwa wananchi ambao hawana uwelewa kuhusu umiliki wa ardhi.

Josephine alisema hatua ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma kubuni kuendesha kliniki ya ardhi imefanya vizuri kwa sababu kuna uwepo wa changamoto za ardhi kwa wananchi na kusababisha migogoro.

Alisema: "Tunaomba zoezi hili liwe endelevu, litasaidia kuondoa changamoto mbalimbali ikiwamo migogoro kwa wananchi," alisema Sawia.

Kadhalika, aliipongeza serikali kutokana na kusimamia masuala ya ardhi akisema itasaidia kupunguza migogoro inayotokea mara kwa mara kwa wamiliki wa ardhi katika maeneo mbalimbali.

# Viongozi CHADEMA watakiwa kufuta fikra za kugombea

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

**CHADEMA kwa sasa kimejielekeza katika lengo moja tu na kwamba hakitaingia kwenye uchaguzi wowote mpaka ipatikane Katiba Mpya na marekebisho yafanyike katika Tume ya Uchaguzi.**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Singida kimewataka viongozi kuondoa fikra za kuwaza kugombea nafasi za uongozi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajia kufanyika mwakani pamoja na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

Badala yake wameshauriwa kujielekeza katika kudai Katiba Mpya na Tume Huru ya Uchaguzi.

Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Singida, Jingu Jackson, alisema hayo jana wakati akifungua kikao cha mashauriano chenye lengo la kuangalia uhai wa chama ambacho kimewashirikisha wenyeviti na makatibu wa wilaya, majimbo na mabaraza kinachofanyika mjini Singida.

Alisema CHADEMA kwa sasa kimejielekeza katika lengo moja tu na kwamba hakitaingia kwenye uchaguzi wowote mpaka ipatikane Katiba Mpya na marekebisho yafanyike katika Tume ya Uchaguzi.

"Kiongozi wa CHADEMA aondoe mawazo maana kuna watu wapo ndani ya chama wanawaza mwaka 2024 nitagombea nafasi gani na mwaka 2025 nagombea ubunge, udiwani na urais kwa ajili ya kupata posho, sasa hivi chama kinataka tujielekeze katika utendaji kazi kufa na kupona kwa ajili ya kudai Katiba Mpya ambayo ndio suluhisho la wananchi wote wa Tanzania ukiwamo Mkoa wa Singida," alisema.

Jackson alisema na uamuzi huo mkali na mgumu wa chama wapo baadhi ya watu watahama chama lakini lazima watambue kuwa kinachofanywa na chama ni kuweka rekodi na heshima ya kizazi kijacho.

Aidha, akisema wapo watu ambao walikuwa wagombea mwaka 2020 na wengine watiania, hivi sasa wakati chama kinapambana na mipango ya kudai Katiba Mpya na Tume Huru ya Uchaguzi wamekipa kisogo chama kana kwamba hakuna kitakachoendelea hapo baadaye.

Naye Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA, Mkoa wa Singida (BAWACHA), Josephine Msweti, alisema zoezi la kuandikisha kadi mpya za uanachama za kielektroniki ambalo limefanywa na BAWACHA limefikia asilimia 73.

Msweti aliwapongeza wanawake wa CHADEMA kwa kuwa mstari wa mbele katika suala hilo na kuwataka kutokata tamaa ili zoezi hilo lifikie kwa asilimia 100 na Mkoa wa Singida uwe kinara kwa utekelezaji wa kazi hiyo.

Mwenyekiti wa Baraza la Wazee Mkoa wa Singida, William Kidanka, alisema mkoa huu bado haujaonyesha uhai mzuri kwa chama kutokana na baadhi ya viongozi kutokuwa makini katika utekelezaji wa majukumu yao ipasavyo.

Alisema: "Singida mnamwangusha Lissu (Tundu Lissu) ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA kunapotokea mikutano nje ya mkoa huu mnashindwa hata kuwagharamia viongozi kwenda huko, tambueni matendo ya uongozi wa chama ni uwajibikaji".



Baadhi ya watu wenye ulemavu wa vichwa vikubwa na mgongo wazi, wakimsikiliza Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (hayupo pichani), wakati wa maadhimisho ya Siku ya Watoto Wenye Vichwa Vikubwa na Mgongo Wazi Duniani, yaliyofanyika kitaifa jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wanafunzi Buigiri hatarini kuugua magonjwa ya mlipuko

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

WANAFUNZI wenye ulemavu wa macho katika Shule ya Msingi Buigiri wilayani Chamwino mkoani Dodoma afya zao zipo hatarini kupata magonjwa ya mlipuko, kutokana na vyoo vya shule hiyo kutokuwa safi.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Samwel Jonathan, alibainisha hayo juzi shuleni hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kero wanazokabiliana nazo wanafunzi wenye ulemavu katika shule hiyo.

Alisema wanafunzi katika shule hiyo wamekuwa wakikabiliwa na kero mbalimbali ikiwamo ya vyoo kufulika kutokana na miundombinu inayotumika kuwa chakavu.

"Watoto wanakabiliwa na changamoto nyingi hapa lakini hii ya vyoo kufulika imekuwa kero kubwa sana hapa kwani mara kwa mara vyoo vinajaa na kulazimika kukodi magari kwa ajili ya kuondosha majitaka." Alisema.

Hivyo, aliwaomba wadau pamoja na serikali kuwasaidia wapate miundombinu mipya ya vyoo ili kuondokana na shida hiyo ambayo imekuwa kero kwao kwa muda mrefu.

Alisema pamoja na vyoo kujaa lakini pia bado wanakabiliwa na shida ya maji katika shule hiyo hali ambayo inaongeza mzigo wa matatizo kwa watoto hao wenye ulemavu katika mabweni yao.

Kadhalika, alisema kero nyingine ni shule kukosa uzio hali ambayo inatishia usalama wa watoto hao haswa wale wenye ualbino ambao ni sehemu ya wanafunzi wanaosoma hapo.

Alisema: "Hapa tunao pia watoto wenye ualbino ambao wanasoma hapa, hivyo kukosekana kwa uzio ni kero kwao kutokana na mwingiliano wa watu wengine kutoka nje ya shule hali ambayo inatishia usalama wao, hivyo tunawaomba wadau pamoja na serikali kutusaidia kupata uzio kwa ajili ya eneo hili la shule".





# Wagoma kufungua milango kukwamisha utoaji chanjo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wakazi wa Mtaa wa Iwambi jijini Mbeya wanadaiwa kukwamisha utoaji wa chanjo kwa watoto kwa kugoma kufungua mageti ya nyumba zao ili kuruhusu watoa huduma kutoa chanjo hiyo.

Malalamiko hayo yalitolewa na watoa chanjo ya polio kwenye kikao cha Kamati ya Afya ya Wilaya ya Mbeya wakati wa maandalizi ya awamu ya pili ya utoaji wa chanjo hiyo, ambayo itatolewa kwa siku tatu kuanzia Novemba 2, mwaka huu.

Mratibu wa chanjo wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Zuhura Mohamed alisema katika utoaji chanjo ya polio awamu ya kwanza lililofanyika Septemba mwaka huu walipata changamoto ya baadhi ya wakazi wa Mtaa wa Iwambi kugoma kufungua mageti ya nyumba zao jambo ambalo lilisababisha zoezi hilo lisifanyike kwa ufanisi.

**Wilaya ilitoa chanjo ya polio kwa asilimia 120 na kushika nafasi ya kwanza kimkoa ingawa anatambua kuwa vilikuwepo vikwazo wakati wa utekelezaji wa chanjo hiyo.**

"Tulipata changamoto katika Mtaa wa Lwambi kutokana na baadhi ya watu kukataa kufungua mageti ya nyumba zao, hali hiyo ilinilazimu mimi mwenyewe kwenda Iwambi kushughulikia changamoto hiyo ambapo katika baadhi ya nyumba tulifanikiwa kuingia lakini nyumba nyingine tulishindwa na hivyo kusababisha baadhi ya watoto wasichanjwe," alisema Zuhura.

Alisema kuwa ili kukabiliana na changamoto hiyo ni muhimu elimu na hamasa itolewe kwa kiwango kikubwa kwenye jamii kwa lengo la kuwaelewesha umuhimu wa chanjo na athari zinazoweza kuwapata watoto ambao hawatapata chanjo hiyo.

Akizungumzia changamoto hiyo, Meya wa Jiji la Mbeya, DorMohamed Issa alisema ili kuondokana na changamoto za aina hiyo ni muhimu wenyeviti wa mitaa wakashirikishwa wakati wa zoezi la chanjo.

Alisema katika maeneo ambayo changamoto hiyo ilijitokeza wenyeviti wa mitaa hawakushirikishwa, hivyo wananchi waliingiwa na hofu kuhusu chanjo hiyo na kusababisha wagome kufungua mageti ya nyumba zao ili kuruhusu watoto wao kuchanjwa.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Benno Malisa alisema katika utoaji wa chanjo ya polio awamu ya kwanza Wilaya ya Mbeya iliongoza Mkoa wa Mbeya kwa kuvuka lengo walilojiwekea la kuwapatia watoto chanjo ya polio.

Alisema kuwa wilaya yake ilitoa chanjo ya polio kwa asilimia 120 na kushika nafasi ya kwanza kimkoa ingawa anatambua kuwa vilikuwepo vikwazo wakati wa utekelezaji wa chanjo hiyo.

Malisa alitoa wito kwa wadau wa chanjo ndani ya wilaya kutumia mbinu zile zile zilizotumika wakati wa la awamu ya kwanza kuhakikisha wanafanya vizuri kwa mara nyingine na kuongoza kimkoa.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiteta jambo na Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, katika kongamano la pili la Chama cha Madereva wa Serikali Tanzania, mjini Morogoro juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wanafunzi wataja chanzo ufaulu mbovu shule ya wazazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari ya Wazazi Meta ya jijini Mbeya wamesema uchakavu wa majengo na miundombinu shuleni hapo ndiyo chanzo cha matokeo mabovu wanayoyapata kwenye mitihani ya kitaifa.

Shule hiyo inayomilikiwa na Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ilijengwa miaka ya 1980 na tangu wakati huo haijawahi kufanyiwa ukarabati hali ambayo imesababisha kuwepo kwa uchakavu wa miundombinu ya shule hiyo.

Wakizungumza wakati wa mahafari ya 37 ya kidato cha nne katika shule hiyo, baadhi ya wanafunzi wameomba wamiliki wa shule hiyo kuifanyia ukarabati mkubwa ili kufanya iwe na mazingira mazuri ya kujifunzia.

Mmoja wa wanafunzi aitwaye Magreth Mlonje alisema kero kubwa iliyokuwa ikiwakabili shuleni hapo ni ubovu wa miundombinu ya shule hasa uchakavu wa madarasa, vyumba vya maabara na ukosefu wa vifaa vya kufanyia majaribio.

Alisema, pamoja na uchakavu wa miundombinu ya shule hiyo pia wanakabiliwa na tatizo la uhaba wa vitabu vya kiada na ziada hali ambayo inafanya suala la kujisomea kuwa gumu kwao.

"Miundombinu ya shule yetu imechakaa kiasi kwamba inaweza hata kuhatarisha maisha ya wanafunzi, pia kuna uhaba wa vitabu na vifaa vya maabara kwa ajili ya kufanya majaribio ya kisayansi, mambo haya yanafanya suala la kujisomea kuwa gumu na hivyo tunashindwa kupata matokeo mazuri kwenye mitihani yetu," alisema Magreth.

# Ummy: Serikali kuongeza uzalishaji dawa, vifaa tiba

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema serikali imedhamiria kuongeza uzalishaji wa ndani wa dawa na vifaa tiba pamoja na bidhaa zingine za afya, ili kuondokana na adha ya kuagiza bidhaa hizo nje ya nchi.

Alitoa kauli hiyo wakati wa ziara ya kutembelea na kukagua kiwanda cha kutengeneza mipira ya mikono (Gloves) kilichopo Idofi Halmashauri ya Mji Makambako Mkoani Njombe.

"Sasa hivi asilimia 85 ya bidhaa za afya ikiwemo dawa, gloves, vitendanishi na vifaa vingine tunanunua kutoka nje ya nchi, kwahiyo unaponunua nje ya nchi kunakuwa na changamoto ya kuchelewa kufika kwa bidhaa, tunatumia fedha za kigeni kuagiza bidhaa za afya na tunachukua bidhaa duni kutoka baadhi ya maeneo" alisema Ummy.

Waziri Ummy alisema lengo la serikali ni kufikia asilimia 50 ya bidhaa zote za afya ziwe zinanunuliwa ndani ya nchi kupitia Bohari ya Dawa (MSD).



Alisema, Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea kutoa fedha ili kutekeleza miradi yote ya maendeleo ya wananchi husussani katika sekta ya afya ambayo ilianzishwa katika Serikali ya Awamu ya Tano.

Aidha, alisema mpaka sasa zaidi ya Sh. bilioni 11 zimetumika kwenye kuendeleza ujenzi wa kiwanda hicho cha mipira ya mikono ambacho mpaka sasa kimefikia asilimia tisini.

Mkurugenzi Mkuu wa Bohari ya Dawa (MSD), Mavere Tukai, alisema kiwanda hicho cha dawa kimeshaanza kuzalisha ila kinachosubiriwa ni TMDA kutoa ithibati ili bidhaa iweze kuingia sokoni.

Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Bunge Afya na Ukimwi, Stanslaus Nyongo, alisema uwekezaji mkubwa ambao Rais Samia Suluhu Hassan anaufanya ni kuwekeza kwenye afya ya binadamu.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka alisema kwakuwa serikali inatumia kiasi kikubwa cha fedha kuagiza mipira ya kiume kutoka nje basi kupitia kiwanda hicho kitakuwa kinatengeneza ili kupunguza uagizaji kutoka nje ya nchi.

Alisema: "Zaidi ya Sh. bilioni 10 za kitanzania zinatumia katika kuagiza mipira ya kiume nje ya nchi, kwahiyo tukasema tutumie nafasi ya uwepo wa kiwanda hiki kutengeneza mipira ya kiume ya kwetu ili tupunguze kuagiza nje ya nchi".





# ZRA yatoa hofu wananchi kodi majengo

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

KAMISHNA Mkuu wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRA), Yussuph Juma Mwenda, amesema kodi ya majengo haitolipwa kwa wananchi wote, bali ni kwa wale wenye uwezo.

Alisema wanaopaswa kulipa kodi hiyo ni wamiliki wa majengo ya biashara, majengo ya ghorofa ya makazi na majengo ya hoteli.

Mwenda aliyasema hayo wakati akizungumza na viongozi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, pamoja na masheha wakati wa kutoa ufafanuzi juu ya kodi ya majengo Zanzibar.

**Kodi hiyo haitokuwa na athari kwa wananchi wa chini, hivyo ni vyema kwa masheha kuwaelimisha wananchi wao.**

Alisema kuwa kodi ya majengo haimuhusu mwananchi wa kipato cha chini na badala yake wanaopaswa kulipa kodi hiyo ni wale wenye uwezo.

"Kodi hii siyo ya watu wote bali ni wale wenye majengo ya ghorofa, majengo ya biashara hawa uwezo wao ni mkubwa na wanachangia tu, wale waliojenga na nyumba zao kupangisha au ameweka duka atachangia kodi ya jengo," alisema.

Aidha, alisema kuwa kodi hiyo inapaswa kulipwa na mmiliki wa jengo husika na siyo mpangaji wa nyumba na kuwataka masheha kuelewa kuwa kodi hiyo haitohusu sehemu zote za majengo ya serikali au nyumba za ibada isipokuwa zile za biashara.

Pia aliwataka masheha hao kila wanapofanya manunuzi ni vyema kudai risiti za kielektroniki ili mapato ya nchi yapatikane.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib, aliwataka masheha kushirikiana na ZRA katika kuhakikisha inatekeleza vizuri majukumu katika maeneo yao.

Aliwataka masheha hao kutambua kuwa kodi ya nyumba ipo zamani lakini serikali ilikuwa haijaweka msisitizo juu ya kodi hiyo.

Hata hivyo, aliutaka uongozi wa ZRA kuchukua hatua za makusudi kutoa elimu kwa wananchi ili kufahamu kodi hiyo na hivi sasa kodi hiyo imeshaleta sintofahamu kwa wananchi, huku baadhi yao wakihusisha na mambo ya kisiasa.

Naye Mkurugenzi wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRA) Pemba, Jamal Hassan Jamal, alisema kodi hiyo haitokuwa na athari kwa wananchi wa chini, hivyo ni vyema kwa masheha kuwaelimisha wananchi wao.

## Serikali kuendelea kuwapa haki za msingi makundi maalum

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Chakechake, Abdalla Rashid Ali, amesema, Serikali ya Zanzibar itaendelea kuunga mkono juhudi za kuwapa haki watu wenye ulemavu.

Aliyasema hayo wakati akifungua kongamano la wadau kwa watu wenye ulemavu Kisiwani Pemba.

Alisema hilo ni kundi pekee linalopaswa kupewa kipaumbele katika mambo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Rashidi alisema watu wenye ulemavu wanapata changamoto kwenye jamii, hivyo ipo haja ya kushirikiana pamoja katika kuhakikisha wanapata haki zao na fursa sawa.

Aidha, alisema kupitia fedha za Uviko- 19 serikali imejenga vituo maalumu kwa watu wenye ulemavu Unguja na Pemba, ili wapate elimu bora itakayowasaidia katika maisha yao ya kila siku.

Ofisa Mdhamini Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Ahmed Abubakar Mohamed, alisema wanachukua juhudi za makusudi ili kuhamasisha na kuhakikisha jamii inaelimika juu ya upatikanaji wa haki kwa watu wenye ulemavu.

Alisema kuwa Baraza la Watu wenye Ulemavu tayari limefanikiwa baadhi ya mambo ikiwamo la kuwekwa mitihani maalumu kwa watu hao kulingana na hali ya ulemavu waliyonayo.

Naye Ofisa Utetezi Haki za Binadamu kutoka Taasisi ya Makuzi na Malezi Bora ya Watoto wadogo (MECP-Z), Nassir Rashid Ali, aliwataka wadau kuwashajihisha wazazi kuwaandikisha watoto wao shule ili wapate haki yao ya elimu.

Mwalimu wa Elimu Mjumuisho, Omar Bakar Shomari, aliwataka wazazi kufuatilia mwenendo na maendeleo ya watoto wao shuleni ili kufanikisha lengo lilokusudiwa.




Ofisa Utumishi na Utawala wa Shirika la Uchumi na Maendeleo la Jiji la Dar es Salaam, Cyprian Mbuya (katikati), akizungumza wakati akifungua jumuiko la kimaitafa la siku tatu la mabibi wanaolea wajukuu ambao wazazi wao wamekufa kwa UKIMWI liitwalo 'International Grandmothers Gathering', Msimbazi jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mwenyekiti wa Jumuiko hilo, Pfiriael Kiwia na Mwanachama wa Shirika la Kimara Peers Educator, Hamza Milambo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Serikali yaendelea kutekeleza ajenda ya uchumi wa buluu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema inaendelea na utekelezaji wa mafanikio katika ajenda ya uchumi wa buluu, kwa lengo la kukuza pato la taifa.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, wakati akifungua warsha ya mapitio ya mfumo wa uthamini wa taarifa za uchumi wa buluu pamoja na uanzishaji wa bango la kidijitali.

Alisema kama ilivyoelekezwa katika miongozo ya Rais Dk. Hussein Mwinyi na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya Mwaka 2050, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar, Sera ya Uchumi wa Buluu na Sera na Mipango inayohusiana na utekelezaji wa ajenda hiyo ya uchumi wa buluu.

Alisema kupitia Sera na Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Buluu, utekelezaji huo umegawika katika vipaumbele vikuu vitano ambayo ni sekta ya utalii, uvuvi na mazao ya baharini, sekta ya usafiri wa baharini, sekta ya nishati ikiwamo mafuta na gesi na katika usimamizi endelevu wa matumizi na hifadhi za bahari.

Alisema vipaumbele hivyo vinahitaji mfumo bora na wa kisasa na ulio sahihi unaotoa hali halisi, mwelekeo na maeneo ya kuboresha katika utekelezaji wa mikakati ya uchumi wa buluu.

Aidha, alisema Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, katika utekelezaji wa majukumu yake, inahitaji mikakati kabambe na iliyoborа ya takwimu na taarifa sahihi na mfumo bora wa ufuatiliaji na utoaji taarifa.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, alisema mfumo huo una umuhimu kwa serikali ambao utasaidia kufanyika utafiti na utoaji wa taarifa sahihi za maendeleo ya utekelezaji wa mikakati ya uchumi wa buluu, kwa kupata takwimu za rasilimali za kiuchumi, kijamii na kimazingira katika utekelezaji wa sera na mkakati wa wizara hiyo.


Alisema kwa sasa asilimia 39.6 Pato la Taifa la Zanzibar linatokana na uchumi wa buluu, asilimia 25.4 ya ajira kufikia mwaka 2020 na thamani ya huduma za serikali za bahari tayari zinafikia Dola za Marekani bilioni 100.76

Mwakilishi kutoka Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Ambrose Mugisha na Mratibu wa Programu za Uchumi wa Buluu katika shirika hilo alisema tangu Serikali ya Zanzibar kuanzisha Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi mataifa mbalimbali yanafika kujifunza jambo hilo.

Alisema taasisi yake imekuwa mstari wa mbele katika kuiunga mkono Zanzibar katika shughuli za maendeleo ikiwamo ya kuona namna gani wananchi wake wananufaika na mafunzo wanayotoa ya kuwajengea uwezo wakulima wa mazao ya baharini.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI




**IBRAHIM GEORGE ARENDE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0661/0053** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ISSENYE SEKONDARI** mwaka 2020. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/30364/2023.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**PIMA MICHAEL SAMSON** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha sita yenye index namba S.0133/658 iliyotolewa na **MINAKI SEKONDARI** mwaka 2023. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/PWA/KIS/2590/2023.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**ANDREW CHARLES SEGELE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.26390075 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia SHULE YA SEKONDAR KINAMBELI mwaka 2020. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: KIO/B.I/27/332/202**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**
**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NAMBA 107 YA MWAKA 2023**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**

**AL-KARIM HUSSEIN JAFFER**
**KAMAL KASSAMALI KHIMJI........................MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 16 mwezi 11, 2023 saa 10:00 asubuhi.
Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 19 mwezi wa 10, 2023

HIGH COURT OF TANZANIA
NAIBU MSAJILI

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**
**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NA 108 YA MWAKA 2023.**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU JOSEPH GABRIEL MSHANA**

**JOYCE GABRIEL NYABUNDEGE.....................1. MWOMBAJI**

**MARRY ZAKAYO TANDARI..........................2.MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 10 mwezi 11, 2023 saa 10:00 asubuhi. Siku ambayo imepangwa kusikilizwa mbele ya Mh. Jaji Asina A. Omari.
Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 24 mwezi wa 10, 2023

HIGH COURT OF TANZANIA
NAIBU MSAJILI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DISMAS MATHIAS KISOKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 207 DKZ – VOLKSWAGON.** Chassis namba **WVGZZZ7L50015473.** Engine namba **AXGJ3002999.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/MTW/MTW/938/2023.**

## KUPOTELEWA NA MATOKEO

**Ndugu DOLOSELA ENERICO** MULISA anatangaza kupotelewa na matokeo ya mwisho ya kumaliza masomo ya shahada ya kwanza (transcript) yaliyotolewa na chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP) Dodoma mwaka 2015/2018 yenye namba IRDP/BDR/15/3229.
Kwa yeyote atakayeyaona atoe taarifa kituo cha polisi au apige **simu namba 0765721227.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EDSON YOHEL LIJOLA**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA TOWNACE RANGI YA BLUU YENYE USAJILI T988CWN ENGINE NO: 5K1080504,CHASISI NO:KM510033528.YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI JALADA NAMBA
**PHQ/IRI/IRI/2486/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIAKATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**

**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......57/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: ABDALLAH SABABU ABDALLAH WA DAR ES SALAAM**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA JUMA SABABU ABDALLAH**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 27 Mwezi 10 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia.

Imetolewa leo tarehe 20 mwezi 10 mwaka 2023

Imetolewa leo tarehe 20 Mwezi 10 Mwaka 2023
HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU**
**DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA MADAI NO. 164 YA MWAKA 2023**

**INSURANCE GROUP OF TANZANIA LTD .......................MDAI**

**SAMWEL FRANCIS NA WENZAKE 2...................... MDAIWA**

**KWA**
1. **SAMWEL FRANCIS**
2. **KASIAN FLUGENS DIMOSO**
3. **COMMERCIAL MOTORS TANZANIA LTD**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya mdai yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo mnahitajiwa kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au kwa wakili au mwakilishi ambaye anaruhusiwa, siku ya tarehe 26-10-2023 saa 7:00 mchana.
**ANGALIA**
Kama hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama mmepokea kuitwa shaurini, itaweza kutoa hukumu kuwa mmeshindwa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 16 Mwezi wa 10/2023

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE

**HARVESTER CAPITAL INVESTMENT LTD**

## NOTISI/TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**HARVESTER CAPITAL INVESTMENT** kwa idhini tuliyopewa na **SME IMPACT FUNDY TANZANIA LIMITED** tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo baada ya siku kumu na nne (14) kuanzia tarehe ya Notisi/ Tangazo hili endapo hatalipa deni lake.

| NA | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA NA MAHALIILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1 | SAMWELI DAUDI SHILYA . | NYUMBA IPO MKOA WA GEITA USHIROMBO MWALO .. | 10 /11/2023 . |

**MASHARTI YA MNADA**
1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/ dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindi wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyopungua 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/ eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

**HARVESTER CAPITAL INVESTMENT**
**P.o.Box 11898, ARUSHA**
**Tel: 0784 200283/ 0767529605**
**Email: harvestercapital558@gmail.com**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



Wakazi wakiwaangalia wafanyakazi wa huduma ya dharura wakiondoa vifusi kwa ajili ya kutafuta majeruhi baada ya Israel kushambulia Mtaa wa Khan Younis katika Ukanda wa Gaza jana. **PICHA: REUTERS**

# Guterres atibua hali ya hewa, baada ya kuikosoa Israel

**NEWYORK, Marekani**

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres, ametoa wito wa kusitishwa mapigano mara moja ukanda wa Gaza na ameliambia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuwa mashambulizi dhidi ya Gaza yanakiuka sheria ya kimataifa.

Katika matamshi aliyoyatoa kwa wajumbe wa baraza hilo juzi, Guterres alikosoa ukiukwaji wa wazi wa sheria ya kimataifa unaoshuhudiwa Gaza kwa Wapalestina waliokaliwa kimabavu kwa miongo kadhaa.

Aliongeza kwamba ni muhimu kutambua mashambulizi yaliyofanywa na Hamas hayakufanyika bila kuwa na sababu.

Balozi wa Israel katika Umoja wa Mataifa, Gilad Erdan, amejibu kauli hiyo kwa kumtaka Guterres ajiuzulu, akimtuhumu katibu huyo kukubaliana na ugaidi pamoja na mauaji uliofanywa na Hamas mnamo Oktoba 7.

Erdan aliandika katika ukurasa wake kwenye mtandao wa X, zamani Twitter na akasema kauli za Guterres zina maana kwamba hafai kuuongoza Umoja wa Mataifa.

Matamshi ya Guterres pia yamemghadhabisha Waziri wa Mambo ya Nje wa Israel, Eli Cohen, ambaye amemnyooshea kidole cha lawama Guterres na kupaza sauti yake akielezea jinsi raia wakiwamo watoto wadogo, walivyouliwa Oktoba 7.

Cohen alifuta mkutano uliokuwa umepangwa kati yake na Guterres baada ya malumbano hayo.

Cohen aliandika akisema hatakutana na katibu mkuu huyo wa Umoja wa Mataifa.

"Baada ya Oktoba 7 hakuna mtazamo wenye uwiano. Hamas lazima iangamizwe kabisa katika uso wa dunia," aliandika.

Vita vyaendelea huko Gaza

Israel imeendeleza mashambulizi dhidi ya maeneo mbalimbali ya kundi la Hamas huku viongozi wa makundi matatu ya wanamgambo wa Hamas, Islamic Jihad na Hezbollah tawi la Lebanon wakikutana.

Wizara ya Afya ya Palestina ilisema jana kwamba tangu kuanza kwa vita kati ya Israel na Hamas, zaidi ya Wapalestina 100 wameuawa katika Ukingo wa Magharibi unaokaliwa kimabavu na Israel.

Hata hivyo ghasia zilikuwa tayari zimeshamiri katika ukingo huo hata kabla ya mzozo huu ulioibuka Oktoba 7.

Jeshi la Israel lilisema limezima jaribio la wapiganaji wa kundi la Hamas katika Ukanda wa Gaza waliojaribu kujipenyeza na kuingia Israel kupitia baharini.

Milio kadhaa ya risasi ilisikika na wanamgambo kadhaa wameuawa.

Kiongozi Mkuu wa kundi la Hezbollah la Lebanon amekutana na viongozi wakuu wa makundi ya wapiganaji wa Palestina wa Hamas na Islamic Jihad, ili kujadili hatua ambazo muungano wao unaweza kuzichukua ili kupata ushindi wa kweli.

Mkutano huo ambao haukutajwa ni lini na wapi ulipofanyika, uliwakutanisha Sayyed Hassan Nasrallah wa Hezbollah, Naibu Mkuu wa Hamas, Saleh al-Arouri na kiongozi wa Islamic Jihad Ziad al-Nakhala.

Kundi la Hezbollah linalomiliki silaha nyingi na ambalo linaungwa mkono na Iran limekuwa likipambana na wanajeshi wa Israel kwenye mpaka wa nchi hizo mbili tangu vita vilipozuka.

Juhudi za usuluhishi

Rais Abdel Fattah al-Sisi alisema jana kwamba Misri inatumia nafasi yake katika kujaribu kupunguza mzozo wa Gaza, huku akisisitiza kutegemea zaidi suluhisho la kidiplomasia.

Naye Kiongozi Mkuu wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, amerejelea wito wake wa kuachiwa kwa mateka wanaoshikiliwa na wanamgambo wa Hamas huku akitoa akitaka kuruhusiwa misaada ya kibinadamu kufikishwa ukanda wa Gaza.

Papa Francis pia alisema ataongoza sala maalum kwa ajili ya amani siku ya Ijumaa katika Kanisa Kuu la Mtakatifu Petro, katika kile alichokiita siku ya mfungo, sala na toba.

Jared Kushner, ambaye alishiriki katika mazunguzo ya kufikia makubaliano ya amani kati ya Israel na mataifa ya Kiarabu, alisema jana kwamba makubaliano ya Abraham yana umuhimu zaidi kwa sasa kuliko hapo awali ukizingatia mzozo huo unaoendelea Mashariki ya Kati.

Kushner ambaye alikuwa pia mshauri wa rais wa zamani wa Marekani, Donald Trump, alisema Israel inapaswa kuwa na usalama wake lakini Wapalestina hawana budi kuwa na fursa ya kuishi maisha bora.

# Liberia yaingia duru ya pili uchaguzi

**MONROVIA, Liberia**

UCHAGUZI mkuu wa Liberia duru ya pili utafanyika mwezi unaokuja, baada ya wagombea wawili Rais George Weah na mpinzani wake mkuu Joseph Boakai wote hawakupata wingi wa kura katika uchaguzi wa awali.

Rais Weah alipata asilimia 43.83 ya kura na Boakai, ambaye alikuwa makamu wa rais akipata 43.44.

Uchaguzi wa Oktoba 10 ulikuwa wa mchuano mkali zaidi wa urais nchini Liberia tangu vita vya wenyewe kwa wenyewe kumalizika takriban miongo miwili iliyopita.

Uchaguzi wa duru ya pili ulitabiriwa awali kutokana na ushindani uliopo kati ya wagombea hao, lakini Boakai (78), amefanya vyema kuliko ilivyotarajiwa kwa kukaribia kura alizopata Weah.

Katika uchaguzi huo hakuna mgombea aliyepata zaidi ya asilimia 50 ya kura katika duru ya kwanza.

Mkuu wa Tume ya Uchaguzi, Davidetta Browne alisema duru ya pili ya uchaguzi itafanyika Novemba 14, mwaka huu.

# Mwanajeshi EAC auawa DRC

**GOMA, DRC**

VIKOSI vya Wanajeshi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo katika Mkoa wa Kivu Kaskazini vinasema kundi la M23 limeshambulia kwa makombora Jeshi la Kikanda la Jumuiya ya Afrika Mashariki (ECRF) katika mji wa Kibumba.

Katika taarifa kwa vyombo vya habari iliyochapishwa kupitia X, Kanali Guillaume Ndjike, Msemaji wa Gavana wa Kijeshi wa Kivu Kaskazini aliwasilisha rambirambi zake kwa wanajeshi wa Afrika Mashariki (EACRF).

Uraia wa mwanajeshi huyo haujafichuliwa na vikosi vya wanajeshi wa Congo na EACRF bado havijatoa tamko lolote kuhusiana na shambulio hilo.

Oktoba 16, mwaka huu msafara wa kikosi cha wanajeshi wa Uganda kilichotumwa Mashariki mwa DRC kama sehemu ya kikosi cha Jumuiya ya Afrika Mashariki, ulikumbana na shambulio la kuvizia lililofanywa na watu wasiojulikana.

Tangu mwanzoni mwa mwezi huu muungano wa makundi yenye silaha, unaojulikana kama Wazalendo, limekuwa likichukua miji iliyokuwa imekabidhiwa kwa vikosi vya EAC na kundi la M23.

# IBRAHIM CLASS, MAJIHA WATAMBA KUTOA DOZI

**Na Saada Akida**

BONDIA Mtanzania Fadhili Majiha pamoja na Ibrahim Class wamesema kila mmoja yuko tayari kuibuka na ushindi katika mapambano yatakayofanyika keshokutwa kwenye Ukumbi wa PTA Sabasaba, Dar es Salaam.

Majiha atapigana na Bongani Mahlangu kutoka Afrika Kusini kuwania mkanda unaotambuliwa na WBC katika pambano la raundi 10 wakati Ibra Class yeye atachuana na Mchina Xion Tau Su.

Akizungumza na gazeti hili, Majiha amewaomba Watanzania kujitokeza kwa wingi kushuhudia atavyompiga mpinzani wake, Mahlangu na kuipa heshima taifa lake.

Majiha alisema amejipanga vyema kuubakisha mkanda huo Tanzania katika pambano hilo la raundi zote 12.

"Nimejipanga kucheza ndani ya kiwango, Mahlangu mara nyingi anakuja nchini kupigana na mabondia wa kawaida, awamu hii amekutana na kisiki," alitamba Majiha.

Naye Ibrahim Class amesema amejipanga vyema kuhakikisha anaibuka na ushindi katika pambano hilo lisilokuwa na kuwania mkanda.

Class alisema tayari amemaliza programu yake ya mazoezi kuelekea pambano hilo na sasa anasubiri siku ifike na anaamini ataipeperusha vyema bendera ya Tanzania.

"Nimejiandaa vizuri kupambana na mpinzani wangu kwa sababu nilikaa kambini Tanga na sasa kazi iliyobaki ni kupanda ulingoni kufanya kazi yangu kwa kumpiga mpinzani," alisema bondia huyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa HD SADIC, Hamisi Kumbucha, ambao ndio waandaaji alisema baada ya kumaliza pambano hilo kampuni yao inajipanga kuendelea kuandaa mapambano mengine ambayo yatasaidia kuwanyanyua mabondia wa nchi za Ukanda wa SADC.

"Kwa mara ya kwanza Tanzania linachezwa pambano la kuwania mkanda wa ubingwa wa WBC Afrika kupitia bondia Fadhili Majiha ambaye atacheza na Bongani Mahlangu kutoka Afrika Kusini," alisema Kumbucha.

Alitaja mabondia wengine watakaopanda ulingoni siku hiyo ni Nasib Ramadhani dhidi ya Zolisa Batyi, Stumai Muki dhidi Loveleen Thaakur, Luqman Ramadhani vs Athony Matheasi, Shomary Milundi vs Nordin Makame, John Chua vs Richard Mkude, Laylah Macho vs Fatuma Juma, Hamza Chanjo dhidi ya Issa Mollel.



Wachezaji wa Prisons ya Mbeya wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC FC itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# Wachezaji Bandari wapewa neno

**Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), imewataka watumishi wote wanaoshiriki michezo ya 17 ya Bandari (Interports Games 2023) kuipokea kwa mikono miwili hatua ya kihistoria ya kusainiwa kwa mikataba ya ushirikiano kati ya mamlaka hiyo na Kampuni ya DP World ya Dubai.

Naibu Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Mhandisi Juma Kijavara, alisema hayo katika ufunguzi rasmi wa michezo ya Bandari inayofanyika kwenye viwanja mbalimbali katika mkoa wa Morogoro.

"Michezo ya mwaka huu imefunguliwa siku moja tu baada ya tukio kubwa la kihistoria la kusainiwa kwa mikataba ya ushirikiano kati ya TPA na Kampuni ya DP World ya Dubai, tukio lililofanyika Ikulu ya Chamwino Dodoma, Oktoba 22, mwaka huu.

Nami nitumie fursa hii kuwaagiza watumishi wote wanaoshiriki michezo hii, kuipokea kwa mikono miwili hatua hii na kutoa ushirikiano wote ili kuendelea kuwa na utendaji wenye ufanisi Katika sehemu zetu za kazi," alisema Kijavara.

Katika michezo ya juzi, upande wa netiboli, Bandari ya Dar es Salaam ilifungwa magoli 34-31 dhidi ya Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC) huku TPA Makao Makuu ikipata ushindi wa magoli 35-20 dhidi ya Bandari Mtwara na katika kikapu TPA Makao Makuu wakipata ushindi wa vikapu 102 kwa 46 dhidi ya Bandari za Maziwa, huku kwenye wavu Makao Makuu wakiwanyoosha seti 2-0 wenzao wa Bandari za Maziwa.

Wakati huo huo, Kocha Mkuu wa Timu ya Netiboli ya Bandari Dar es Salaam, Judith Ilunda, amesema anatumia mashindano hayo kwa ajili ya kujiandaa na Ligi Daraja la Pili Taifa.

## New City mambo magumu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MZIMU wa matokeo mabaya umeendelea kuitesa New City FC baada ya kukubali kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Maendeleo katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau A juzi usiku.

New City inapoteza mchezo wa pili mfululizo katika ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa New City, Razak Salum, alisema licha ya kuonekana kikosi chake kimeimarika, lakini bado idara ya ushambuliaji imekuwa na tatizo la kushindwa kutumia nafasi wanazopata.

Salum alisema ameshaanza kufanyia kazi mapungufu hayo na anaamini watazinduka katika mechi zinazofuata na kufufua matumaini mapya katika msimu huu.

"Tumecheza michezo nane na makosa yote ni yale yale yanajirudia, bado umakini unahitajika kwa upande wa washambuliaji na walinzi wetu, pia lazima wachezaji wangu wanahitaji kuongeza ujanja wa kufanya uamuzi pale tunaposhambuliwa," aliongeza kocha huyo.

## Ruvu Shooting FC yaisimamisha TMA

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Ruvu Shooting imepata sare ya kwanza dhidi ya TMA na kuwazuia wenyeji kurejea kileleni katika msimamo wa Ligi ya Championship inayoendelea katika viwanja mbalimbali.

Kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha juzi, bila kutarajia Ruvu Shooting ilikomaa na kutoka sare ya bila kufungana na TMA, ikiwa ni ya kwanza baada ya kupata vipigo katika mechi zote zilizopita.

Timu hiyo imepoteza mechi sita mfululizo kabla ya kufanikiwa kupata suluhu ya ugenini dhidi ya wenyeji ambao walikuwa wakiongoza ligi hadi kufikia raundi ya sita kabla ya KenGold kuchukua nafasi hiyo baada ya kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Cosmopolitan.

Ruvu Shooting ambayo ilishuka daraja msimu uliopita, inaburuza mkia ikiwa na pointi moja.

Matokeo ya mechi nyingine katika ligi hiyo FGA Talents ikiwa nyumbani kwenye Uwanja wa Jamhuri, Morogoro ililazimishwa suluhu dhidi ya Stand United.

## ZISIKUPITE

### MUSIALA KUONDOKA BAYERN

WINGA wa Bayern Munich na Ujerumani, Jamal Musiala mwenye miaka 20 anaweza kufikiria kuhamia Manchester City au Real Madrid ikiwa anahisi malengo yake ya kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ballon d'Or hayana uhalisia tena akiwa klabuni hapo. **(Sky Sports)**

### PHILLIPS ATAJWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inaweza kufufua nia yao ya kumnunua kiungo wa kati wa Manchester City na England, Kalvin Phillips mwenye umri wa 27, ikiwa wataamua kumsajili kwa muda mfupi ili kufidia kutokuwepo kwa mchezaji wa kimataifa wa Italia, Sandro Tonali. **(Mail)**

### NEWCASTLE YASAKA VIUNGO

VIUNGO walioko katika rada ya Newcastle United kuchukua nafasi ya Sandro Tonali, ambaye anakabiliwa na marufuku ya kuvunja sheria za kamari, ni pamoja na nyota wa Manchester United Scott McTominay (26), wa Scotland, nyota wa Everton na Ubelgiji, Amadou Onana (22), na Mreno Joao Palhinha (28). **(The Athletic)**

### TONALI NJE MIEZI 10

SANDROTonali wa Newcastle mwenye umri wa miaka 23, anakabiliwa na marufuku ya miezi 10 ambayo itamfanya kukosa msimu uliosalia na Euro 2024, ikiwa Italia itafuzu baada ya uchunguzi wa tuhuma za makosa ya kamari. **(Sky Italy)**

### RAMSDALE ANUKIA CHELSEA

CHELSEA iko tayari kujaribu kumnunua kipa wa England na Arsenal, Aaron Ramsdale mwenye umri wa miaka 25, ambaye amepoteza nafasi yake kwa mchezaji kwa David Raya katika kikosi cha Mikel Arteta msimu huu. **(Daily Mail)**

### WILLIAMS AGOMBEWA EPL

KLABU za Arsenal, Liverpool na Tottenham Hotspur zinavutiwa na winga wa Athletic Bilbao ambaye ni raia wa Hispania, Nico Williams. Aston Villa pia ilijaribu kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. **(90min)**

### SANCHO KUONDOKA UNITED

JADON Sancho mwenye umri wa miaka 23, huenda akaruhusiwa kuondoka Manchester United kwa "mkopo wa muda mrefu" Januari huku klabu ya winga huyo wa zamani wa England, Borussia Dortmund ikiongoza mbio hizo za kumwania. **(90min)**

### GUIRASSY AWANIWA FULHAM

KLABU ya Fulham inataka kumsajili fowadi wa Stuttgart na Guinea, Serhou Guirassy mwenye umri wa miaka 27, ambaye amefunga mara 14 kwenye Bundesliga msimu huu, zikiwemo hat-trick mbili. Guirassy ana kifungu cha kutolewa cha zaidi ya pauni milioni 15. **(Standard)**

### CATAMO ANUKIA VILLA

KLABU ya Aston Villa inamfuatilia winga wa Sporting Lisbon na Msumbiji, Geny Catamo mwenye umri wa miaka 22. **(Birmingham Live)**

### DAU LA DIAZ LAANIKWA

ASTON Villa na West Ham wameambiwa na Real Madrid lazima walipe takriban euro milioni 20 kama wanataka kumsajili kiungo mshambuliaji mzaliwa wa Hispania, Brahim Diaz mwenye miaka 24. **(Birmingham Mail).**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA AHOFIA JERAHA LA JESUS

Ni baada ya mshambuliaji huyo Mbrazil kuomba...

**SEVILLE, Hispania**

MIKEL Arteta alionyesha wasiwasi wake juu ya jeraha la msuli la, Gabriel Jesus baada ya mshambuliaji huyo wa Arsenal kutolewa nje dakika ya lala salama wakati wa ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Sevilla, juzi

Mbrazil huyo alihusika katika mabao yote mawili ya Washikabunduki akimtengenezea, Gabriel Martinelli katika dakika za lala salama kabla ya kuukwamisha mpira kwenye kona ya juu ya goli.

Sevilla walipata bao moja kupitia kwa Nemanja Gudelj lakini Arsenal wakaondoka na pointi tatu muhimu za Ligi ya Mabingwa Ulaya, ingawa kutolewa kwa Jesus kumeibua wasiwasi kwa Arteta kabla ya mechi ya Jumamosi dhidi ya Sheffield United.

Bosi huyo wa Arsenal mwenye umri wa miaka 41, alisema: "Jesus alihisi kitu kwenye msuli wa paja, lakini ngoja tuone.

Moja kwa moja aliomba kutolewa, habari ambayo si njema kwa sababu yeye si mchezaji anayefanya hivyo hata kidogo hivyo itabidi tusubiri na kuona siku chache zijazo."

Arteta alijawa na sifa za kuonyesha Jesus na kuongeza: "Unahitaji nyakati za michezo kama hii na unahitaji wachezaji wakubwa kuingilia kati na kuunda nyakati hizo."

Kocha huyo pia alichukua muda kuwapongeza wachezaji wake wengine.


Alisema: "Nimefurahi sana kushinda hapa. Hakuna timu nyingi zilizoshinda hapa katika miaka kumi iliyopita katika michuano ya Ulaya lakini sisi tumefanikiwa.

"Niliipenda sana timu, hasa dakika 60, 65 za kwanza kwa sababu tulicheza mchezo tunaotaka, baada ya kwenda mbele kwa mabao 2-0 tulipaswa kufunga la tatu na tukapata nafasi za kufunga na hatukufanya hivyo.

"Katika kona moja, hatua ya kwanza ambapo walikuwa na kitu walifunga na kutoka hapo, wana uzoefu, wana watu wengi na imani kubwa wanaweza kupata kwenye mchezo."

Arsenal sasa wanaongoza kundi lao katika michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya Lens na PSV Eindhoven kutoka sare ya bao 1-1.

# MAGUIRE, ONANA WAIBEBA UNITED




**MANCHESTER, England**

ERIK ten Hag alimsifu, Harry Maguire wakati beki huyo wa kati wa Manchester United alipofunga bao pekee kwenye ushindi wa 1-0 dhidi ya FC Copenhagen katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa juzi usiku.

United waliepuka matokeo mengine ya kukatisha tamaa kwenye Uwanja wa Old Trafford huku Maguire akifunga bao hilo dakika ya 72 kabla ya Andre Onana kuokoa penalti katika mechi hiyo.

Maguire amerejea kwenye kikosi cha Ten Hag katika michezo ya hivi karibuni na bosi huyo anaamini nyota huyo wa kimataifa wa England anaonyesha maboresho makubwa.

Akimzungumzia beki huyo kwenye mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi iliyofanyika kwenye Uwanja wa Old Trafford, Ten Hag alisema: "Anacheza kwa umakini zaidi katika kumiliki mpira, kuingia na kupiga pasi. Pia kwa mguu wa mbele, pia akipiga hatua katika kulinda mbele, anajiamini sana.

Nadhani anatawala katika wakati muafaka. Anatawala wapinzani wake. Na kisha unaona anapata thawabu na bila shaka, kuongoza ni ujuzi mzuri sana kutoka kwake."

Jioni hiyo pia itahisi tamu sana kwa Onana, ambaye bila shaka alifurahia wakati wake bora zaidi akiwa na jezi ya Mashetani Wekundu hadi leo baada ya kuanza kwa shida tangu kuhama kwake kwa pauni milioni 47 kutoka Inter Milan.

Ten Hag alisema, kuhusu mlinda mlango wa Cameroon: "Huo ni moja ya ujuzi wake. Ni mwokoaji mzuri sana wa penalti.

"Na pia usisahau kuokoa maisha baada ya muda wa mapumziko kwenye shambulio la kaunta."

Ingawa kampeni ya United ya Ulaya hatimaye imeanza na kuendelea, ushindi huo mdogo hauwezekani kusitisha ukosoaji kuja baada ya maonyesho mengine yasiyoridhisha.

Ten Hag aliongeza: "Kipindi cha kwanza hakikuwa kizuri.

"Ilikuwa ngumu kwa sababu Copenhagen walikuwa wamejipanga vyema. Ilikuwa vigumu kutengeneza nafasi.

"Nusu ya pili nadhani ilikuwa bora zaidi. Kujenga kulikuwa bora zaidi."

# Mwenyekiti wa Everton afariki

**LIVERPOOL, England**



MWENYEKITI wa Everton, Bill Kenwright amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 78, klabu hiyo ya Ligi Kuu England, imetangaza

Kenwright ambaye alikuwa mtayarishaji wa filamu ndiye mwenyekiti aliyehudumu kwa muda mrefu zaidi wa Everton katika zaidi ya karne moja baada ya kumrithi, Philip Carter, mwaka 2004.

Aliaga dunia kwa amani Jumatatu usiku, akiwa amezungukwa na familia yake na wapendwa wake, Everton alisema.

"Klabu imepoteza mwenyekiti, kiongozi na rafiki," taarifa ya klabu ilisema.

Katika misimu yake 19 kama mwenyekiti, Everton ilipata nafasi 12 za juu, ikiwa ni pamoja na nafasi ya nne mwaka wa 2005. Pia walifika fainali ya Kombe la FA mwaka 2009 na kufuzu kwa mashindano ya Ulaya mara sita.

Kenwright, shabiki wa muda mrefu wa Everton ambaye alihudhuria mara kwa mara michezo ya timu hiyo kwenye Uwanja wa Goodison Park, alijiunga na bodi ya klabu ya Kaskazini-Magharibi mwaka wa 1989, alinunua hisa za asilimia 68 mwaka 1999 na akawa mwenyekiti miaka mitano baadaye.

Ilikuwa ni nafasi ambayo bado alishikilia hadi kifo chake, licha ya msukosuko wa miaka michache iliyopita chini ya mmiliki wa Everton, Farhad Moshiri, ambaye amekuwa akitafuta kuiuza klabu hiyo na hivi karibuni akabadilisha bodi.

Wayne Rooney, nguli wa England na Manchester United ambaye alifanikiwa kuingia Everton akiwa na umri wa miaka 16, aliandika kwenye X, zamani Twitter, Kenwright "Mtu mkubwa na msukumo mkubwa."

Kenwright, ambaye alizaliwa Liverpool, alianza kazi yake ya showbiz kama mwigizaji na alionekana katika opera ya sabuni "Coronation Street" mwishoni mwa miaka ya 1960, akirudi kwa kuonekana mara kwa mara kwa miaka mingi baada ya kuhamia katika utayarishaji wa filamu.

Alikua mmoja wa waigizaji wakubwa wa Jukwaa la Uingereza, akifanya maonyesho katika West End ya London na kwenye Broadway -- baadhi ya miondoko, nyimbo nyingi, ikiwa ni pamoja na "Blood Brothers," iliyofanyika kwa miaka 24, na utayarishaji wa utalii wa "Joseph and the Dreamcoat ya ajabu ya Technicolor." Miongoni mwa maonyesho yake ya hivi majuzi kama mtayarishaji ni "Heathers: The Musical.

# Bellingham fiti kuivaa Barcelona

**LONDON, England**

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti alisema kiungo nyota, Jude Bellingham yuko fiti baada ya kubadilishwa dakika ya 89 katika ushindi wa mabao 2-1 wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Braga, mechi iliyochezwa Jumanne usiku.

Bellingham aliifungia Madrid bao la pili na kuisaidia timu yake kupata ushindi unaowafanya waendelee kubaki na pointi tisa kileleni katika Kundi C kupitia mechi tatu kabla ya Clasico dhidi ya Barcelona.

"Yuko sawa," Ancelotti alisema alipoulizwa kwa nini Bellingham alibadilishwa.

Rodrygo aliiweka Madrid mbele dakika ya 16 kwa shuti kali kutoka ndani ya eneo la hatari, bao lake la kwanza tangu Agosti, mwaka huu baada ya kukimbia kwa Vinícius Júnior chini upande wa kushoto, na Bellingham akaongeza bao la kuongoza dakika ya 61 kwa shuti hafifu ndani ya eneo la hatari.

"Lakini tulicheza vizuri na kufunga mabao kwa nafasi tulizotengeneza. Na tungeweza kufunga zaidi. Ni lazima tuendeleze mchezo huu baada ya kushinda mechi tatu za kwanza." alisema Vinicius.

Bellingham (20), amefunga katika kila mechi kati ya mechi tatu za kwanza za Ligi ya Mabingwa kwa msimu wa pili mfululizo, baada ya kufanya vivyo hivyo na Borussia Dortmund msimu wa 2022-23.

Alidhibiti kasi ya mchezo kwenye eneo la kiungo na kuisaidia Madrid kutawala mapema. Braga, ambayo ilikuwa imeshinda mechi tano mfululizo katika mashindano yote, haikuwa na majaribio yoyote ya kulenga goli katika kipindi cha kwanza.

Vinara hao wa LaLiga sasa watajiandaa kwa mechi yao ya kwanza dhidi ya Barcelona msimu huu, huku Madrid wakiwa mbele kwa pointi moja dhidi ya miamba hao wa Katalunya baada ya mechi 10 walizocheza.



# TWIGA STARS, BOTSWANA MECHI YA KISASI OLIMPIKI

**Na Saada Akida**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars) inatarajia kuwakaribisha Botswana katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Michezo ya Olimpiki itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Michezo ya Olimpiki itafanyika mwakani jijini Paris Ufaransa.

Hata hivyo, mshindi wa jumla kati ya Twiga Stars na Botswana atakuwa amefuzu raundi ya pili ya mashindano hayo baada ya Congo Brazaville kujiondoa katika michuano hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Twiga Stars, Bakari Shime, alisema wanafahamu umuhimu wa mchezo huo na wamejiandaa vyema kuwakabili wapinzani wao na hatimaye kusonga mbele.

Shime alisema mechi hiyo haitakuwa nyepesi kwa kila upande na kila mchezaji wake yuko tayari kwa ajili ya kupambana kusaka ushindi.

"Tumejiandaa vyema na wachezaji wako tayari kuhakikisha wanapata ushindi hapa nyumbani. Tunajua umuhimu wa mashindano haya, hivyo tunawaalika mashabiki kufika kwa wingi Chamazi kutushangilia," alisema Shime.

Naye nahodha wa timu hiyo, Amina Bilali alisema wamefanya mazoezi ya kutosha na wanachosubiria ni muda wa mchezo huo ili kuwapa furaha Watanzania.

Amina alisema anajua Botswana ina kikosi imara na wao wataingia katika mechi hiyo kwa lengo moja la kusaka ushindi.

"Tumejiandaa vizuri kwa ajili ya mchezo huo na tunatarajia kufanya vizuri kwa sababu tayari benchi la ufundi limefanyia kazi mapungufu yetu, kazi kubwa imebaki kwetu kuendelea kuwapa furaha Watanzania," alisema Amina.




Kikosi cha Timu ya vijana ya Namungo (U-20), kilichoanza katika mechi dhidi ya KMC iliyochezwa kwenye Uwanja wa Kituo cha TFF Kigamboni, Dar es Salaam jana asubuhi. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: TFF**

# Kiluvya, Malimao 'zaua' Daraja la 2

**Na Adam Fungamwango**

TIMU za Kiluvya FC na Malimao zimeanza kwa kishindo Ligi Daraja la Pili 'First League' kwa kupata ushindi wa mabao 3-0 kila moja kwenye mechi zao za ufunguzi za ligi hiyo.

Katika ligi hiyo inayochezwa kwa makundi mawili, kila kundi ikiwa na timu nane kwa ajili ya kusaka timu tatu zitakazokwenda kucheza Ligi ya Championship msimu ujao, Kiluvya iliwachapa Dar City mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Mabatini, Mlandizi, Pwani huku Malimao ilioyokuwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam iliwafunga Tunduru FC.

Mechi zote zilikuwa za Kundi A, ambapo mbali na hizo, pia kuna timu za Nyumbu FC, African Lyon, Lipuli na African Sports.

Katika mechi za kundi B, Kurugenzi FC ikiwa nyumbani kwenye Uwanja wa Kambarage, Shinyanga, ilijikuta ikiangukia pua kwa kuchapwa mabao 2-0 dhidi ya Mapinduzi FC, TRA ikaibamiza Alliance FC magoli 2-0 kwenye Uwanja wa Ushirika, Moshi, Kilimanjaro na Tanesco ikakubali kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa Kasulu United, mechi ikifanyika kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma.

Ligi hiyo inatarajiwa kuendelea tena wakati timu mbili za taasisi za serikali, Tanesco itawakaribisha TRA kwenye Uwanja wa Ushirika, Moshi.

## Robertinho: Al Ahly wametupa 'darasa'

INATOKA UK. 24

inapaswa kupongezwa na kuheshimiwa kwa kuonyesha maendeleo makubwa katika mechi za kimataifa kutokana na kuweka rekodi ya kutoa sare kwa mara ya kwanza ikiwa Misri na kufunga bao dhidi ya mabingwa hao wa Afrika.

Ahmed alisema kama si kanuni ya faida ya mabao ya ugenini, basi mechi hiyo ingekwenda kwenye hatua ya penalti na lolote lingeweza kutokea.

"Mnyama aheshimiwe, leo (juzi) Mwarabu ameomba poo. Kuna hatua kubwa sana imepigwa na klabu za Tanzania licha ya baadhi ya watu kugoma kuona, kuna sehemu ndogo sana tunakwama kiufundi ila tunaiona kesho bora mbele yetu," alisema Ahmed.

Aliongeza kama kuna nyakati ambazo wanachama na mashabiki wa Simba wanapaswa kujivunia ni kipindi hiki kwa sababu miaka ya nyuma timu hiyo ilikuwa inapata tabu hata kupata sare ikiwa ugenini dhidi ya Al Ahly.

"Miaka miwili iliyopita ilikuwa tabu hata kupata sare kwenye Uwanja wa Cairo nchini Misri dhidi ya Al Ahly, lakini leo watu wameshuhudia dakika 90 zilizokuwa chungu wa Al Ahly, iliwalazimu kusawazisha bao ili kuelekea kwenye raundi inayofuata, miaka mingi imepita Simba haijawahi kupata bao Misri," alisema Ahmed.

Aliongeza kutolewa kwa kufuata kanuni kunaonyesha ukubwa wa Simba na wala viwango vya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), haviongopi kuiweka kwenye nafasi ya nane.

"Lakini leo tunapata bao nyumbani kwao timu namba moja barani Afrika, kama tungekuwa na nguvu ya kuhimili presha basi tusingeweza kuruhusu bao, Simba ya jana siyo ya leo na ya leo haitakuwa ya kesho, tunaonekana tunapiga hatua kubwa, tumeondolewa mashindanoni pasipo kufungwa," alisema kiongozi huyo.

Katika hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba iko Kundi B pamoja na Wydad Cassablanca, Asec Mimosas na Jwaneng Galaxy.

## Gamondi afunguka kibarua cha mabeki

INATOKA UK. 24

mbele yetu ikiwamo dhidi ya Singida Fountain Gate FC, ni timu ngumu na tunahitaji kupambana kupata matokeo mazuri ili kujihakikishia kubaki katika nafasi ya juu," aliongeza kocha huyo ambaye amepoteza mechi moja tu msimu huu.

Baada ya mechi hiyo dhidi ya Singida Fountain Gate, Yanga itaanza maandalizi ya kukutana na Simba katika mechi ya mzunguko wa kwanza itakayochezwa Novemba 5, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Michezo

Alhamisi Oktoba 26, 2023
Nipashe



## Arteta ahofia jeraha la Jesus

UKURASA 21



Straika wa Simba, John Bocco (katikati), akijiandaa kuwatoka nyota wa Al Ahly katika mechi ya mashindano ya African Football League iliyochezwa kwenye Uwanja wa Cairo, Misri juzi. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: SIMBA SC**

# ROBERTINHO: AL AHLY WAMETUPA 'DARASA'

## Mabosi wataka sasa Simba iheshimiwe kutokana na...

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

LICHA ya timu yake kutolewa katika mashindano ya African Football League, Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho', amesema kikosi chake kimeonyesha ubora mkubwa katika mechi waliyocheza dhidi ya vigogo wa Afrika, Al Ahly ya Misri.

Simba imeondolewa katika michuano hiyo inayofanyika kwa mara ya kwanza kwa Al Ahly kuwa na faida ya magoli ya ugenini, walitoka sare ya mabao 2-2 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na Mnyama akalazimisha sare ya goli 1-1 ilipokuwa ugenini Misri.

Tayari kikosi cha Simba kimesharejea nchini kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ambapo keshokutwa itawakaribisha Ihefu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Akizungumza na gazeti hili, Robertinho alisema Al Ahly imewapa kazi maalumu ya kufanya ili kuwa bora zaidi.

Robertinho pia amewashukuru wachezaji wake kwa kujituma na kucheza kwa nidhamu kubwa katika mchezo wa marudiano.

Mbrazili huyo alisema wametolewa kwenye mashindano hayo na timu kubwa Afrika lakini Simba nao imeonyesha ukubwa wao katika michezo yote miwili waliyokutana.

"Tulikuwa kwenye ubora mkubwa, lakini yapo maeneo lazima tuongeze uimara, yapo makosa madogo madogo katika namna ya kujilinda, tutafanyia kazi mapungufu kidogo tuliyoyaona, lakini kwa ujumla timu imecheza vizuri. Nawasifu na najivunia wachezaji wangu kwa kile walichokionyesha," alisema Robertinho.

Aliongeza kuondolewa katika michuano hiyo sasa kunawapa nafasi ya kujikita kwenye michuano mingine wanayoshiriki na watayafanyia kazi mapungufu kwa ajili ya kufanya vizuri na hatimaye kufikia malengo.

"Tunarejea nchini kuendeleza harakati zetu za kufanya vizuri kwenye Ligi Kuu msimu huu, lakini tupo kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, naamini tutakuwa bora zaidi," Robertinho alisema.

Aliongeza mashindano ya AFL yamewaongezea 'kitu' wachezaji na timu kwa ujumla kuelekea kwenye michezo ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Mchezo na Al Ahly ni mchezo mkubwa, mchezo dhidi ya timu kubwa na imara, kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi tutacheza michezo inayofanana na huu, hivyo umetupa kitu kama timu," aliongeza kocha huyo.

Naye Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema timu yake

INAENDELEA UK. 23

# Gamondi afunguka kibarua cha mabeki

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi sasa amewageukia mabeki wake kwa kuwataka kuwasaidia mastraika na viungo kufunga mabao katika mechi zinazofuata za mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Yanga inatarajia kuwakaribisha Singida Fountain Gate katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Gamondi aliliambia gazeti hili anataka kuona mabeki wake wanatumia nafasi wanazopata kufunga mabao hasa wanapokuwa ndani ya eneo la 18 la timu pinzani na si kuwaachia jukumu hilo mastraika au viungo pekee.

Kocha huyo alisema moja ya jukumu kubwa ambalo lipo mbele yake ni kuhakikisha wanafanya vizuri katika michezo hiyo na kuwataka wachezaji wake kupunguza presha ya mbio za kutetea ubingwa.

Alisema kikubwa anataka kuona mabeki wake wakifunga na kutengeneza nafasi za mabao kutokana na uwezo mkubwa waliokuwa nao na wasitegemee mchezaji mmoja au mshambuliaji kukamilisha jukumu hilo.

"Kikosi changu nataka kila mchezaji anayepata nafasi ya kufunga aitumie vizuri ikiwamo mabeki, kuna timu inatengeneza mabao kupitia pembeni, nimewaongezea mabeki mbinu za kufunga mabao, sio tu kutengeneza mabao pekee.

Ukweli ligi ni ngumu, lakini hatuwezi kusema tunataka kurudi nyuma kwa sababu hizi mechi ambazo zipo mbele yetu zinahitaji kupata matokeo mazuri," alisema Gamondi.

Aliongeza anataka kuona timu yake inashinda na kila mchezaji hasa mabeki wanafunga magoli ili kufikia malengo ya klabu.

"Tumejipanga vizuri, tunahitaji kushinda mechi zote zilizopo

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >